**29 APRILI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 29 Aprili, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali. Waheshimiwa Wabunge Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimwite sasa Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 167

**Wazee Kuwekwa kwenye Mfumo wa Hifadhi ya Jamii**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha Wazee kuanzia umri wa miaka 60 nchini wanaingia katika Mfumo wa Hifadhi ya Jamii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Patrobass Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 wanaendelea kunufaika na Mfumo wa Hifadhi ya Jamii hapa nchini, Serikali imeweka utaratibu wa kuwawezesha wazee waliokuwa katika Sekta Binafsi kuendeleza uanachama wao katika Mfuko wa *NSSF* hadi kufikia miaka 70. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tauhida.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je; kuna

maslahi yapi ya ziada ambayo Serikali inayatoa mahususi kwa ajili ya wazee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kinga zipi za wazee zinazolindwa kisheria na Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida. Kwanza; nimshukuru na kumpongeza kama jinsi wanavyofanya Waheshimiwa Wabunge wengine, lakini yeye amekuwa mahiri sana katika kutetea haki za wazee na makundi maalum hasa yakiwemo wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali lake ni kwamba kwa upande wa Serikali, maslahi yanayotolewa kwa wazee mojawapo ni pamoja na kuangalia ustawi wao katika masuala ya afya na ya kiuchumi. Katika Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kusimamia vizuri sana mpango uliopo wa kuendeleza kaya maskini au duni kwa Mpango wa *TASAF* kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa pia na mpango wa matibabu bure ambao ni maslahi ambayo wazee wamekuwa wakinufaika nayo ikiwa ni pamoja na kutambua changamoto za wazee na kuweza kuwasaidia kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba, kuna mpango wa msamaha. Kwa mfano, maslahi ya kikodi ya ardhi, wazee wanasamehewa kulingana na umri ambao umekuwa *justified* kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huduma za upendeleo ambayo ni maslahi wazee wamekuwa wakiyapata, mojawapo ikiwa ni kutoa upendeleo kwenye maeneo ya misongamano labda pale kunapohitaji huduma ya jamii kama vile kwenye kupiga kura, zoezi kubwa ambalo litampa ushindi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; wazee watatangulia mbele kupiga

kura. Pia, huko hospitali kwenye matibabu ni moja ya maslahi ambayo wazee wanapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali lake la pili la kuhusiana na kinga za kisheria ambazo wazee wanazo. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Katiba yake ya Mwaka 1977 inatoa haki kwa wazee. Katika Ibara ya 11(1) inaeleza kuhusiana na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii hasa kwa kundi la wazee, lakini pia na wakati wa maradhi au watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Tanzania imekuwa nchi ya pili na ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa na Sera mahususi ya Wazee ya Mwaka 2003 na sasa tupo kwenye mchakato kupitia Wizara husika ya kwenda kupata Sheria ya Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii imeweka maainisho ya kuzitaka Mamlaka za Serikali; Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pia upande wa familia na mawakala wa hiyari kuhakikisha kwamba wanaangalia kwanza kuwatambua wazee na kuhakikisha kuna matunzo kwenye masuala ya umaskini, huduma za afya, ushirikishwaji pamoja na uundaji wa mabaraza ya wazee, ili kuweza kuhakikisha kwamba wanahudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi niishie hapa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali lakini hapa wazee aliowazungumza ni wale waliopo kwenye Sekta Binafsi. Wapo wazee ambao wamekuwa na mchango mkubwa wa uzalishaji katika Taifa letu, lakini wapo katika sekta isiyo rasmi. Serikali haioni sasa kwamba, kuna umuhimu wa kuja na mpango madhubuti unaoeleweka tofauti na hii mipango ambayo mingi inaonekana ipo katika huruma zaidi na siyo katika sheria?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi, Serikali imeweka mpango siyo tu kwa wazee walio katika Sekta Binafsi, wameangaliwa pia wazee wastaafu ambao walikuwa kwenye utumishi wa umma. Pia, wameangaliwa wazee ambao wapo katika sekta zisizo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo kupitia Mfuko wa *NSSF* kupitia hili Bunge lako Tukufu tulibadilisha sheria hapa na tukaweka utaratibu wa kwamba, mafao sasa na masuala ya uchangiaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hata mtu yeyote ambaye alikuwa kwenye Sekta Binafsi, Utumishi wa Umma au alikuwa nje ya mfumo wowote ule, ana uhiyari wa kuweza kuchangia kwenye huu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, ili aweze kupata masurufu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ile Sera ya Wazee inajumuisha wazee wote bila kubagua ikiwa ni pamoja na kama nilivyosema awali, takwa la Ibara ya 11(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, haya maslahi ni ya wazee wote nchini kwa kuangalia kulingana na hali na tuna jukumu kubwa la kuwatambua kwa hali zao na sifa zao za kiuchumi na hali walizonazo, ili waweze kuhudumiwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kama swali la msingi linavyosema kuna wazee zaidi ya 60%, tunafahamu kilimo ndicho kinatumika katika Taifa letu. Hawa wazee ambao wamelisaidia Taifa hili kwa kilimo na leo hii wamekuwa wazee wananufaikaje na *NSSF,* ili waweze na wao kuendeleza maisha yao? Hatuoni kuna haja ya kubadilisha hizi kanuni na kuwaona kundi kubwa hili la wazee ambao wapo vijijini wanahitaji kupata mafao ya aina hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu ya swali la msingi na kwenye hatua ya pili ni kwamba hata hao wazee walio kwenye kilimo, ambao ndio tunasema sekta isiyo rasmi, ni rasmi kwa maana ya kutambulika kwa sababu ina Wizara yake mahususi, tunawatambua. Hata *NSSF* kwa sasa mtu yeyote ili mradi tu amekidhi masharti na vigezo ambavyo vipo hasa kwa kuangalia umri na utu uzima, anaruhusiwa kupeleka michango yake *NSSF* kwa kiwango ambacho itakuwa ni kulingana na uwezo wake wa kiuchumi. Kwa hiyo, tunawaangalia kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pia kwenye huduma nyingine za kiupendeleo zote hizi zinawagusa wazee katika sekta zote. Tulichobakiza ni hiyo hatua ya kwenda kutunga sheria, ili mambo haya yaweze kusimamiwa na kutekelezwa kwa kadri ambavyo sera inataka. Pili, kuweka ule umuhimu na msisitizo wa mamlaka za Serikali kuu na Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia vizuri na kuratibu utoaji wa huduma za wazee.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania Visiwani, wazee wanapata posho kutokana na sera ya kule. Je, hatuoni kwamba kuna umuhimu sasa na Tanzania Bara kukawa na sera ya kuwapatia posho wazee? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la Mheshimiwa Mnzava, ni kweli kwa upande wa Tanzania Visiwani wameanza utaratibu huo na sisi kwa sera yetu hii ambayo ni ya mwaka 2003, moja ya maeneo ambayo yamewekewa mkazo ni pamoja na hili la kuangalia hali

za kiuchumi na kuwanusuru wazee katika lindi la umaskini na changamoto za kiuchumi. Kwa hivyo, nimelipokea na tutaendelea kulifanyia kazi kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara husika, ili kuweza kuona hali ya kiuchuni kama itaruhusu basi hiyo itatekelezwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kasalali Mageni, kwa kifupi.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la manyanyaso na usumbufu kwa wazee wastaafu kwenye nchi hii limekuwa ni utamaduni wa kawaida wanavyokuwa wanafuatilia mafao na stahiki zao. Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kutunga sheria kali inayotoa adhabu moja kwa moja kwa mtumishi au afisa yeyote wa Mamlaka ya Hifadhi ya Jamiii anayenyanyasa na kuchelewesha mafao ya mzee? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitambue kweli masuala ya unyanyasaji kwa kipindi cha nyuma yalikuwepo kwa sababu kumnyima mtu haki yake au kutokumlipa mtu ujira wake kabla jasho halijakauka ni sawa na kumnyanyasa au kumwonea na kuvunja haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu tulishafanya marekebisho hapa ya Sheria ya *NSSF* na *PSSSF* ambazo zinamtaka mwajiri kwanza kuwasilisha michango ya mfanyakazi kwa wakati. Hatua ya pili, ndani ya siku 30 baada ya kustaafu anapaswa kuwa amelipwa mafao yake. Hilo jambo linasimamiwa kisheria na uzoefu uliopo sasa kwa sababu ya teknolojia kubwa na mapinduzi ya TEHAMA kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alielekeza na tumetenga fedha. Tayari tumeshaanza kuwalipa hata kabla ya siku saba, mtu anapata mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la namna ambayo nimeeleza kwamba sheria kuchukua hatua kali. Sheria hii inataka pia Mfuko

wenyewe wa *NSSF* ama *PSSSF,* ikitokea mwajiri hakuwasilisha michango, anaweza kupelekwa Mahakamani *by summary suit,* akaenda kushtakiwa na kuchukuliwa hatua kali ili kuweza kulinda haki na stahiki za hawa wafayakazi wastaafu.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Vijijini, aulize swali lake.

Na. 168

**Kukamilisha Stendi ya Ngangamfumuni – Moshi**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Stendi ya Ngangamfumuni - Moshi Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa niaba yake Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Ngangamfumuni katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ulianza kutekelezwa mwaka 2019 kwa Mkataba wa shilingi bilioni 28.9 ambapo hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 7.5 zimetolewa na mradi umefikia 51% ya utekelezaji. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga bajeti ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa fedha za ujenzi wa stendi hii, kadri hati za malipo zitakavyokuwa zikiwasilishwa hadi mradi utakapokamilika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa kukwama kwa mradi huu kwa miaka mitatu nyuma siyo tatizo tena la fedha kwa sababu Wizara ilishakubali, tatizo kubwa ni Mkadarasi *CRJE* ambaye amekuwa na masharti magumu na ahadi za uongo kurudi *site* na kwa kuwa, tulienda mpaka Ofisi za TAMISEMI tukiwa na Mkurugenzi, Mstahiki Meya na Mwakilishi wa *RAS* tukafanya naye kikao na hajarudi; je, Serikali ipo tayari kutumia mbinu mbadala ili kumshinikiza arudi *site?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa sababu kile ni chanzo cha mapato na muda ambao umepita umeshakuwa mkubwa na fedha zikiwa zimeshatumika kiasi, Serikali ipo tayari sasa kuvunja mkataba kama atakataa sasa kurudi tena *site? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba Mkandarasi wa Ujenzi wa Stendi ya Ngangamfumuni aliacha *site* kwa kipindi cha takribani miaka miwili au mitatu kama Mheshimiwa Mbunge Tarimo alivyosema na kulikuwa na changamoto ya *management* ya mkataba kati ya Mkandarasi na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo, tumekubaliana na tumefanya vikao. Tulifanya kikao tarehe 01 Januari, 2025 na mwezi Februari tulifanya vikao pia kati ya Ofisi ya Rais - TAMIESMI, Wizara ya Fedha, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro kukubaliana na Mkandarasi arejee kwenye *site* aendelee kufanya kazi. Hivi sasa tupo hatua za mwisho za makubaliano kati ya Serikali na Mkandarasi ili kuhakikisha kwamba anarejea *site* na kuendelea na ujenzi wa stendi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea na *negotiations* hizo kuhakikisha kwamba mkandarasi anarejea. Kama itatokea hajakubaliana na mazungumzo yetu kati yetu na Serikali, basi Serikali itachukua hatua nyingine ikiwemo kuvunja mkataba kwa mujibu wa sheria na taratibu, ili tuhakikishe tunakwamua mkwamo wa Ujenzi wa Stendi ya Ngangamfumuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Monni Mohamed.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chemba ni Mji ambao unakua kwa kasi sana, lakini hauna stendi ya kisasa. Ninataka kujua, upi mpango wa Serikali wa kujenga stendi ya kisasa kwenye Mji wa Chemba? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ni moja ya halmashauri ambazo tayari tulishatoa maelekezo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuandaa andiko la kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa. Pia, tulielekeza kutafuta eneo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Monni kwamba, Serikali inatambua umuhimu na uhitaji wa stendi ya kisasa katika Halmashauri ya Chemba na tayari tulishatoa maelekezo kwa Halmashauri. Kinachofuata ni kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo kwa awamu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Halmashauri ya Kibondo imeshaandika Andiko la Mpango wa Kujenga Stendi ya Kisasa katika Jimbo la Muhambwe. Je, nini mpango wa Serikali

kuhakikisha wananchi wa Muhambwe wanapata stendi ya kisasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninawapongeza Halmashauri ya Kibondo kwa kuandika andiko la ombi la ujenzi wa stendi ya kisasa pia ninawahakikishia tu kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tunaendelea kuangalia uwezekano wa kupata fedha, kwa ajili ujenzi wa stendi za kimkakati katika Halmashauri zenye uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ni maelekezo ya Serikali kwamba halmashauri pia kupitia mapato yao ya ndani wahakikishie wanatenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hizi, kwa sababu stendi hizi ni mahitaji ya wananchi katika maeneo hayo na Halmashauri pia zinaendelea kukusanya fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali. Kwa hiyo, pamoja na Serikali Kuu na uandishi wa miradi ya kimkakati, lakini pia ni wajibu wa Halmashauri kuendelea kutenga fedha. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelipokea andiko hilo na tutatafuta fedha pia tutashirikiana na Halmashauri kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa awamu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, bado tuko Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Sasa nimwite Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, aulize swali lake.

Na. 169

**Ujenzi wa Stendi ya Kisasa Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Stendi ya Kisasa – Makete kupitia miradi ya kimkakati ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga na kuboresha stendi za mabasi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Makete inayo stendi yenye eneo la ukubwa ekari 3.1 katika eneo la Mabehewani. Stendi hii iliboreshwa na Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, ambapo kiasi cha shilingi milioni 40 kilitumika na stendi hii inatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Halmashauri ya Makete imetenga shilingi milioni 100 ili kuboresha miundombinu ya Stendi ya Mabehewani. Aidha, ili kuwa na stendi kubwa ya kisasa zaidi, Halmashauri ya Makete imetenga eneo la ekari 24.5 na sehemu ya eneo hilo itatengwa kwa ajili ua ujenzi wa stendi ya kisasa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa majibu ya Serikali, yanaleta matumaini na ni majibu ambayo wananchi wa Makete wanayo matumaini nayo, lakini nina swali moja kubwa la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza Mkuu wangu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi, Mkuu wangu Mheshimiwa Kissa Gwakisa Kasongwa na Mkurugenzi Jerry Mwaga kwa sababu wameanza kulifanyia kazi suala hili ambalo unalisema na kutenga shilingi milioni 100. Pili, ujenzi wa barabara kutoka Njombe kuelekea Makete na kutoka Makete kuelekea Mbeya ndiyo unaotufanya tuwe na uhitaji wa stendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja tu, ni upi mkakati wa Serikali kwamba, Halmashauri ya Makete mapato yake bado ni madogo yako chini na imetenga eneo la ekari 24.5 kwa ajili ya kujenga stendi ili barabara ikikamilika ikutane na stendi

imekamilika? Je, Serikali haiko tayari kutupatia fedha kwa mkopo au kwa namna nyingine ili halmashauri yetu iweze kujenga stendi hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba kuna ujenzi wa barabara ya lami ambayo tayari imekamilika, kutoka Njombe mpaka Makete, lakini kuna mpango wa Serikali kuendelea na ujenzi wa barabara kutoka Makete kwenda Mbeya, barabara hizi zitaongeza sana idadi ya magari yanayoingia katika Halmashauri ya Makete hivyo kulazimika kuwa na stendi kubwa na ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Sanga kwamba, Serikali hii inatambua uhitaji wa stendi katika Halmashauri ya Makete na ndiyo maana ilimwelekeza Mkurugenzi kutenga eneo na ameshatenga eneo la ekari 24.5. Ninakuhakikishia tu kwamba tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo kwa awamu, kwa kushirikiana na mapato ya ndani pia Serikali Kuu ili tuhakikishe kwamba huduma za usafiri zinaimarishwa zaidi katika Wilaya ya Makete. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba maswali mafupi kwa watakaopata nafasi. Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi katika Mji wa Mbulu kupitia Mradi wa *TACTIC*?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *TACTIC* unaendelea kutekelezwa katika miji 45 ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Tayari tuko awamu ya kwanza na ya pili na tunatarajia kuanza awamu ya tatu wakati wowote. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa

sababu stendi hiyo iko kwenye mpango wa *TACTIC*, tutahakikisha tunapoanza utekelezaji wa *tier* hiyo, tunaanza na ujenzi pia wa barabara pamoja na stendi ili Mji huo uwe na huduma nzuri zaidi za usafiri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Injinia Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwaka jana tarehe 6 Agosti, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi alifanya ziara katika Mkoa wa Kagera, Tarehe 07 akawa Biharamulo na ziara hiyo aliambatana na Waziri wa TAMISEMI ambaye aliwakilishwa na Naibu Waziri. Moja ya maombi ya watu wa Biharamulo ilikuwa ni ujenzi wa stendi ya kisasa na alitoa maelekezo ambapo majibu tuliyoyapata ni kwamba ilibidi andiko lirekebishwe liweze kurudishwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, andiko limerekebishwa na tayari liko Wizarani, TAMISEMI. Sasa, ni lini ujenzi wa stendi ya kisasa Wilayani Biharamulo utaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumepokea andiko la kimkakati la Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kwa ajili ya ujenzi wa stendi, na tunafahamu kuna uhitaji mkubwa wa stendi. Kama yalivyo maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama lakini ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunajenga stendi ya kisasa pale Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge *Engineer* Chiwelesa kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari tumepokea andiko hilo, tunafanya mawasiliano na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupata fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo, angalau kwa awamu, lakini tunahakikisha kwamba tutaanza utekelezaji mapema iwezekanavyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani swali langu limeshauliza na Mheshimiwa Rahhi.

**MWENYEKITI:** Basi swali limejibiwa. Mheshimiwa Mjika, Mheshimiwa Kabati una swali la msingi leo.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wilaya ya Meatu imeshaandaa eneo kwa ajili ya stendi mpya. Je, ni lini sasa Serikali itajenga stendi mpya katika Wilaya hiyo ya Meatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu uhitaji wa stendi ya mabasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, lakini kama ambavyo uko uhitaji katika halmashauri mbalimbali, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza kwa Waheshimiwa Wabunge wote na ninatoa msisitizo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote kote nchini ambao wana maeneo na uhitaji wa ujenzi wa stendi kwa ajili ya huduma za usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza waainishe maeneo ya ujenzi wa stendi hizo, lakini pili waanze kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hizo na wale ambao watakuwa hawana uwezo wa ujenzi wa stendi hizo walete maombi hayo kwa ajili ya ujenzi kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafuatilia hilo ombi na tuone namna ambavyo tutaanza ujenzi katika Halmashauri ya Meatu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Bado tupo Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Sasa nimwite Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, aulize swali lake.

Na. 170

**Upungufu wa Walimu wa Sayansi Shule ya Sekondari Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya upungufu wa Walimu wa Masomo ya Hesabu na *Physics* shule ya Sekondari Bukene?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake, Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejenga shule mpya ya Sekondari Mbale ambayo imesaidia kupunguza idadi ya wanafunzi katika shule ya Bukene kutoka 589 (wavulana 262 na wasichana 327) hadi 488, (wavulana 203 na wasichana 285), hivyo kupunguza tatizo la ikama ya walimu katika shule hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Bukene ina uhitaji wa Mwalimu mmoja wa Fizikia, waliopo ni watatu. Hisabati uhitaji ni mwalimu mmoja, waliopo ni watatu. Hivyo, shule hii haina upungufu wa walimu wa masomo ya fizikia na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendana na ongezeko la shule na idadi ya wanafunzi, Serikali itaendelea kuajiri walimu kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Zedi, swai la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali kadhaa ya sekondari ndani ya Jimbo la Bukene.

Karibu sekondari zote kwenye changamoto zao walitaja upungufu wa Walimu wa Fizikia na Hesabu kama ni changamoto kubwa sana. Nililichukua tatizo hilo na kuliwasilisha Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninaipongeza Wizara kwamba, kwa kipindi hiki kifupi cha tangu mwezi Oktoba, 2024 ninayo taarifa kwamba mwezi Machi, mwezi uliopita tumepata mgao wa walimu kupitia ajira mpya, walimu kama 74 wa masomo ya fizikia na hesabu na hivyo kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa fizikia na hesabu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kupokea pongezi kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Bukene kwa kumaliza tatizo la Walimu wa Fizikia na Hesabu kwa kipindi kifupi tu cha tangu mwezi Oktoba walipoleta changamoto hiyo, mpaka leo hii mgao wa mwezi uliopita umemaliza tatizo hilo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi pokea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea pongezi hizo, ni dhahiri Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inafanya jitihada zote kuhakikisha inaendelea kuimarisha Sekta ya Elimu, Elimu Msingi (shule ya awali, msingi na sekondari). Ndiyo maana katika kipindi cha uongozi wake wa miaka minne amefanya uwekezaji mkubwa wa zaidi ya shilingi trilioni 5.1 na hiyo kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea pongezi hizo na tunaona hii kazi kubwa ambayo inafanyika na Serikali ya Awamu ya Sita, itaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Hezya, Hasanga, Msiya, Kipunga na Kilimampimbi zina upungufu wa walimu wa fizikia na hesabu. Je, ni upi mkakati wa Serikali kutusaidia kutatua tatizo hili? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali imetoa kibali cha kuajiri walimu 15,925. Mpaka wakati huu walimu 13,105 tayari wameshapangiwa vituo vya kazi katika shule mbalimbali kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa walimu hawa ambao wataajiriwa katika kibali hiki cha walimu 15,925, wapo walimu wa masomo ya sayansi, ikiwemo fizikia na hisabati. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaweka kipaumbele kutazama ili tuweze kuleta walimu hao katika Jimbo lake, waweze kutoa elimu nzuri kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Changamoto ya upungufu wa Walimu haipo tu Bukene, ipo pia katika Wilaya yetu ya Karatu kwenye shule zetu za msingi na sekondari, hivyo wazazi wanachukua jukumu la kuchanga fedha hili kuwalipa walimu wale wa kujitolea. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba kupitia ajira hizi walimu wanaajiriwa wa kutosha na kuondoa upungufu uliopo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuhakikisha kwamba inaendelea kuboresha elimu ya msingi, kwa maana kuanzia shule za awali, madarasa ya awali, msingi na sekondari, inafanya jitihada kubwa sana ya kuongeza walimu kwa sababu udahili wa wanafunzi umeongezeka mara dufu kutokana na utekelezaji wa programu ya elimu bila malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua mahsusi ambazo zinachukuliwa na Serikali ni pamoja na kuajiri Walimu. Kama nilivyotangulia kusema, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetoa kibali cha kuajiri walimu 15,925. Miongoni mwa walimu hawa wapo walimu wa sayansi ambao watapangiwa vituo vya kazi katika shule mbalimbali kwenye Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Cecilia Paresso kwamba, ninafahamu uhitaji katika Wilaya ya Karatu, katika mgao wa walimu hawa, ninakuhakikishia kwamba Karatu watapatikana walimu wa masomo ya sayansi ikiwemo fizikia na hisabati, kwa ajili ya kuweza kuwafundisha watoto wetu na kuwapatia elimu iliyo bora. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Wakati tatizo hili likiisha katika Jimbo la Bukene, bado katika Jimbo la Kishapu kwa maana ya Wilaya ya Kishapu, Kata ya Lagana, Sekondari ya Kiloleli, Sekondari ya Bunambiyu, Sekondari ya Mwamalasa, Mwataga, zina upungufu mkubwa sana wa walimu wa masomo ya sayansi, hasa hisabati, fizikia, baiolojia. Ni lini sasa Serikali itakwenda kutatua tatizo hili ambalo ni kubwa sana katika taaluma, Wilayani kishapu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ajira za walimu, hizi 15,925 ambazo tayari kuna walimu wameshapangiwa vituo vya kazi, walimu 13,105, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutazingatia uhitaji wa walimu wa masomo haya ya sayansi ikiwemo fizikia, hisabati, pamoja na baiolojia kwenye Jimbo lake na tutaweza kuwapanga walimu hawa ili waweze kuja kuwafundisha watoto katika shule zetu, katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Ilemela ina uhitaji wa walimu wa sayansi 325, mpaka sasa tuna walimu 280 wakiwemo na hawa 80 ambao tumepata mgao wa juzi, lakini bado tuna upungufu wa walimu 85 wa sayansi. Je, ni lini sasa tutaongezewa walimu wa sayansi ili waweze kukidhi mahitaji katika shule zetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, kwamba Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetoa kibali cha kuajiri walimu 15,925, na mpaka wakati huu walimu 13,105 tayari wamepangiwa vituo vya kazi katika shule mbalimbali kwenye Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, kupitia ajira hizi mpya ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula kwamba, katika shule ambazo ziko kwenye Jimbo lake naye atapata mgao wa walimu hao, wakiwemo walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee vilevile, kutumia nafasi hii kusisitiza mamlaka zetu za Serikali za Mitaa na zenyewe kutumia njia kama kuajiri Walimu kwa mikataba kwa kutumia mapato ya ndani kwenye Halmashauri, pia kutumia walimu wanaojitolea. Kuna njia nyingi ambazo tunaweza tukazitumia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapata walimu wa kuwafundisha na tunaweza kupunguza ukali wa upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutatumia mikakati hii na katika Jimbo lake ataletewa walimu kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu iliyo bora. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, bado una swali moja. Sasa nimwite Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, aulize swali lake.

Na. 171

**Kuboresha Miundombinu Mji Mdogo wa Katoro**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya barabara katika Mji Mdogo wa Katoro ikiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini na kubaini kuwa zinahitajika zaidi ya shilingi bilioni 15 ili kuboresha miundombinu ya Mji wa Katoro, ikiwemo ujenzi wa lami kilometa 10, changarawe kilometa 20 na mitaro kilometa 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza uboreshaji wa miundombinu ya Mji huo kwa kujenga mitaro kilometa nane na ukarabati wa barabara kilometa nane kwa kiwango cha changarawe kupitia Mradi wa Dharura *(CERC)*, kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, wenye thamani ya shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mchakato wa ununuzi upo kwenye hatua za mwisho za kumpata mkandarasi atakayetekeleza kazi hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni nini mkakati wa Serikali katika uboreshaji wa miundombinu ya barabara kwenye Miji Midogo inayokua ya Nyarugusu, Bukoli, Nyakagwe, Chigunga, Nyakagomba, Rwamgasa, Jimboni Busanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Waziri yupo tayari kuambatana na mimi kwenda Jimboni Busanda kuona hali ya miundombinu ya barabara hii ninayoizungumzia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha kwamba inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara zetu hizi za Wilaya ambazo zina umuhimu mkubwa sana kiuchumi, lakini zinawawezesha wananchi kufikia huduma za muhimu za kijamii. Ndiyo maana dhamira hiyo utaiona katika ongezeko la bajeti ya *TARURA*. Mathalani utaona kwenye Wilaya hii, bajeti ya *TARURA* imeongezeka kutoka shilingi bilioni 1.9 mpaka sasa wanapokea shilingi bilioni 5.3 kila mwaka, kwa ajili ya kuhudumia barabara hizi za *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi katika Jimbo lake la Busanda ipo pale pale. Ndiyo maana utaona katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali imepanga kufanya matengenezo ya barabara kadhaa. Mathalani, Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 166 kwa ajili ya matengenezo ya kilometa 16 katika Barabara ya Nyamilamba – Nyakagwe, pia Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 148 kwa ajili ya matengenezo ya kilometa 16 za Barabara ya Bukoli – Nyamigogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imetenga shilingi milioni 248 kwa ajili ya matengenezo ya kilometa 23 kwenye maeneo ya Rwamgasa na Nyarugusu, vilevile Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 284 kwa ajili ya ukarabati wa kilometa 14 katika Barabara ya Buyagu – Nyarugusu. Ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kila mwaka wa bajeti inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu hii ya barabara hizi muhimu ili ziweze kuwanufaisha wananchi. Katika Jimbo la Busanda ninaomba Mheshimiwa Mbunge ninaomba ukae mkao wa kupokea kwa

sababu Serikali ya Awamu ya Sita inaleta maboresho makubwa sana katika miundombinu hii muhimu ya barabara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaboresha barabara za Mji wa Mbalizi kwa kiwango cha lami, ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano? Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Viongozi wetu Wakuu ni kipaumbele namba moja katika mipango na utekelezaji wa shughuli za Serikali. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali italeta fedha katika jimbo lake na katika eneo hili la Mbalizi, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, inafanya maboresho na ukarabati na ujenzi wa barabara muhimu kabisa, hizi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Suma Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Rungwe, Tukuyu Mjini, kuna Daraja la muhimu sana liitwalo Mafurasopo, daraja hilo ambalo lilibomoka linaunganisha Kata ya Buliaga na Kata ya Ibigi. TAMISEMI kwa kutambua umuhimu wa daraja hilo mlikuja kuangalia na mkasema mtatuma fedha mara moja, ili daraja hilo lijengwe. Sasa je, ni lini daraja hilo la Tukuyu Mjini la Mafurasopo litajengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, inachukua hatua za dharura kwenye maeneo ambayo mawasiliano yanakatika.

Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika eneo hili alilolitaja na nitumie pia, fursa hii kuzungumza na meneja wa *TARURA* wa ngazi ya mkoa na ngazi ya wilaya, waweze kushughulikia maandalizi yote, kwa ajili ya kuchukua hatua za dharura, kwa ajili ya kurudisha mawasiliano katika eneo hili muhimu, ili wananchi waweze kupata miundombinu iliyo bora na wasipate kikwazo cha kufanya shughuli zao za kijamii na za kiuchumi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Ipo Barabara, ya Moo, Kata ya Kimochi, Jimbo la Moshi Vijijini, ambayo inaanzia Barabara ya lami kuelekea *Forest* na *Keys Hotel*. Barabara hii ni muhimu kwa sababu, inapita watalii. Ni lini barabara hii itatengenezwa ili iweze kupitika kirahisi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Felista Njau kwamba, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Ndiyo maana utaona kila mwaka wa bajeti katika Serikali hii ya Awamu ya Sita bajeti ya *TARURA* imeongezeka mara dufu kutoka shilingi bilioni 275 kwa mwaka na mpaka sasa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, bajeti ya *TARURA* itaenda kuwa shilingi trilioni 1.18. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafika katika maeneo haya aliyoyataja, kwa ajili ya kuimarisha barabara na miundombinu hii, ambayo ina umuhimu mkubwa sana kiuchumi na kijamii pia, kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge bado mpo wengi, dhamira ya Serikali tumeshasikia kwenye maeneo yote kwenye masuala yote ya barabara. Kwa hiyo, kwa wale ambao sio lazima waulize, ninaomba waridhike na majibu yanayotolewa.

Nimemwona Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia, alipotembelea Mji wa Babati alitoa ahadi ya kilometa tano za lami na ninaomba nim-*quote* mwananchi, ambaye amekuwa akiulizia, Mheshimiwa Mbunge kumbushia Bungeni ahadi ya Mheshimiwa Rais ujenzi wa kilometa tano za lami hapa mjini; wananchi wanauliza ni lini ujenzi huo utaanza? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Viongozi Wakuu ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa mipango na majukumu ya Serikali. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Pauline Gekul kwamba, kilometa tano hizo za lami katika jimbo lake zitajengwa. Ninaomba akae katika mkao wa mapokeo, Serikali ya Awamu ya Sita itahakikisha kwamba, fedha zinapatikana, kwa ajili ya kuboresha miundombinu hiyo muhimu kabisa katika jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumeuliza maswali mengi kwenye eneo hili, ninaomba tuendelee. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako.

Tunakwenda Wizara ya Viwanda na Biashara. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 172

**Serikali Kutambua Biashara Mtandao**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, Serikali inatambua biashara ya mtandao na Makampuni mangapi yamejisajili na mapato kiasi gani yamepatikana kwenye biashara hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Exaud Kigahe.

**NAIBU WAZIRI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Serikali inatambua uwepo wa Biashara ya Mtandao. Kwa sasa kuna jumla ya kampuni 1,820 ambazo zimesajiliwa, ambapo kampuni 1,075 za Biashara Mtandao ni shughuli yao kuu na kampuni 745 Biashara Mtandao ni shughuli nyingine. Kwa sasa Serikali inaendelea kuchukua hatua muhimu za kuwa na mfumo madhubuti utakaosimamia biashara hiyo ambayo imeanza kuzaa matunda. Mfano, kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Serikali ilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 192.78 kutoka kwenye Biashara Mtandao, ambayo inajumuisha *betting* ya mitandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha tunaenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya teknolojia kwenye biashara, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Biashara Mtandao *(National Electronic Commerce Strategy)* ambao upo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji wake. Maeneo yatakayofanyiwa kazi katika utekelezaji wa mkakati huo ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA, uboreshaji wa Sera, Sheria na Kanuni na pia, uboreshaji wa huduma za mawasiliano, usafirishaji na uchukuzi; uimarishaji wa huduma za miamala kwa njia ya mtandao na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu biashara mtandao, ili waweze kutumia mitandao iliyopo kufanya biashara. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, ninaomba sasa niulize maswali yangu mawili. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani katika kuzuia udanganyifu na utapeli mkubwa unaofanywa katika biashara hizi za mitandaoni kwa sababu, kuna watu wengi sana wamelizwa, kwa ajili ya hii biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; je, Serikali inadhibiti vipi wanaouza bidhaa kwenye *social media* bila leseni kwa sababu, pia, kuna utapeli mkubwa sana unafanyika ili kuweza kukusanya mapato? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hilo swali la pili, sijui kama ni la Wizara hii. Ninadhani Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza ndio swali lako.

**NAIBU WAZIRI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa ufuatiliaji kwenye biashara na mahususi biashara mtandaoni. Ni kweli bado tuna changamoto nyingi na ndiyo maana nimesema Serikali imekuja na mkakati huo madhubuti na huu mkakati ni utekelezaji wa Sera ya Biashara ya Taifa ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2023, ambalo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Dkt. Selemani Saidi Jafo, alipitisha. Katika kutekeleza hilo tumeweka mkakati huu mahususi ambao umelenga kuboresha biashara mtandaoni kwa sababu, tumeona changamoto hiyo iliyopo katika biashara mtandaoni kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hiyo ni moja ya mkakati, lakini mikakati mingine ni Serikali kupitia Wizara mbalimbali, kwa mfano, Wizara ya Fedha tayari wana kitengo mahususi ambacho chenyewe kinasimamia biashara mtandaoni. Ndio maana utakuta rekodi zetu za mapato yameongezeka kwa sababu, tayari tuna-*track* kuhakikisha biashara zinazofanyika mtandaoni zinalipia kodi, lakini pia mapato ya Serikali hayapotei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tayari kuna sheria mbalimbali ambazo zote hizi zinalenga kudhibiti au kuboresha biashara mtandao. Kwa mfano, wana Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015, lakini pia, wana Sheria ya Miamala ya Kieletroniki ya mwaka 2015 na pia, kuna ile Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022. Yote haya yanalenga kuhakikisha tunapunguza au tunaboresha biashara mtandao ili iweze kuwa na manufaa kwa Watanzania, lakini pia kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili ni kweli kuna changamoto ya biashara ya kuuza bidhaa mtandaoni bila ya kuwa na kampuni. Kwa mfano, mtu anapiga picha bidhaa ya mtu kwenye duka halafu anarusha mtandaoni anatafuta wateja. Sasa mtu kama hujui, ameweka na namba ile ambayo bado ukituma hela mzigo hutapata, lakini pia na fedha yako itakuwa imetapeliwa. Sasa moja ya vitu ambavyo tumefanya, kama Serikali, tunawasaidia vijana, kwa mfano, sasa hivi tumewaambia kuna vijana wa Tanzania wamebuni mfumo mzuri ambao wenyewe unasaidia kuunganisha kati ya mteja kwa maana ya mnunuzi na mteja muuzaji kwamba, wameanzisha kampuni moja inaitwa *fortune technology company* na wana *App* moja inaitwa *Swift PAC,* ambayo yenyewe wanashirikiana na shirika la posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba ukinunua fedha zako zitakaa pale kwanza na ukithibitisha kwamba, umepata mzigo ndio wale wana-*release* ile fedha kumpelekea yule ambaye anauza. Kwa hiyo, hizi ni hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa na Serikali ili kuhakikisha tuna boresha biashara mtandao kwa sababu, hatuwezi kukwepa. Sasahivi biashara mtandao ndio kila kitu, lakini lazima tupunguze changamoto au athari hasi za biashara mtandao. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nimwite sasa Mheshimiwa Mtemvu, hayupo, lakini kwa niaba yake Mheshimiwa Mariam Kisangi

Na. 173

**Ujenzi wa Vituo vya Polisi Kibamba**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Mitaa ya Mpiji Magohe na Saranga katika Jimbo la Kibamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel Baran.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Saranga na Kata ya Mbezi, ambayo Mtaa wa Mpiji Magohe upo, hakuna maeneo yaliyotengwa, kwa ajili ya kujenga Vituo vya Polisi. Napenda kutumia fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, kutenga maeneo ili Serikali iweze kujenga Vituo vya Polisi vya Kata ya Saranga na Kata ya Mbezi, ambayo Mtaa wa Mpiji Magohe upo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam, kwa niaba, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, wananchi wa Tegeta A, Kata ya Goba, kwa kushirikiana na Mbunge wao, Mheshimiwa Issa Mtemvu, wameweza kujenga Kituo cha Polisi cha Tegeta A na kimefikia kiwango cha 80% ya ujenzi. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha wanakamilisha kituo hiki, ili wananchi waweze kupata huduma ya ulinzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, Serikali imeelekeza kwamba, kwa maeneo hayo hatuwezi kupata Vituo vya Polisi kwa sababu, hatuna maeneo. Ninataka kujua, je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuhakikisha kwamba, maeneo ambayo hayana Vituo vya Polisi wanawapelekea ulinzi wananchi wake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Mheshimiwa Sillo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kibamba, Mheshimiwa Issa Mtemvu, pamoja na Wananchi wa Tegeta A kwa kazi kubwa uliyoifanya ya

ujenzi wa Kituo cha Polisi ambacho kimefikia 80%. Nimhakikishie, Serikali imekuwa ikiunga mkono juhudi za wananchi na katika Kituo cha Tegeta A pia, Serikali itatafuta fedha na kuunga mkono umaliziaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili; ni kweli kuna baadhi ya maeneo bado hawajatenga maeneo, lakini nitoe wito kwa halmashauri zetu kutoa maeneo, kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Polisi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa maeneo ambayo hayana Vituo vya Polisi, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kulinda raia na mali zao kwa kutumia Vituo vya Polisi vya Jirani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge watakaopata nafasi ninaomba maswali mafupi, nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wilaya ya Tanganyika haina kituo cha Polisi. Mkuu wa Wilaya amefanya jitihada za kuanzisha wadau na kuwapa hadhi ya kuchangia, tumechangia. Ni lini Serikali itaweza kuunga juhudi za Mkuu wa Wilaya na ahadi iliyotolewa na Wizara, shilingi milioni 20 kuwa-*support;* ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Tumeanza na swali refu, ninaomba maswali mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mkuu wa Wilaya kwa hatua hiyo kubwa aliyoanzisha, kuanza kuchanga na kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kama imeshaahidi shilingi milioni 20 jua ni hela ndogo na nimhakikishie kwamba, tutatafuta fedha hizo na kuziwasilisha, ili wakamilishe Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Tanganyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Maswa ni Wilaya Kongwe ya kwanza kabisa katika Mkoa wa Simiyu, haina Kituo cha Polisi. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Maswa? Swali hili nimeuliza mara tatu, ni lini watajenga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga Vituo vya Polisi vya Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Wilaya hata na Kata. Nimhakikishie Mheshimiwa Esther kwamba, swali hili ameshauliza mara nyingi, kituo hiki cha Wilaya ya Maswa kimeshaingizwa kwenye mpango, kitatengewewa fedha na kuanza kujengwa, kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa Wilaya ya Maswa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Momba yenye majimbo mawili ya uchaguzi, Momba pamoja na Tunduma, Kituo cha Polisi chenye hadhi ya wilaya kimejengwa Tunduma, Wilaya ya Momba na Jimbo la Momba hakuna kituo cha Polisi, ambapo Mkuu wa Wilaya anaishi hapo na kuna *Police Post* tu. Je, ni lini mtatupatia pesa, ili tuweze kujenga Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya kwa kuwa, Mkuu wa Wilaya na vyombo vyake wanaishi hapo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo yote ambayo hakuna Kituo cha Polisi cha Wilaya, amesema kwenye wilaya nzima kuna Kituo kimoja cha Polisi cha Wilaya ila kwa eneo lake la Momba ndio hamna Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya, kwa sasa watumie hicho Kituo cha Polisi cha Kati ambacho kipo maeneo yale, wakati Serikali inajipanga kutafuta fedha, kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya, kwa eneo lake la Momba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ajali za moto zimekuwa zinajitokeza mara kwa mara katika Jimbo la Moshi Vijijini na Askari Zimamoto wamekuwa wanachelewa kufika kutokana na umbali na maeneo ya tukio. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha vituo vya zimamoto katika ngazi ya tarafa ili wananchi waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali, kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, imeendelea kujenga vituo vya zimamoto kwenye mikoa. Mheshimiwa Mbunge ametoa ushauri kwamba, sasa twende kwenye wilaya na tarafa kwa hiyo, ushauri wako umepokelewa pia, utafanyiwa kazi na Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Kalambo haina Jengo la Polisi, wanaazima Majengo ya CCM. Ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi, Wilaya ya Kalambo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026 tumeshatenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kalambo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kushirikiana na Askari tumejenga Kituo cha Polisi, Kata ya Kilando, na kimefikia hatua ya *lintel*. Nini *support* ya Serikali, ili angalau kuwaonesha wale Askari walioanza kujitoa, kuwatia moyo basi, kwa kile ambacho kimebakia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, ambaye leo anauliza kwa mara ya pili, kama sio ya tatu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwanza ninawapongeza sana Askari Polisi ambao wameamua kujenga Kituo cha Polisi, Kata ya Kalando. Nimhakikishie kwamba, Serikali itaunga mkono juhudi hizo nzuri, ili kukamilisha kituo hicho, kwa ajili ya kutoa huduma za wananchi na mali zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu iliahidiwa kujengewa Kituo cha Polisi katika mwaka

huu wa fedha ambao unakwisha, bado miezi miwili. Ni lini Kituo hicho cha Polisi kitajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Mhata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Serikali ipo palepale, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge. Serikali inatafuta fedha na ikipatikana tutaipeleka, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nanyumbu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Ludewa inakuwa sana kwa shughuli za kiuchumi na kijamii na kumekuwa na matukio ya moto, hasa kwenye mabweni. Nini mpango wa Serikali kuleta gari la zimamoto Ludewa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaagiza magari na imeshalipia magari 150 ya Zimamoto na Uokoaji kwa ajili ya kusambaza katika wilaya zote hapa nchini ikiwepo na Wilaya ya Ludewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Je, ni upi mpango wa Serikali wa kukarabati nyumba za polisi zilizopo Kata ya Kiusa,

Manispaa ya Moshi ambazo zinavuja sana? Swali hili nimeshaliuliza tena hapa Bungeni.

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bushiri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za askari wake wote hapa nchini pamoja na magereza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia kwamba eneo la Moshi ambalo amelisema tutaliweka kwenye mpango na kulitafutia fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba hizo ili askari wake katika maeneo salama waendelee kulinda raia na mali zao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel Sillo tunakushukuru sana kwa majibu yako. Bado una swali lingine moja. Nimwite Mheshimiwa Maulid Salehe Ali, Mbunge wa Welezo, aulize swali lake.

Na. 174

**Hitaji la Kituo cha Polisi Mtofani – Zanzibar**

**MHE. MAULID SALEHE ALI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Shehia ya Mtofani katika Jimbo la Welezo Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu wa kujenga Vituo vya Polisi daraja C Katika kila Kata na Shehia hapa nchini. Katika Shehia ya Mtofani Jimbo la Welezo Zanzibar hakuna eneo lililotengwa kwa ajili ya kujenga kituo cha Polisi. Ninaomba

nitoe wito kwa Halmashauri ya Manispaa ya Magharibi A kutenga eneo, ili Serikali iweze kujenga kituo cha Polisi katika Shehia ya Mtofani. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maulid Salehe Ali, swali la nyongeza.

**MHE. MAULID SALEHE ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaweka mkakati wa kuwa na *database* ya pamoja ya ukusanyaji wa taarifa na utunzaji wa kumbukumbu na upokeaji wa malalamiko ya wananchi kwenye vituo vya polisi nchini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Salehe Ali, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari ina mfumo thabiti kabisa wa kupokea na kutunza kumbukumbu au malalamiko ya wananchi. Hili kwa sasa limeanzia kwenye Ofisi za Mikoa yote kwa Makamanda wa Mikoa na Makao Makuu. Mpango ni kuhakikisha kwamba mfumo unaendelea kwenye wilaya na vituo vidogo vya chini. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Maryam Mwinyi.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Kijiji cha Pujini kuna kiwanja cha kujengea kituo cha polisi. Je, ni lini Serikali itajenga kituo hicho cha polisi kilichopo Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Maryam kwa ufuatiliaji wake. Nimhakikishie kwamba, kuwa eneo tayari wameshalitenga

Serikali pia itatenga fedha kwa ajili ya Kituo cha Polisi kule Chake Chake Pemba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdalla, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itakamilisha Kituo cha Polisi Jamii, Shehia ya Kendwa ambacho wananchi wenyewe wamekwishakamilisha hadi hatua ya linta? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Abdalla, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifuatilia sana na juzi nilikuwa naye Ofisini kwangu tumelizungumzia jambo hili. Nimhakikishie kama nilivyomwahidi, kwamba Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya umaliziaji wa kituo cha polisi ambacho kimejengwa na wananchi na nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Tarafa ya Daudi kama ilivyowekwa kwenye mpango wa bajeti mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kituo cha Polisi cha Daudi tupo kwenye mpango na tunatafuta fedha, zikishapatikana tutazipeleka kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho tayari kwa ajili ya

kuhudumia wananchi wa Tarafa ya Daudi pamoja na Wilaya ya Mbulu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itajenga Kituo cha Polisi Makao Makuu ya Halmashauri kwa kuwa tayari Mkurugenzi ameshatoa eneo na mimi Mbunge nimechangia tofali 5,000. Sasa nini *commitment* ya Naibu Waziri ya kuanza ujenzi huu haraka iwezekanavyo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na pia Halmashauri kwa kutenga eneo tayari kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya. Nimhakikishie, kwamba Serikali hii sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inayojali usalama wa raia na mali zao itatenge fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya kule Halmashauri ya Msalala. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Usonge Hamad, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Takribani zaidi ya miaka mitatu ninaulizia na ninakililia Kituo changu cha Polisi kilichopo Jimbo langu la Chaani, Lungalunga. Je, ni lini Serikali italeta ile shilingi milioni 80 waliyoahidi mwaka jana kwenye mwaka wa bajeti kwa ajili ya kukimalizia Kituo cha Polisi kilichopo Lungalunga?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Usonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali iliahidi kupeleka shilingi milioni 80 kwa ajili ya kumalizia kituo cha polisi alichokitaja, cha eneo la Chaani. Nimhakikishie kwamba mwaka wa fedha unaendelea tutahakikisha kwamba tunapata fedha kwa ajili ya kukamilisha kituo cha polisi ambacho kipo hatua nzuri. Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Maji. Nimwite sasa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, aulize swali lake.

Na. 175

**Muswada wa Chanzo cha Fedha Mfuko wa Maji**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta Muswada kuhakikisha Mfuko wa Taifa wa Maji unakuwa na chanzo cha uhakika cha fedha za Mfuko huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha uhakika cha fedha kwa Mfuko wa Taifa wa Maji kwa sasa ni tozo ya Shilingi 50 inayotokana na mauzo ya mafuta ya dizeli na petroli. Aidha, pamoja na kuwepo kwa chanzo hicho, Serikali imeendelea kubuni vyanzo vingine vya kutunisha Mfuko huo ikiwemo uwekezaji wa hati fungani na uandaaji wa maandiko ya miradi ili kupata fedha kutoka katika Mifuko ya Kimataifa ya kufadhili utekelezaji wa miradi ya maji, ambapo kiasi cha Dola za Marekani

milioni 17.35 zimepatikana kupitia Dirisha la Mabadiliko ya Tabianchi la Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutafuta vyanzo vingi zaidi kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa fedha kwa Mfuko wa Taifa wa Maji ili uweze kutimiza majukumu yake ipasavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Swali la kwanza; Mfuko huu unakusanya takriban shilingi bilioni 250 na zaidi, lakini Serikali imeweka ukomo wa bajeti kwenye Mfuko huu wa shilingi bilioni180. Sasa kutokana na matatizo mkubwa ya maji kwa nini, Serikali inaweka ukomo wa bajeti kwenye fedha zile ambazo ni fedha maalum kwa ajili ya Mfuko ule? Serikali inatafuta vyanzo vingine kuongeza fedha wakati fedha inazokusanya imeweka *cut off point* haizitumii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; mwaka jana katika Kata yangu ya Chali takribani watu 14 walifariki kwa ugonjwa wa kipindupindu kwa ukosefu wa maji. Upo mradi pale unaendelea Serikali imelipa mkandarasi lakini kazi ya kuendeleza hatua inayofuata haifanyiki Serikali ina mpango gani wa kukamilisha mradi huu wa maji katika Kata ya Chali ambao umechukua miaka mitatu sasa pila mafanikio?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na kumshukuru Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Bahi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa ufuatiliaji wa miradi ndani ya jimbo lake na vilevile kwa ushauri ambao ameendelea kutupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji tunatambua Mfuko wetu wa Maji ni mfuko ambao upo kwa mujibu wa sheria kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema. Vilevile tunatambua kwamba sisi Wizara ya Maji tumeendelea kushirikiana na wenzetu

Wizara ya Fedha; na kwa kweli tangu tumeenza kuongea nao tumeona mtiririko wa fedha umeendelea kuboreshwa zaidi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda zaidi ya hapo, Mfuko wa Maji umeingia *MOU* na *TRA* ili tuwe na uhakika kwamba kile kinachokusanywa ndicho ambacho kinakuja. Kwa kweli tumeona kwamba kuna *improvement* kubwa. Nimhakikishie tu pamoja na Bunge lako Tukufu, kwamba changamoto ambazo bado zipo katika namna ambayo *ceiling* inavyowekwa tupo katika mazungumzo na tupo katika hatua nzuri. Kwa hiyo hilo tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nikiri kabisa, kwamba Mradi wa Chali, Igongo Isanga pamoja na eneo la Makulu ni mradi ambao unagharimu shilingi bilioni 2.5. Ninatambua pia mkandarasi alikuwa anatudai *1.5* na Serikali imekwishamlipa. Sisi tumekwishaelekeza, kwamba mkandarasi asiporudi *site* na kuendelea na kazi *DG RUWASA* ahakikishe kwamba kwa kutumia wataalam wake wa kisheria aletwe katika meza na atuambie kwa nini harudi. Ikibainika kwamba hana nia njema na mradi ule basi Serikali itachukua hatua stahiki za kisheria ili ku-*terminate* kabisa ule mkataba na wengine wapatikane kwa ajili ya kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa kabisa kwamba Serikali inaendelea kuwekeza katika eneo la Bahi na tuna visima tunaendelea kuchimba katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge anatamani mradi ukamilike ili kuhakikisha kwamba tunaendelea *subsidize* maeneo ambayo bado yana changamoto kubwa ya maji. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea bado tupo Wizara ya Maji. Nimwite sasa Mheshimiwa Innocent Bilakwate, kwa niaba yake swali litaulizwa na Mheshimiwa Oliver Semuguruka. *(Makofi)*

Na. 176

**Kuanza kwa Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji – Kyerwa**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA K.n.y. MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, lini Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji wa Rutunguru, Kaisho - Isingiro utaanza ili kuondoa adha wanayoipata wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Maji Kaisho-Isingiro ambayo inahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa maji lita 225,000 pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 17. Lengo la mradi huo ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wapatao 37,500 waishio kwenye vijiji 11 vya Kaisho, Nyabishenge, Ibare, Ishaka, Karukwanzi A, Karukwanzi B, Kihanga, Kaitambuzi, Katera, Rutunguru pamoja na Nyakakoni. Utekelezaji wa awamu hiyo umefikia 95% na unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kutatafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi huo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Miradi ya Maji ya Runyinya, Chanya, Kikukuru, Kimuli, Rwanyango wakandarasi wameondoka *site* kwa sababu hamna *certificate*. Ningependa kujua, je, ni lini Serikali itawalipa ili waweze kukamilisha mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Mradi wa Maji Nyakanazi, Biharamulo umesimama kutokana na madai ya mkandarasi. Je, ni lini mkandarasi atalipwa pesa hiyo ili naye aweze kukamilisha mradi huo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Oliver Semuguruka pamoja na Mbunge wa eneo husika kwa kuendelea kuwapigania wananchi wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Nyakanazi, Biharamulo ni mradi ambao unatekelezwa na mkandarasi Bozz Bona ambapo chanzo tayari kilishajengwa, tenki limeshajengwa, na bomba zimeshalazwa. Hata hivyo, tunaelewa kwamba kuna sehemu chache na *DP* hazijakamilika. Tunatambua kwamba mkandarasi huyo anatudai na Serikali inayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili ni upande wa mradi wa Kikukuru mradi huu wenye gharama ya shilingi bilioni 5.1 ambao unatekelezwa na mkandarasi wa Tondwe umefikia 92%; kwenye upande wa chanzo alikuwepo mkandarasi mwingine anaitwa Serengeti ambaye ameomba ku-*withdraw* yeye mwenyewe ili asiendelee na mradi huo. Sasa Serikali imeanza utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunapata mkandarasi mwingine ili aweze kumalizia upande wa chanzo ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Vijiji vya Kitanula, Kalangali, Ipalalyu, Itagata na Mbugani katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi havina kabisa mtandao wa maji. Je, upi mkakati wa Serikali wa kupeleka maji katika vijiji hivyo ili kumtua ndoo mwanamke? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya kuwapambania Wanasingida.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika maeneo haya tumechimba visima vitano, lakini kuna visima vitatu bahati mbaya hatujafanikiwa kupata maji. Tunaendelea kufanya utafiti ili tuweze kuona tunatatua changamoto hii kwa namna ambayo itafaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vijiji ambavyo havina maji vihakikishe kwamba tunawapelekea miradi ya maji, ukiwemo Mradi mkubwa wa Miji 28 ambao unagharimu shilingi bilioni 17. Kwa sababu lile tenki limejengwa mpakani kati ya Manyoni Mashariki na Manyoni Magharibi, yaani Itigi. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba tutakapokuwa tumejiridhisha kuwa hatujapata chanzo kingine basi tenki hilo litasaidie kupeleka upande wa Itigi na kutatua changamoto ya maji katika maeneo haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa muda wetu umekwenda maswali bado tunayo mengi. Kwa hiyo, ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Tunaendelea Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nimwite sasa Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, aulize swali lake.

Na. 177

**Kufuta Hati ya Shamba la Balali**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafuta Hati ya Shamba la Balali na kuwakabidhi wananchi wa Melela?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, atajibu swali hilo Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro wa Shamba la Balali kwa muda mrefu ulikuwa ukishughulikiwa na Serikali ili kuweza kuutatua kiutawala. Hata hivyo, wananchi waliokuwa wanalalamikia shamba hili waliamua kutumia njia ya Mahakama kwa kufungua shauri Mahakama Kuu. Baada ya Mahakama kusikiliza hoja za wananchi hao pamoja na mmiliki wa shamba iliamua kuwa shamba tajwa ni mali ya familia ya Balali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu ulishughulikiwa na Mahakama Kuu Mkoa wa Morogoro kupitia Shauri la Ardhi Na.5 la mwaka 2023. Natoa rai kwa wananchi kuheshimu uamuzi uliotolewa na Mhimili wa Mahakama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; mgogoro huu wa Shamba la Balali unafanana kabisa na mgogoro wa Shamba la Kambenga. Je, Serikali ina mpango gani katika kuutatua mgogoro wa Kambenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana jioni nimepokea wananchi kutoka Kijiji cha Utengule wakiambatana na Mwenyekiti wao wa Kijiji kuna mgogoro baina ya Kitalu cha uwindaji na wananchi wa Kijiji cha Utengule. Je, yupo tayari mara tu baada ya kipindi hiki cha Bunge nimkutanishe na hao wananchi niliowapokea jana?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana naye kwamba mara baada ya kipindi hiki cha maswali tukutane ili kuweze kujadili mambo yote haya mawili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya. Nimwite sasa Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 178

**Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Kitete Tabora**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete Tabora?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Kitete unatekelezwa kwa awamu ambapo hadi sasa Serikali imetoa fedha shilingi bilioni 3.27 ambapo awamu ya kwanza zilitolewa shilingi bilioni 2.69 na awamu ya pili shilingi milioni 578.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora, Kitete

ambapo hadi sasa ujenzi umefikia 50%. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Februari, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, Mkoa wa Tabora ni mkoa wa tatu kwa wingi wa watu kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022. Kipaumbele cha Mheshimiwa Rais katika masuala ya afya ni afya ya mama na kupunguza vifo vya mama mjamzito na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; mpaka leo Tabora Hospitali ya Mkoa tunaambiwa inajengwa kwa awamu kuanzia mwaka 2020 mpaka sasa jengo lile bado halijakamilika. Serikali ituambie ile ni Hospitali ya Mkoa ama ni kitu gani? Kwa sababu mpaka leo hakuna uwezekano wa kumalizika kwa jengo lile, bado bilioni mbili zinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; pamoja na changamoto ya majengo likiwemo na jengo hilo la mama na mtoto na ndiyo maana nikashauri hospitali ile iwekwe iwe ya Wilaya na Hospitali ya Mkoa ijengwe nyingine. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaboresha huduma za afya za Mkoa wa Tabora, kwa sababu ni mkoa ambao una watu wengi na wanahitaji huduma za afya badala ya kuwapa rufaa kila siku kwenda Bugando na kuja Hospitali ya Benjamini wakati pale tunaambiwa tuna Hospitali ya Mkoa? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa hamasa aliyokuwa nayo nzuri ya kuhakikisha Hospitali yao ya Mkoa ya Tabora inafanyiwa kazi vizuri. Niseme tu kwa kweli anafanya kazi vizuri sana

Mheshimiwa Mbunge akishirikiana na Mheshimiwa Mwakasaka kwa ajili ya kutetea hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe Mheshimiwa Mbunge wasiwasi, kwanza alimwona jana Waziri wa Afya, alikwenda kwenye hospitali hiyo na alikwenda kwa msisitizo wa kuhakikisha kwamba hospitali hiyo sasa haya anayoyasema yanaenda kutatuliwa mara moja kabla ya kufika Februari, 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe tu wasiwasi, leo fedha ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiingiza kwenye Sekta ya Afya ni nyingi sana kiasi kwamba sio tu zimetatua matatizo ya afya kwa Tanzania yetu, imebubujika imekwenda mpaka kwenye mataifa yanayotuzunguka, ndiyo maana unasikia leo watu wanatoka nchi mbalimbali wanakuja kutibiwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi, tunaanza moja moja, bora wao waliokuwa na hospitali hiyo ya mkoa ya zamani, wenzao walikuwa hawana hospitali ya mkoa kabisa na leo wanayo. Sasa usiogope, kila kitu ambacho mnataka kwenye Mkoa wa Tabora, kwenye eneo la afya Mheshimiwa Rais wetu ameshajipanga kwa ajili ya kuhakikisha hayo mambo yanatekelezeka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Bado kuna upungufu mkubwa wa madaktari katika Hospitali yetu ya Kitete na Serikali ilikuwa imetuahidi itatuongezea Madaktari, mpaka sasa hivi imeshatuongezea madaktari wangapi bigwa ambao tulikuwa na upungufu nao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ushahidi unaoonesha jinsi ambavyo Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mwakasaka wanashirikiana kwa pamoja

kuhakikisha Hospitali ya Kitete inakuwa imekaa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme tu, Mheshimiwa Mwakasaka jana alimwona Mheshimiwa Waziri amekwenda pale na anakumbuka siyo muda mrefu mimi na yeye tulishirikiana tukaenda kwenye hospitali yenu na hili ni kwa sababu kumekuwa kunapelekwa wataalam mbalimbali kwenye hospitali yetu. Toka niende pale mpaka sasa sina namba kamili, lakini baada ya hapa tuje tukae na yeye ili tuweze kuangalia namba kamili nimwambie, nisije nikamwambia namba isiyo sahihi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maliasili na Utalii, nimwite Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini aulize swali lake.

Na. 179

**Vivutio vya Utalii Kilwa kuwa na Tija kwa Taifa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvifanya vivutio vya Mapango ya Nang'oma, Namaingo, Likolongomba na Nampombo kuwa na tija kwa Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imeanza kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha vivutio vya Mapango ya Nang'oma, Namaingo, Likolongomba na Nampombo vinakuwa na tija katika uchumi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hiyo ni pamoja na kuanzisha Adhimisho la Kumbukizi ya Vita ya Majimaji ambalo

hufanyika Mwezi Agosti kila mwaka katika Wilaya ya Kilwa kwa lengo la kutangaza vivutio mbalimbali vya kilwa ikiwemo mapango hayo kwa wadau wa utalii, washiriki, waandishi wa habari na wananchi wanaotembelea katika tukio hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya Wizara ni kuwa jitihada zinazoendelea zitaongeza idadi ya watalii na wageni wanaotembelea maeneo hayo. Hivyo, Wizara inatoa rai kwa wadau wa sekta ya utalii kuchangamkia fursa ya uwekezaji kwenye shughuli na huduma za utalii katika maeneo haya. Lengo ni kuhakikisha kuwa sekta ya utalii inaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa wananchi wa Kilwa na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Awali ya yote nipende kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza kiasi kikubwa chenye tija katika sekta yetu ya utalii. Ikiwemo kutoa GN ya Kumbukumbuzi ya Vita vya Majimaji kwa Mnara wa Majimaji pale Nandete kupitia *GN* namba 166 na *GN* namba 163 ambayo inatambua hayo mapango mawili yaliyoelezwa kwenye …

**MWENYEKITI:** Swali lako.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata pia boti ambayo imeongeza watalii mara dufu kule Ukanda wa Pwani wa Kilwa. Swali langu la kwanza; ni mwaka 2024 wakati wa maadhimisho ya vita vya majimaji Serikali iliahidi kwamba itajenga jengo la makumbusho pale Nandete na kujenga ngazi za kushukia katika Pango la Nang’oma. Je, mkakati huu umefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni kwamba, bado kuna maeneo mbalimbali ya vivutio vya majimaji hayajaendelezwa na kupatiwa *GN*. Kwa mfano kule alipokuwa anaishi Jemedari

Kinjekitile Ngwale ambaye alikuwa ni mwanafalsafa na mhamasishaji wa vita ile, lakini pia kuna baadhi ya mapango bado hayajapata *GN*. Je, ni lini Serikali itatoa *GN* kwa hivyo vivutio vilivyobaki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wizara iliahidi kufanya ujenzi katika eneo lile kwa kuweka kituo cha utalii, lakini kujenga njia za kwenda kwenye mapango. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari Wizara imejipanga kwa ajili ya kukamilisha jambo hilo, tumekwishatenga bajeti ya kutekeleza miradi hiyo, kazi inayoendelea sasa ni kukamilisha michoro ya majengo hayo ili kazi iweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili kuhusiana na *GN* kwenye yale mapango mawili yaliyobakia, lakini vilevile kwenye makazi ambayo Kinjekitile alikuwa akiishi. Ninataka nimhakikishie kwamba sasa hivi zipo kazi za kukusanya takwimu na taarifa za kiuhifadhi na kiutalii za maeneo hayo, kazi hii ikikamilika tunaamini kwamba ikifika mwaka 2026, tangazo hili la maeneo haya litakuwa limetoka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nifahamu, Serikali imefikia hatua ipi kulipa fidia wakazi wa Kijiji cha Ndolezi kwa ajili ya kupisha uhifadhi wa kimondo katika Wilaya ya Mbozi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na taratibu za uhakiki wa jambo hili na mara baada ya kazi hiyo ikikamilika wananchi wale watapewa fidia yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu yako.

Waheshimiwa tunaendelea, muda wetu umetutupa mkono, Wizara ya Uchukuzi. Nimwite sasa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, aulize swali lake.

Na. 180

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Omukajunguti – Kagera**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege Omukajunguti utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua changamoto za usalama wa Ndege na abiria katika Mkoa wa Kagera, Serikali imeanza utekelezaji wa mpango wa kudumu unaohusisha mjenzi wa kiwanja kipya kitakachokuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa ambapo mnamo mwezi Januari, 2025, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi iliteua timu ya wataalam kwa lengo la kufanya tathmini ya uchaguzi wa eneo la ujenzi wa kiwanja kipya kikubwa cha Ndege ya Daraja 4C ambacho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa za abiria zinazoweza kubeba hadi abiria 220 kwa wakati mmoja. Pamoja na majukumu mengine, lengo la Kamati hiyo lilikuwa ni kufanya tathmini na kushauri eneo linalofaa kwa ujenzi wa kiwanja hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya eneo pendekezwa ambalo ni eneo la Kihabajwa lililopo eneo la Wilaya ya Misenyi

imeridhiwa na Serikali na kwa sasa inaendelea na taratibu za utoaji ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya, tayari imeanza kushauriana na Serikali ya Mkoa, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Baada ya zoezi la utoaji ardhi kukamilika taratibu za ujenzi zitaanza mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru sana na kuipongeza Serikali kwa kuwa juhudi za kujenga uwanja wa ndege ndani ya Wilaya ya Misenyi ambayo ulikuwa ni wa Omukajunguti ni za muda mrefu, lakini Serikali kama inavyosema kupitia Kamati maalumu iliweza kubaini eneo lingine ambalo ni karibu na eneo la awali la Omukajunguti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; wananchi ambao walikuwa katika maeneo ya Omukajunguti walisimamishwa kufanya shughuli za uendelezaji na za kiuchumi katika maeneo yao kwa muda mrefu na kimsingi walikuwa wameshafanyiwa na tathmini kulipwa fidia kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege. Sasa, ni nini tamko la Serikali kwa wananchi hao kuhusiana na maeneo yao ili waweze kuyaendeleza katika shughuli zao za kiuchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa eneo la Kihabajwa linakaribiana na maeneo yanayomilikiwa na wananchi lakini mengine yanamilikiwa na Serikali zetu za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini mkakati wa Wizara yetu ya Uchukuzi kushirikiana na Wizara ya Ardhi na uongozi wa Mkoa na Wilaya ya Misenyi kuhakikisha kwamba tunafanya mipango miji vizuri kupima maeneo hayo, ili kuweza kuwa na maeneo ambayo yamepimwa ili kuleta kivutio pindi uwanja wa ndege utakapojengwa na maeneo ambayo yanazunguka uwanja huo yawe na yenyewe yana hadhi kama uwanja huu utakavyojengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, kwa maelezo yake mazuri aliyoyatoa ya kuipongeza Serikali yetu kwa jitihada ambazo tunazifanya, lakini ninampongeza kwa sababu ya uhamasishaji mkubwa ambao amekwishaanza kuufanya ikiwa ni pamoja na kuwaanda wananchi juu ya mradi mkubwa wa kiwanja cha ndege utakaojengwa katika eneo la Kihabajwa ambao haujawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye baada ya kuona umuhimu wa mkoa huo kiuchumi pamoja na sekta nyingine akaelekeza Wizara yetu kwamba, uwanja mnaotaka kuendelea kuuboresha hapana, ninataka ujengwe uwanja mkubwa utakaoendana na mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lake la kwanza alilouliza, je wananchi wanaruhusiwa kuendeleza maeneo yao? Jibu ni ndiyo, kwa kuwa tayari tumeshakubaliana kwamba tutakwenda kujenga Kiwanja cha Ndege cha Kihabajwa, maana yake hili eneo la awali halitatumika tena kwa ajili ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lake la pili anauliza mpango wa Serikali. Ninapenda kumhakikishia na bahati nzuri nami nimekwenda eneo hilo nilikuwa na yeye mwenyewe na anafahamu kidogo. Sema hapa ninataka nchi nzima iweze kufahamu, tayari Serikali yetu kupitia Wizara ya Uchukuzi, ikishirikiana na Ofisi ya Mkoa kupitia Mamlaka yetu ya Viwanja vya Ndege, imekwishawasiliana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kuanza mpango wa upimaji ili kuweza kuboresha eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni nini? Moja, ni kuhakikisha kwamba maeneo jirani na uwanja wa ndege yanakuwa na mandhari mazuri; lakini pili, kuvutia uwekezaji. Wote tunafahamu uwanja huu hautaishia kunufaisha watu wa Kagera tu, hata nchi jirani zitakwenda kuutumia uwanja huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ni lini ujenzi wa uwanja wa ndege wa Musoma utakamilika kwa maana ya *run way* pamoja na jengo la abiria ili kuweza kuanza kutumika na kukuza uchumi wa Mara kupitia utalii, biashara, pamoja na kurahisisha usafiri na usafirishaji? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Matiko kwa sababu anavyokimbizana kufuatilia uwanja wa ndege wa Musoma, siyo muda mrefu atamkaribia mpaka Mbunge wa Jimbo la pale mjini jinsi anavyohangaikia usiku na mchana kuona kwamba uwanja huu unakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie, kutokana na umuhimu mkubwa wa utalii, madini na maeneo mengine, Serikali iliamua kufanya maboresho ya uwanja wa Musoma na hivi ninavyozungumza umevuka asilimia 58 na mjenzi yupo *site* anaendelea na kazi baada ya kusimama kwa muda mrefu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninamwomba aendelee kuwa na subira, Serikali ambayo imekwishaanza kujenga inakwenda kukamilisha uwanja huo wa Musoma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa Manyara *Airport* ili kuongeza utalii katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Manyara *National Park?*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Awack kama alivyoliuliza. Anaulizia kuhusu uwanja wa ndege, ninafikiri anaongelea wa mkoa maana pale kuna viwanja viwili. Kama anazungumzia wa mkoa, tupo kwenye hatua za utoaji wa ardhi, tutakapozikamilisha Serikali itaanza kufanya taratibu za ujenzi. Kama anazungumzia ule wa utalii kwa maana ule wa *Lake Manyara,* tayari tumeshampata mkandarasi, tupo kwenye hatua za *mobilization* na ujenzi utaanza mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza ninachukua nafasi hii kuipongeza Serikali pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri. Nauliza Serikali, imewalipa wananchi 226 kati ya wananchi 1,800. Je, Serikali ina mpango gani kuwamalizia hawa wengine maana wapo kwenye hali mbaya na kuna mvua kubwa zinazonyesha? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajibu kwa kifupi lakini moyo usio na shukrani hukausha mema yote. Ninampongeza Mheshimiwa Bonnah kwa kuweza kufuatilia na kupongeza Serikali hii kwa sababu jambo hili lilikwama kuanzia miaka ya 1990 ambapo wananchi zaidi ya 1,528 walikuwa wanadai. Tumekwishalipa shilingi bilioni 20 na siyo muda mrefu tutakwenda kulipa tena. Hii ni jitihada za Mheshimiwa Rais wetu na ninaamini kwa kuwa wameshaanza kulipa na hata waliobakia hao atakwenda kukamilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Enosy Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya ujenzi wa uwanja wa ndege Mkoa wa Njombe na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja kwenye *cave* akaona lile eneo. Wananchi wetu wa Makambako, Njombe Mjini, Lupembe, kuna wafanyabiashara wengi sana, hata Mwenyekiti Mheshimiwa Deo Mwanyika ili

apande ndege mpaka aende Mkoa wa Songwe au aje Mkoa wa Iringa, ni lini uwanja wa ndege Mkoa wa Njombe atajengwa sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu na ujibu vizuri Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri utaniambia nijibu kwa ufupi, lakini naona hujazungumzia hilo. Wewe na Mheshimiwa Swalle pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Njombe, mmelifuatilia jambo hili kwa ukaribu sana na Serikali inatambua umuhimu wa uwanja wa ndege wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali tulikuwa na mpango kwa ajili ya kukarabati ule uliopo, lakini baada ya kuona eneo ni dogo na mipango ni mikubwa, Serikali ikaona ni lazima ibadilishe uwanja ijenge uwanja mkubwa pengine wenye hadhi sawa na uwanja wa Songwe. Hii kwa sababu gani? Kwa sababu, kwanza unaweza kuona Mkoa wa Njombe ndiyo una maghala makubwa ya chakula ya *NFRA*. Mbili, tunao Mradi wa Liganga na Mchuchuma ambao tukikamilisha ujenzi wa reli ya kusini, uwanja ule ndiyo utakuwa jirani kwa ajili ya kufikisha watu mbalimbali kwenye eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uwanja huo pia utakuwa na faida kubwa kwa kilimo cha parachichi pamoja na mazao mbalimbali, lakini pia yapo maeneo jirani ikiwa ni pamoja na Chimala ambapo pia kuna madini mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa uwanja huu, nimesema wiki iliyopita ninaomba nirejee tena, tumeshampata mkandarasi anaitwa *Intercontinental Technocrats* ambaye anafanya uhuwishaji, upembuzi yakinifu ili kuweza kujua gharama na mahitaji ya uwanja huo yatakuwaje. Hatimaye tukishamaliza hatua hiyo tutatangaza na tutampata mjenzi ajenge uwanja kama ambavyo yeye mwenyewe amekuwa akihitaji kwa muda mrefu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu hayo na tunakuomba basi jambo hili lipate kutimia.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha kabisa, ninaomba tuendelee na swali letu la mwisho, Wizara ya Kilimo. Nimwite sasa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, aulize swali lake.

Na. 181

**Ushindani wa Ununuzi wa Zao la Pamba Nchini**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani na madhubuti kuhakikisha kunakuwa na ushindani kwa wafanyabiashara katika ununuzi wa pamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa David Silinde, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa pamba nchini hufanyika kwa utaratibu wa soko huru ambapo zaidi ya kampuni 35 zimesajiliwa na kupewa leseni ya kununua pamba na usajili unaendelea ili kuongeza ushindani. Kampuni hizi hununua pamba kulingana na hali ya soko ya msimu husika na bei dira iliyokubaliwa na wadau. Aidha, Serikali husimamia na kuhakikisha bei dira iliyokubalika na wadau inazingatiwa katika ununuzi wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utaratibu huo, Bodi ya Pamba imeingia mikataba na Kampuni za ununuzi wa pamba ambao wameajiri Maafisa Ugani wanaotoa huduma za ugani katika kata zinazozalisha pamba kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo. Kampuni hizo zinapewa leseni ya kununua pamba katika kata zilizoajiri Maafisa Ugani kulingana na bei dira inayokubaliwa na wadau kwa msimu husika kulingana na bei ya soko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mfumo wa sasa wa *AMCOS* kupokea fedha kutoka kwenye kampuni, ndipo *AMCOS* inunue pamba kwa niaba ya hizo kampuni hauruhusu kabisa ushindani na kwa kuwa Wizara mlifanya utafiti kidogo mkaona huo utaratibu una kasoro; ni kwa nini Serikali isiruhusu Mfumo wa "*Simiyu Model*" wa kuwaruhusu wanunuzi ama kampuni za pamba kuwa kila mmoja na mlango wake wa kununulia pamba ili kuruhusu huu ushindani wa kweli na halisia? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi kwani amekuwa ni mdau mkubwa katika zao la pamba na amekuwa akilifuatilia kwa ukaribu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho nimthibitishie, hili alilolizungumzia yeye kama Mbunge tumeshalipokea katika ofisi yetu na kesho tarehe 30 Aprili, tutakuwa na Mkutano mkubwa wa Wadau pale Shinyanga ambapo katika moja ya jambo litakalojadiliwa ni pamoja na haya mapungufu ambayo ameyaeleza na namna bora ya kutumia Mfumo wa "*Simiyu Model*" katika ununuzi wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tarehe 30 (kesho) tutaweka utaratibu mzuri ambao ninaamini utakuwa na faida kwa wadau wote wa Sekta ya Pamba. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge hili tumelizingatia na kesho tutapata majibu yake ya mwisho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali umeisha na tumeongeza kidogo. Kwa hiyo kwa ambao hawakupata nafasi, kesho nayo ni siku.

Waheshimiwa ninaleta majina ya wageni waliopo ndani ya ukumbi wetu siku ya leo na tunaanza wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Tuna wageni 10 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na Waziri wetu Mkuu, ambao ni Viongozi, Watendaji, Mwenyekiti, na Katibu wa CCM Mkoa na Wilaya kama ifuatavyo:-

Tunaye Brigedia Jenerali Mstaafu Aloyce Mwanjile, huyu ni Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho; tunaye Ndugu Barnabas Essau, huyu ni Katibu wa CCM Mkoa wa Lindi; Ndugu Ibrahim Ndolo, huyu ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ruangwa; Ndugu Mussa Mkoyage; Mheshimiwa Mariam Kasembe, huyu alikuwa Mbunge mwenzetu hapa kutoka Masasi, Bunge la Kumi mwaka 2010, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia, Ndugu Antonia Shayo; Mheshimiwa Abdallah Ngokwe; Mheshimiwa Faith Mitambo, huyu naye alikuwa ni Mbunge wa Bunge la Kumi mwaka 2010; Ndugu Mussa Manjaule; na mwisho katika hili kundi ni Ndugu Ally Mkigijagi. Ahsanteni na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati ambao ni Wakuu wa Wilaya; Ndugu Mwanahamisi Munkunda ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mwanga na Ndugu Onesmo Buswelu ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Hawa ni Watendaji wa Kampuni ya *ARA Petroleum* ya Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo Ndugu Erhan Saygi, wako hapa wamekaa sehemu mbalimbali, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wengine 22 wa Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Mheshimiwa David Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi. Hawa ni wageni wao kwa

pamoja ambao ni Asasi ya Vijana wa Umoja wa Mataifa *(YUNA) 2000'S APEADU*. Tuwaone, karibuni sana, sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Hawa ni viongozi wa *SMAUJATA* (Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania) kutoka Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 39 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo. Hawa ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Oltepes Kilimo kutoka Mkoa wa Arusha, wako pale, karibuni sana kwa mafunzo. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa George Mwenisongole. Huyu ni Ndugu Anna Msumemo, Mtangazaji wa *Radio Dream FM* kutoka Mkoani Mbeya, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni 14 wa Mheshimiwa Yahya Ally Mhata. Hawa ni Makatibu wa Chama cha Ushirika cha Kilimo cha Masoko *(AMCOS)* kutoka Nanyumbu, Mkoani Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 45 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu (Mbunge). Hawa ni wanafunzi na Walimu wa Shule ya Sekondari Moivo, Arumeru Magharibu Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula. Hawa ni marafiki zake kutoka Nyamagana Mkoani Mwanza, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 40 wa Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa. Hawa ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Waheshimiwa Madiwani; Wakuu wa Divisheni na Vitengo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo Mkoa wa Kagera, wako pale, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni wanafunzi 91 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari

*Don Bosco Seminary*, kutoka Mkoa wa Iringa Wilaya ya Mafinga, wako pale. Karibuni sana kwa mafunzo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Haya ndiyo majina niliyonayo kwa sasa.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yaliyo mbele yetu ya kupitisha Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Nina orodha ya wachangiaji wengi hapa lakini tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa fursa hii. Ninaomba nianze kwa kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wengine wa Bunge kwa namna mnavyoendesha Bunge hili. Niwatakie kila la kheri kwenye uchaguzi unaokuja ili wapigakura wenu wawarudishe hapa kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba katika kuchangia Wizara hii, kwanza ni lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amewezesha Wizara hii ya Nishati inayoongozwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kuiwezesha kutekeleza mambo makubwa sana katika hii nchi ndani ya kipindi kifupi cha miaka minne. Ninataka niseme kwamba kuna mengi ambayo tumeyaona pamoja na kukamilisha ile miradi migumu sana kama ule wa Bwawa la Nyerere kwa wakati tulioutarajia na kuweza

kufanya hii nchi ijitosheleze kwa uzalishaji wa nishati angalau kwa kipindi hiki ambacho tumefikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba tuna ziada sasa ya umeme na ni kitu ambacho watu wengi hawakutarajia kwamba tutafikia hapo. Pia, ninashukuru kwamba hiyo ziada Wizara hii imeendelea sasa kuunganisha gridi yetu kwenye *Power Pool* ya Afrika Mahariki pamoja na *SADC, which means* kwamba pengine hata sisi tunauza umeme kwa nchi fulani ambayo hatujaweza kuambiwa, lakini ninaamini ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba pengine tumshukuru sana na tumpongeze sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuzindua Benki ya Ushirika jana. Hilo ni jambo kubwa sana ambalo ninaamini watu wengi hawajaelewa kilichofanyika, lakini sisi tuliokuwa tunafuatilia ni Taasisi au ni Benki ambayo imechukua muda mwingi sana na kazi kubwa sana ya Mheshimiwa Rais mwenyewe pamoja na Waziri wa Kilimo na wale wengine wanaohusika kuweza kuanzisha hiyo Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mambo ya Benki hapa kwa sababu ninaunga mkono hoja ya kwamba kwa gharama kubwa za uunganishaji wa umeme kwenye yale maeneo ya miji na miji midogo, ninaamini sasa *TANESCO* inaweza kwenda kutafuta fedha ya mikopo ili waweze kugharamia hizo gharama za kuunganisha wananchi kwenye umeme na halafu wakalipa ule mkopo kwa kutumia kuongeza ile gharama ya *invoice* ya umeme. Ninaamini ni vigumu sana kwa wananchi wengi kujiunga kwa shilingi 350,000 na zaidi kwa maeneo mengine kwenye umeme bila kupewa nafasi ya kulipa kidogo kidogo kwa hiyo gharama ya kujiunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, nimpongeze pia Naibu wake pamoja na Watendaji wake kwenye hizi taasisi. Mheshimiwa Waziri ana taasisi nyingi na Watendaji wake wote wanaonekana ni Watendaji waadilifu, ni Watendaji ambao wana-*deliver* (wanafanya ili waone matokeo chanya). Ninasema

kwamba hawa watu ninaamini kazi na utu vinaendelea na ninaamini kwamba wataendelea kusonga mbele kwa namna hiyo na kwa *slogan* hiyo ya "Kazi na Utu, Tunasonga Mbele."

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa taarifa Mheshimiwa Mzee wangu Kimei kwa kupongeza. Ninampa taarifa kwa sababu tulikuwa tuna changamoto ya umeme kwenye vijiji lakini kazi hiyo imekamilika. Ni matumaini yangu sasa Serikali inakwenda kukamilisha umeme kwenye vitongoji ikiwemo Kitongoji cha Mlima Mbwanda kule Mlimba, Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei unaipokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunambi?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kupunguza muda wangu kwa kulikubali hilo, lakini ninampongeza na yeye amepata umeme kwake na ataendelea kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi kwamba kazi imefanyika na kwenye Jimbo langu nilivyopata Ubunge mwaka 2020 tulikuwa tuna vitongoji 191 ambavyo havina umeme. Leo hii ninavyozungumza hapa vitongoji vimebaki 40 tu ndiyo havina umeme. Ninaamini hivyo vinaenda kukamilishwa siku za karibuni kwa sababu kuna ule mradi wa vitongoji 15 ambapo tayari tumeanza kuona kuna wakandarasi wanatekeleza kwenye vitongoji vya Umasaini na Kimala pale relini Kata ya Kahe Magharibi; Karango *A* na *B* - Mwika Kusini; Kiruiche, Kalimani na Kisimani kwenye Kata ya Makuyuni; Kwakipura - Mwika Kaskazini; Kiraracha kwenye Kata ya Kilwa Vunjo Kusini; Msufini - Kilwa Vunjo Mashariki; na Reli juu, Kahe Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo inatekelezwa na hivyo tunapunguza hata hiyo 40 ambayo tumesema. Ninashukuru sana kwamba Serikali imetekeleza ahadi yake kama ilivyofanya na kwamba hivi vingine 40 vilivyobaki navyo vitaenda kupata Wakandarasi na fedha ili tuweze kuona kwamba Wanavunjo wanajivunia nchi yao, wanajivunia maeneo yao na miradi yao ambayo wanatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba katika mambo yangu ya jumla kabla sijaenda mengine ya Vunjo huko, niseme kwamba mimi ninaamini kwenye Gridi Imara. Gridi Imara sasa ndiyo jambo kubwa na ndiyo mradi ambao tunatakiwa tuutekeleze kwa nguvu zote. Nimeona bajeti yake ni ndogo, mimi ninaamini kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ataenda kupigania tupate fedha ya ziada ili Gridi Imara sasa iweze kutekelezeka kwa sababu tunaona umeme unakatika katika, lakini siyo kwa sababu umeme ni mdogo, ni kwa sababu ya uimara mdogo wa usambazaji wa umeme ule. Kwa hiyo, hilo ninaona ni jambo la maana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninafikiri ni la umuhimu ni ile *Project* ya *LNG*. Watu wengi wameizungumzia kidogo jana, lakini ile *project* imekaa kwenye *drawing board* kwa muda mrefu. Tumekuwa tukiambiwa inakamilika, lakini tunamwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kutoa msukumo zaidi kwenye utekelezaji wa huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi tena Vunjo sasa niseme hivi; vijiji na vitongoji kadhaa kama nilivyosema vimepata umeme lakini kuna wananchi wanakaa mbali sana na zinapopita zile *line* za umeme. Kwa hiyo, ule mradi wa umeme jazilizi ni mradi pia ambao unahitajika kwa sababu kusema ukweli watu wengi ambao wanaona umeme umepita lakini hawawezi kuuvuta kwa sababu uko mbali na ni gharama kubwa kuweka zile nguzo inakuwa ni jambo gumu sana. Kwa hiyo, ninaomba kwamba sasa Serikali ione uwezekano wa kusukuma umeme jazilizi ili kupunguza gharama za wananchi kujiunganisha kwenye huu umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Vunjo kuna wananchi 784 ambao wanadai fidia kwa vile walipisha maeneo yao kupitisha umeme wa Kilowati 132 yenye umeme mkubwa kutoka Chungu kwenda Wilaya ya Rombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa wananchi wengi wapo kwenye kata yangu mojawapo. Kwa hiyo, tunamuomba sasa Mheshimiwa Waziri tusilaze damu hawa wananchi wakalipwe hiyo fidia yao. Fidia yao tayari imeshahakikiwa na Wizara yako wakishirikiana na Wizara ya Fedha. Ni fidia ambayo ni kama shilingi bilioni 7.6, siyo fedha nyingi, ninaamini kwamba wanakwenda kulipwa kwa sababu kusema ukweli wanasononeka licha ya kwamba Rombo wamefaidi na tunataka wafaidi huo umeme, lakini wao wanaona kwamba ni haki na kila Serikali ina hiyo sera ya kulipa fidia bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme hivi, kwa vile ninazungumza mambo ya fidia na huyu ni Naibu Waziri Mkuu, ninaomba pia nimbebeshe ambalo siyo la kwa kwake kabisa. Kuna fidia ya wananchi wa pale Gona na Njiapanda wamepisha ujenzi wa Kituo cha Kukagulia Mizigo cha Pamoja (*One Stop Centre* ya Kukagulia Mizigo) pale kwenye maeneo ya Gona na Njiapanda. Pia, wengine kule Mabungo ambapo napo wamepisha ujenzi wa kituo kama hicho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ninaomba unisaidie kusukuma hiyo, kwa sababu iko Wizara ya Fedha na *TANROADS,* lakini tokea mwaka 2013 wanapeleka haya madai yao na bado hawajapata kitu. Mheshimiwa ninaomba utusaidie kwenye hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei hii ni kengele ya pili. Kwa hiyo, tunaomba ...

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Masaburi, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kipenzi cha Watanzania, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Mheshimiwa Rais ambaye amejipambanua nchi hii, kwa kuhakikisha fedha zinapelekwa vijijini kwenda kutatua matatizo ya wananchi ni Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye amehakikisha huduma ya majiko ya gesi inaanza kusambazwa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amehakikisha katika kipindi kifupi vijiji vyote vya Tanzania vinapata miundombinu ya umeme, Mheshimiwa Rais huyu amehakikisha hata bwawa la kufua umeme la Rusumo lililopo wenye Jimbo la Ngara nalo linajengwa linakamilika, kila Mtanzania anasema Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitano tena ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan haijaja hivi hivi ni kwa sababu Mheshimiwa Rais huyu amegusa maisha ya Watanzania, si tu amepeleka nuru ya mwanga wa umeme vijijini ni kwa sababu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameondoa vibatari vijijini, kwa sababu wananchi ambao walikuwa hawana umeme wamekuwa wakiendelea kutumia vibatari hasa kwenye vijiji na sasa jambo hilo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameliondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale wanaosema *no reform no election,* wale wengine wa mlengo wa kushoto na wenyewe kimya kimya wanakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan mitano tena, hata kama wanaisema kimoyo moyo. Mimi na wananchi wa Jimbo la Ngara tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa

namna ambavyo anaendelea kuchapa kazi, tunamuombea afya njema ili aweze kuendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, wewe pamoja na viongozi wenzako wa Wizara ya Nishati kwa kuweza kuelewa na kutafsiri vizuri maono ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Wizara hii ya Nishati, hakika katika kipindi chako Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko tumejifunza funzo moja la tofauti kati ya kukatika kwa umeme na kukatika katika katika kwa umeme. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma ulikuwa unashangaa huku unaangalia mpira umeme unakatika paa! Wananchi wapo kwenye shughuli zao umeme unakatika, lakini sasa hivi tumeshuhudia maboresho makubwa kwenye Wizara hii ya Nishati hasa upande wa *TANESCO,* ambapo umeme unapotaka kukatwa wamejitahidi wateja wanapewa taarifa mapema, mwenye kujiandaa anafanya maandalizi na taarifa za kisasa zimeboreshwa katika kiwango ambacho wanawaeleza Watanzania kwamba umeme utakatika muda kadhaa na matarajio ya huduma ya umeme kurudi ni muda kadhaa, hivyo watanzania wanaweza kujipanga. Wale wanaomiliki mitambo ya kuzalisha kwa kutumia umeme wanaweza kujipanga na kufanya shughuli zao, hakika Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko umeboresha huduma ya *customer care* baina ya *TANESCO* na wananchi hongera sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, wewe na wenzako kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunapoelekea tutajifunza funzo linguine, tutakuja kujifunza tofauti na kukatika na kutokatika kwa umeme. Tunafahamu maendeleo ni hatua na hatua moja huanzisha hatua nyingine, kazi yenu mmeifanya vizuri hongera sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelekeza mchango wangu kwanza kwenye eneo la kuongeza matumizi ya umeme vijijini, wakati tunashukuru kwa kupongeza Serikali kufikisha miundombinu ya umeme kwenye kila makao makuu ya kijiji, bado

mahitaji ya umeme ni makubwa kuliko kipindi chochote kile. Wananchi kwenye vitongoji wanasubiria kupata umeme na kiu yao ni kubwa, ninaomba maboresho ya kuongeza matumizi ya umeme kwenye vitongoji yaanze mara moja hasa kwenye mwaka huu wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo mapana iwe ni kuhakikisha tunawapelekea wananchi kwenye vitongoji umeme ili inapofika mwaka 2030, asilimia kubwa ya wananchi kwenye vitongoji vya Tanzania wawe wamepata nishati ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho mengine kwenye kuongeza tija na matumizi ya umeme kwenye vijiji na kwenye vitongoji kuna hizi *transformer* ambazo imewekwa zenye *KVA* 50 msema ukweli ni mpenzi wa Mungu, hizi *transformer* uwezo wake ni mdogo, lazima nikiri na niseme kwamba uwezo ni mdogo kwa sababu tumekuwa tukiwalaumu *REA* na *TANESCO* ni kwa nini wananchi hawapewei huduma ya umeme, yamkini ni kwa sababu hofu yao ni kwamba wataongeza *load* ya umeme matokeo yake *transformer* zitashindwa kuhimili mahitaji ya umeme ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ushauri wangu kwa Wizara ya Nishati na *TANESCO,* tunaomba muanze sasa kutufungia transformer zenye ukubwa wa KVA 100 hadi *KVA* 200 hii inaenda kusaidia wananchi wengi kuweza kuunganishwa kwenye huduma ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza matumizi ya umeme, ninaomba Wizara hii ya Nishati na *TANESCO* pamoja na *REA* muweze kuanza ku-*push* mitungi ya gesi inayoendana sambamba na majiko yanayokubali kupika kwa kutumia umeme na kwa kutumia gesi hii itawasaidia wananchi wakati mwananchi anasubiria kwenda kununua mtungi wa gesi aweze kuunganisha jiko lake la kupikia kwa umeme na umeme uliopelekwa majumbani. Umeme mpaka sasa hivi matumizi yake ukienda vijijini kwa sehemu kubwa wanatumia kwa ajili ya mwanga na sehemu kidogo wanatumia kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuwasaidie ku-*push* ajenda hii tusiishie tu kusambaza mitungi ya gesi ndugu zangu wa *REA*, tusambaze mitungi ya gesi inayoendana na majiko yanayokubali kupika kwa kutumia umeme na kwa kutumia gesi na hata ikiwezekana kwa kutumia makaa, kama jiko hilo hilo unaweza ukaweka mkaa likapika tutafurahia kupata teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza matumizi ya umeme vijijini, ninashauri Wizara ya Nishati muanze ku-push ajenda ya kuondoa kodi kwenye vifaa vya kieletroniki vinavyotumika jikoni na sebuleni hapa ninazungumza matumizi ya *TV*, majiko ya umeme, *blender* za kusagia juisi na vitu vingine watanzania tunapowapelekea umeme vijijini, tuwasadie na kupata vifaa vinavyotumia huo umeme ili kuendeleza kurahisisha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba Wizara ya Nishati pushini ajenda ya kuondoa kodi kwenye vifaa hivi ili Watanzania waweze kuvipata kwa pesa kidogo ambayo wanaweza kuhimili. Nina uhakika jambo hili Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko analiweza, wale wanaomwongelesha wamwache tupo tunazungumza na yeye! Mwenyekiti awe unatusaidia katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko utusaidie ku-*push* hii ajenda Watanzania waweze kupata *access* ya vifaa vinavyotumia umeme ambavyo kodi yake imepunguzwa ili kuwe na mantiki ya kupeleka umeme kwenye vijiji na kwenye vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kuzungumzia ni namna gani *TANESCO* na *REA* wanajipanga kurejesha huduma ya umeme inapotokea umeme umekatika ama inapotokea miundombinu ya umeme imeungua. Hivi nimesimama hapa nina vijiji vitano ambavyo *transformer* zimeungua na wananchi wanasubiria huduma ya umeme kwa muda mrefu tumeendelea kuwatafuta *TANESCO, TANESCO* wanarudisha mpira kwa *REA, REA* inarudisha mpira kwa mkandarasi hivi ninavyozungumza Vijiji vya Mkalinzi, Kititiza,

Mkubu, Mumilamila na Mganza, wananchi hawa *transformer* zimekatika muda mrefu, zimeungua wananchi hawana huduma ya umeme. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha hoja hii uje na majibu, aje na suluhu ili niweze kukubaliana, nisiweke pingamizi kwenye bajeti hii. Aje na suluhu ni lini wananchi wangu hawa watapata huduma ya umeme ambayo imekatika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba, nilikuwa nangoja umalize naona humalizi muda wako umeisha.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Juliana Shonza, nilisema Mheshimiwa Masaburi, lakini atakuwa ni Mheshimiwa Juliana Shonza atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninashukuru pia kwa kupata anafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati ambaye pia ni Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Kwanza katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuweza kutimiza azma yake ya kuhakikisha kwamba anasambaza umeme kwenye vijiji na vitongoji vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Songwe sisi tunavyo vijiji 307, katika vijiji vyote 307 vitongoji vyote tayari vimeshafikishiwa umeme. Vijiji vipo 307 na vitongoji 1489 katika hivyo vitongoji 1489 tayari umeme umeshafikishwa katika vitongoji 749 na sasa hivi vimebakia vitongoji 740.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hivyo vitongoji 740 tayari katika awamu hii nyingine tumepata vitongoji 540 ambavyo hivyo vitongoji 540 Wilaya ya Ileje imepata vitongoji 107, Wilaya ya Momba imepata vitongoji 161, Wilaya ya Songwe imepata vitongoji 74, pia Wilaya ya Mbozi imepata vitongoji 205. Ombi letu wananchi wa Mkoa wa Songwe tunatamani kwamba hivi vitongoji ambavyo tumevipata 540 kazi hiyo iweze kukamilika kwa wakati ili wananchi hawa waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vitongoji vile 200 ambavyo bado vitakuwa havijaweza kupatiwa umeme tunaamini kwamba vitongoji hivi vingine 540 vitakavyo kamilika basi wananchi hawa ambao wanakaa katika vitongoji hivi 200 nao waweze kufikishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nizungumzie hali ya upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Songwe. Kwa miaka mingi sana hali ya upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Songwe imekuwa siyo ya kuridhisha, tumekuwa na changamoto ya muda mrefu ya kukatikakatika kwa umeme, changamoto hiyo inatokana na kwamba Mkoa wa Songwe tumekuwa tukitegemea stesheni ya umeme kutoka Mwakibete – Mbeya, kwa hiyo kwa miaka mingi Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tukiomba kwamba nasi tuweze kupatiwa stesheni yetu ndani ya Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana jitihada mbalimbali za Serikali ambazo zimefanywa zimesaidia sana kuweza kupunguza tatizo la kukatika umeme katika Mkoa wa Songwe. Mimi kama Mheshimiwa Mbunge ninakiri kwamba sasa hivi angalau sasa tunaona kwamba hali kidogo imetengamaa tofauti na ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya ndani ya Mkoa wa Songwe, vilevile kwa kuunganisha Mkoa wetu wa Songwe katika gridi ya Taifa ambayo *lane* yake inatoka Iringa inakuja Mbeya inapita Songwe, ikitoka Songwe inaenda Sumbawanga inaenda mpaka Zambia. Tayari ndani ya

Mkoa wetu wa Songwe Mheshimiwa Rais ameanza Mradi wa Kujenga Kituo cha Kupooza Umeme katika Kata ya Nkangamo. Kituo hicho kitagharimu zaidi ya bilioni 250, tayari mradi huo tangu uanze kutekelezwa mwaka jana mwezi Mei tunatarajia kwamba utakamilika mwezi Mei, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yetu wananchi wa Mkoa wa Songwe kwamba, mradi huo utakapokamilika kwa kiasi kikubwa sana utasaidia kumaliza tatizo la kukatikakatika kwa umeme ndani ya Mkoa wa Songwe, lakini tunafahamu kwamba mradi huo utakapokamilika utasaida sana kuweza kuchochea ukuaji wa kiuchumi na shughuli vile vile za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba Mkoa wa Songwe ni Mkoa ambao upo kwenye lango la *SADC*, kwa hiyo ni Mkoa wa kimkakati. Tutakapokuwa na umeme wa uhakika ndani ya Mkoa wetu wa Songwe tafsiri yake ni kwamba, tutaweza pia kuvutia wawekezaji wengi kuja kuwekeza na kufungua viwanda ndani ya Mkoa wa Songwe na hatimaye Mkoa wetu wa Songwe utapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshakuja mara kadhaa ndani ya Mkoa wetu wa Songwe, vilevile amekuwa akijibu maswali kwamba lini kituo hicho kitaweza kukamilika. Nami kama Mheshimiwa Mbunge juzi nilipita pale nikakuta tayari tumefikia kwenye utekelezaji wa 18%, tunaweza tukajiuliza ndani ya mwaka mmoja tumefikia utekelezaji wa 18% tafsiri yake ni kwamba umebakia mwaka mmoja tu ili mradi huo uweze kukamilika. Je, ndani ya huo mwaka mmoja 82% ambazo zimebaki zitakuwa zimekamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, uweze kufika ndani ya Mkoa wetu wa Songwe, tumemwona ametembelea kwenye vituo vya kupooza umeme pale Urambo pamoja na Kidatu na sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe tunatamani afike ndani ya Mkoa wa Songwe ili uweze kutembelea kituo chetu cha kupooza umeme pale

Nkangamo ili tuweze kujua kwa nini kasi ya ukamilikaji wa kile kituo ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Songwe tunatamani hata ikiwezekana pamoja na kwamba mradi inabidi ukamilike inabidi ukamilike mwezi Mei, 2026 tunatamani kwamba mradi huo ikiwezekana ukamilike kabla ya muda huo, kwa sababu tumeshuhudia pia kwenye miradi mingine imekamilika kwa wakati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nishati wananchi wa Mkoa wa Songwe wanakusubiri sana Songwe ili kwa pamoja tuweze kujua ni nini ambacho kinasabisha mradi huo uende taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie hali ya utendaji wa Shirika la *TANESCO* ndani ya Mkoa wa Songwe. Tunafahamu kwamba Mkoa wa Songwe ni mpya, jiografia ya mkoa wetu haijakaa vizuri. Jiografia sisi ni ya milima na asilimia kubwa ni maeneo ambayo ni ya vijijini. Watendaji wa Shirika la *TANESCO* ndani ya Mkoa wa Songwe wanapata shida sana kutokana na kwamba hawana vifaa vya kutosha hususani magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ndani ya Mkoa wa Songwe wanayo magari mawili tu, ambayo magari hayo mawili ndiyo ambayo yanatumika kwenye Wilaya ya Mbozi, lakini ukienda kwenye Wilaya ya Momba ambayo ni lango la *SADC* hakuna gari hata moja, hivyo inapelekea pale ambapo itakea changamoto labda *transformer* imeharibika au nguzo zimeanguka wananchi wanachelewa sana kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Wilaya ya Ileje huko nyuma tulikuwa tuna gari moja lakini tangu lile gari limepata ajali mpaka sasa hivi bado hatuna gari lolote ndani ya Wilaya ya Ileje. Zinapotokea hitilafu inawalazimu kwenda kuazima magari kitu ambacho ni gharama sana. Ukienda kwenye Wilaya ya Songwe ambayo ndiyo Wilaya ya uchimbaji, kule sisi tunachimba dhahabu, lakini bado *TANESCO* ndani ya Wilaya ya Songwe hawana gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri sisi tunafahamu kwamba wewe ni mchapa kazi na wananchi wa Mkoa wa Songwe wana imani kubwa sana na utendaji kazi wako kwa sababu tumekuwa tukikuona mara kwa mara ukichukulia hatua na kufanyia kazi mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyasema ndani ya Bunge hii. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, katika bajeti hii ninajua kwamba mnayo bajeti ya kununua magari, miongoni mwa yale magari ambayo wameyapanga kwenda kuyagawa kwenye mikoa mingine mimi niombe Mkoa wetu wa Songwe upate kipaumbele kwa sababu kwanza ni mkoa ambao ni mpya, lakini jiografia yetu sisi ni mbaya ili basi changamoto zinazotokea wananchi wale waweze kupata huduma kwa haraka kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana kwa kutunza muda. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mheshimiwa Edward Olelekaita, ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipatia nafasi na nguvu na afya kusimama kwenye Bunge lako Tukufu siku ya leo. Napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Wizara hii kwa kuwapa fedha, kwa kuhakikisha kuwa umeme unawaka na watu wanapata umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko ambaye ni Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye sekta hii ya umeme, kuwa wananchi

wengi amepata umeme wa kutosha. Pia, namshukuru Naibu wake Mheshimiwa Judith Kapinga, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wizara yote kwa ujumla, pamoja na Kamati ambayo inashughulikia jambo hili la nishati. Nawapa pongezi kwa sababu, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere, ambalo linatoa umeme wa maji. Kweli, tunashukuru sana Mheshimiwa Dotto Biteko na Naibu wako wamefanya kazi kwa sababu, sasa hivi mitambo yote tisa imekamilika, umeme unaingizwa kwenye grid na hivyo, umeongezeka mpaka megawati 4000, pamoja na vyanzo vingine vya umeme kama *solar*, jua na mambo mingine ambayo yanaongeza umeme. Kwa hiyo, sasa hivi tuna imani umeme umeongezeka na tunaweza kuuza hata nchi za nje. Kwa kweli, Tanzania tunajidai kwa uongozi wa Mama Samia, ambaye anatuongoza vizuri kwenye hii sekta ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kukatikakatika kwa umeme hata Mkoa wetu wa Morogoro umeme unakatika ingawa tuna vyanzo vingi vya umeme, kuna Kidatu na Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, ninashauri kuwa hili suala la kukatikakatika kwa umeme liangaliwe kwa sababu, umeme unapokatika vifaa vinaharibika, *TV* zinaharibika, *fridge* zinaharibika, mboga kwenye *fridge* zinaharibika. Kwa hiyo, ni vizuri uweze kuangaliwa usiwe unakatikakatika, la sivyo Mheshimiwa Dkt. Biteko anafanya kazi nzuri, ila hili jambo la kukatikakatika linatia doa. Inaonekana kuna hitilafu mbalimbali, siyo kusema umeme ni kidogo ila hitilafu nyingine, nyaya zinaweza zikashikana, zikafanya nini, kwa hiyo, watu wapate taarifa kama tulivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kusambaza umeme, hasa kwenye vijiji na vitongoji. Mkoa wetu wa Morogoro, vijiji vyote kwa wastani vimepata umeme ila tatizo liko kwenye vitongoji. Kwa hiyo, ninashauri kuwa, Mheshimiwa Waziri liangalie suala hilo la kupata umeme kwenye vitongoji kwa sababu, kila mmoja anafurahia kupata umeme, anapenda kupata umeme; umeme ni muhimu kwa binadamu, umeme ni muhimu kwa nchi

yetu, umeme unakuza uchumi, umeme unaendesha viwanda, umeme ni kila kitu. Kwa kweli, umeme ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hata hawa wakandarasi ambao wanawaweka kwenye kusambaza umeme waweke harakati kubwa kama fedha zipo, kusudi waweze kuweka umeme kwenye vitongoji vyetu. Kwa sababu, Mkoa wangu wa Morogoro, ukweli wameanza kuweka kwenye vitongoji, lakini vitongoji vingi pamoja na Taifa kwa ujumla bado havijapata umeme ila naamini kwa jitihada yako tutapata umeme, kama ilivyopangwa ila jitihada ziweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nishati safi na salama. Kwa kweli, majiko haya ya gesi, elimu imeenea, watu wanapenda sana kutumia nishati hii nzuri, inakufanya uwe na afya, ufurahie wewe mwenyewe wakati unapopika, lakini tatizo ni moja tu, bei bado iko juu. Waziri aangalie jinsi ya kuwapunguzia bei kusudi kila mmoja aweze kumudu kununua hii mitungi au mtungi unavyokwisha aweze kujaza kwa sababu, unakuta akinamama kweli wana mitungi, wanafurahia, lakini gesi inapoisha hana shilingi 23,000 ya kujaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba iangaliwe, ili kusudi waweze kuitumia, iwe endelevu, isiwe wanapata tu ndiyo mwisho. Iwe endelevu kusudi hata akinababa, kuna akinababa wengine wanapika, ni babalishe na wenyewe wanafurahia kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaliongelea ni kuhusu usambazaji, hasa wa umeme majumbani. Tunasema mijini ni shilingi laki tatu, vijijini ni shilingi 27,000, lakini kumbuka hata wewe unatoka huko mjini, kuna wengine wanatoka mjini hawamudu shilingi laki tatu kuingiza umeme, lakini wanaupenda. Kwa hiyo, ninaomba kadri tunavyozidi kupata umeme mwingi nchini kwetu halafu vyanzo vinakuwa vingi, kuna makaa ya mawe yanazalisha umeme, kuna maporomoko ya maji yanazalisha umeme, ninaomba waweze kuangalia kuingiza

umeme kwenye nyumba zetu bei iweze kuangaliwa kadri tunavyopata umeme mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo wananchi wamenituma ni kuhusu bei ya nguzo za umeme. Wanatamani kuweka, lakini wakati mwingine unakuta bei inakuwa juu kuingiza nguzo kama tatu kufika nyumbani kwake au ngapi, wakati mwingine unakuta ni shida sana. Kwa hiyo, ninaomba sana na Ienyewe waliangalie kusudi wananchi waweze kupata umeme wa kutosha, wafurahie maisha na waweze kufanya biashara ndogondogo. Kwa mfano, kusaga unga unatumia umeme, viwanda vidogovidogo hivyo unatumia umeme, mwanga unatumia umeme, yaani vitu vingi unatumia umeme; wanafunzi kusoma wanatumia umeme, sasa hivi ni *science and technology* tunatumia umeme. Kwa hiyo, ninaomba sana hiyo bei ya umeme iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi sana, kwa kweli, ukiwa na umeme unafurahi sana; watu wengi wanapenda umeme, watu wengi wanapenda nishati safi. Kwa hiyo, ninaomba sana hizo bei ziweze kuangaliwa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Biteko ambaye ndiye Waziri wa Nishati na Wizara nzima nafikiri umenisikia, nimeongea kwa kifupi, nimechangia kwa kifupi. Yale ndiyo nimetumwa na wanawake wa Morogoro na wananchi wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Christina Ishengoma. Sasa nimwite Mheshimiwa *Engineer* Tumaini Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Olelekaita, Mheshimiwa Ally Juma Makoa ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa fursa hii aliyotupatia tena ya kuchangia katika Wizara ya Nishati Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa wasilisho zuri la hotuba hii ambalo limesheheni mambo mengi, ambayo ni mafanikio na maombi, kwa ajili ya bajeti inayofuata. Nimpongeze sana Naibu Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa anayofanya ya kumsaidia Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba, kazi hizi zinatekelezeka; bila kuwasahau wataalam, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wawili wa mafuta na yule wa umeme pamoja na Nishati Jadidifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wako wakurugenzi mbalimbali wakiwemo wa *REA, EWURA* na *PURA* kwa sababu, Wizara hii imesheheni mambo mengi ambayo yanatumiwa na wananchi wetu. Kwa hiyo, niwapongeze wataalam wote kwenye Wizara kwa kazi kubwa ambayo inafanyika kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia hotuba hii nikagundua bajeti ya mwaka jana ilikuwa takribani shilingi trilioni 1.88 na ya mwaka huu imekwenda shilingi trilioni 2.25, maana yake ni kuna mambo makubwa mengi yanakwenda kufanyika. Kwa hiyo, kuwapongeza kwangu ni kwa sababu ya hayo waliyofanya na ambayo wanategemea kwenda kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Ukurasa Namba 116 utaona mafanikio mengi yameandikwa hapo, ambayo yanatokana na utekelezaji wa bajeti iliyopita, kwanza kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya uzalishaji, *installed capacity,* ambayo imekwenda mpaka takribani megawati 4000 na 31.71 katika hii na vyanzo mbalimbali vinaonekana hapo. Ukiangalia utaona vyanzo, kwa mfano, mitambo inayozalisha kwa kutumia maji inatuletea karibu megawati 2000.7, ukiangalia mitambo ya mafuta ni megawati 101, Tungamotaka *10.55* megawati na umeme jua una megawati tano, unaweza ukajua nchi hii ina jua, lakini tumeweza kupata umeme jua megawati tano tu, maana yake ni hatujafanya vizuri sana kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, ukiangalia huko ndani tuna *plan* ya kuwa na megawati 150, lakini kasi yenyewe nafikiri ni ndogo, iongezewe, ili tuweze kupata hiyo *energy mix*.

Kwamba, uzalishaji wetu uwe na vyanzo mbalimbali, ili hata maji yakipata changamoto, basi tuwe tunaweza kupata *atleast* umeme wa kuweza kufanya nchi isiende gizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile inaonekana tuna harakati, tuna mchakato mzuri wa jotoardhi. Mpaka sasa bado jotoardhi halijaonekana kwenye ile *energy mix* ya kwetu hapa nchini, niombe sana, hapa kwenye jotoardhi tufanye kitu. Wenzetu wa Kenya wanatakribani karibu megawati 1000, sisi bado tuko katika mchakato. Tuna kitu cha kujifunza kutoka kwa majirani zetu, ili tuweze kuhakikisha kwamba, jotoardhi kitu ambacho hakitakuwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi kitusaidie kuhakikisha kwamba, kwenye *energy mix* inatuletea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafanikio haya, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa sababu, ni mara ya kwanza *installed capacity* yetu imekwenda kwa takribani 151%, kwenye hotuba hii inaonesha yaani umezalisha mara *151% more,* inaonesha kabisa kwamba, kuna kazi kubwa imefanyika na mimi niwapongeze, kama tutaendelea kwa kasi hii maana yake ni tutakuwa na uwezo wa kukutana na *demand* yetu maana inabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia waliyopata mwaka jana na mwaka huu, imeshabadilika. Maana yake ni watu wengi wameanza kutumia umeme. Kwa hiyo, *maximum demand* tukienda baada ya muda mfupi itabadilika sana na baadaye mahitaji yetu yatakuwa makubwa sana. Kwa kuwa, sasa tumezalisha megawati 4000 tujitahidi kuona vyanzo tunavyoweza kuvipata, ili *at least* twende kwenye megawati 8000 kwa sababu, unajua mahitaji ya umeme ndani ya nchi hii yanaweza kuwa mara mbili au mara mbili na nusu baada ya miaka mitano tu inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewapongeza sana kwa sababu, inaonekana kwenye ripoti yetu kuna *line* nyingi zimejengwa za kilovoti 400; kuna *line* ya Singida kwenda Arusha, kuna *line* ya Kutoka Julius Nyerere kuja Chalinze, lakini kuna *line* ya kutoka Nyakanazi kwenda Kigoma. Hizi zitakupa uwezo mkubwa

wa kufanya watu wetu waweze kupata umeme, lakini kuna *line* moja ambayo inatakiwa ije hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kwamba, kutoka hapa Dodoma kwenda kuunga Singida, *line* hii ijengwe kwa wakati, ili kuhakikisha umeme huu sasa hiyo *networking* imeshapatikana na namna hiyo tutakuwa na uhakika kwamba, hata tukitaka kuuza umeme kutoka Julius Nyerere tutauuza kwa urahisi. Leo hii tukiulizana, tukitaka kuuza umeme wa Julius Nyerere itakuwa ni changamoto, ile *network* tunafikaje huko Singida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni changamoto. Kwa hiyo, niombe sana hili lifanyike mapema, ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunaweza ku-*access* kwa wenzetu hiyo *Eastern Africa Power Pool* tuhakikishe kwamba, tunaweza kuitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi wetu wa *TAZA* ambao unaenda kutuunganisha kule Kusini, nao ufanyike kwa wakati, uongezewe kasi, ili uweze kukamilika, lakini pamoja na haya kumeongezeka wateja. Wateja wameongezeka kutoka 2,766,745 sasa wanaonekana wamefika 5,449,278. Inaonekana kabisa katika miaka hii mitatu, minne, wateja wameongezeka sana. Kilichofanyika ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika ni kwamba, tunawapongeza *REA* kwa sababu, wamepeleka umeme vijijini. Sasa kazi kubwa tuliyonayo ni tuna vitongoji vingi, ukiangalia kwenye taarifa jumla tuna vitongoji kama 64,000, vilivyopata umeme ni kama 33,000 hivi kwa hiyo, vitongoji 31,000 bado havijapata umeme. Kuna kazi kubwa ndugu zangu, yule wa *Rural Energy Master Plan,* kuhakikisha wanapanga vizuri ni kiasi gani na wanapata wapi mafungu kwenye hizi bajeti zetu kuhakikisha kwamba, vitongoji vyote tulivyonavyo vinapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipolifanya hili wananchi wetu kule kwa sababu, wanaishi jirani wataanza kuna kama kuna watu wamependelewa na wengine wameachwa nyuma. Kwa hiyo, tulifanye hili ndani ya miaka mitatu, minne tuhakikishe kwamba,

kila kitongoji kina umeme, ili kila mmoja ashiriki kutumia umeme, lakini vilevile ashiriki kujenga uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kulisema hapa ni habari ya gesi asilia *CNG,* tunahitaji sana *CNG*. Mikakati yetu inaonekana kabisa, tulikuwa na vituo viwili mwaka 2021, sasa tuna vituo tisa, lakini vituo tisa havitoshi. Mimi na jirani yangu hapa tulikwenda Dar es Salaam kukagua tukagundua vituo bado vinahitajika sana, magari mengi sasa yanatumia *CNG* kule Dar es Salaam. Maaneo ambapo *CNG* ipo na ukiangalia kwenye takwimu wameonesha mwaka 2021 tulikuwa na takribani 29,000 leo tuna 188,000 maana yake ni *multiplication* yake utaona ongezeko ni kama mara saba hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuhakikisha kwamba, Mradi wa *LNG (Liquified Natural Gas)* umefanikiwa tutaweza kuhakikisha gesi hiyo inaweza kufika Dodoma, itaweza kupelekwa Mwanza, itaweza kupelekwa Arusha na itaweza kupelekwa Mbeya. Mazingira hayo yatafanya watu wengi waingie kwenye matumizi ya *LNG* na kwa matumizi hayo kwa sababu, gharama imeshaonekana ni ndogo watu wengi watapata uchumi bora kuliko ilivyo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai tu kwamba, hapa kwenye *CNG* tufanye kweli, wanasema Waswahili, kuongeza vituo. Ipo *plan* kwamba, mpaka mwaka kesho, kwenye ripoti hii, vituo vitakuwa 20 sawa, lakini Dodoma kutakuwa na vituo vingapi, ili magari ya Serikali yaliyo Dodoma yatumie gesi hii? Changamoto yetu iko hapo, lazima tuje na *LNG*. Kwa hiyo, niwaombe sana, kwenye hili tuhakikishe kwamba, tunakwenda kasi na kuhakikisha tunaweza kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninaona taa imewaka, kuna *clean energy,* hapa tumeingiza kwenye *national energy compact*. Watu wetu wameanza kutumia gesi, watu wetu tumewapelekea mitungi, lakini hatujawapelekea elimu ya kutosha, ili watumie gesi huko vijijini na bado hatujawapelekea vituo viwe karibu ili wakitaka ku-*refill* wasipate gharama kubwa kwenda kujaza mitungi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, umewasha taa, ninaomba kuunga mkono hoja. Ninaomba niishie hapo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Tumaini Magessa. Sasa nimwite Mheshimiwa Wakili Edward Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Makoa. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia kwa miradi mingi sana ya umeme nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema vijiji vyote kuna umeme na hakuna kijiji hakina umeme, sasa tunamaanisha kazi aliyofanya Dkt. Samia kwa miaka minne ni ya mfano. Kwa hiyo, kwa kweli, tunampongeza kwa dhati sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kweli, kwa kazi kubwa anayofanya; mzee wa kusema na kutenda. Kwa kweli, tunampongeza kwa kazi za Wizara na kazi anayoifanya kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia. Kwa wale wanaofuatilia kwa karibu, Mheshimiwa Dkt. Biteko ameongeza kasi kubwa sana kwenye masuala ya nishati nchini, lakini mzee, ziara zake tunazifuatilia sana, anaponya watu wengi sana na anazungumza vizuri sana; watu ni walewale, ambapo kwa kweli, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu tunampongeza sana. Yeye ni kati ya viongozi ambao ni *very humble* sana na silaha kubwa kwenye uongozi ni kuwa *humble*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Wakili Judith Kapinga, naye kwa kweli, anafanya kazi nzuri sana ya kumsaidia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Ni kijana, lakini anafanya kazi nzuri sana, anapeperusha bendera ya vijana vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumpongeze Katibu Mkuu, Wakurugenzi na mameneja wa Mikoa. Ninazungumza habari ya Mkoa wa Manyara na Dodoma kwa sababu, Kiteto kwa

*TANESCO* tunaitikia Mkoa wa Dodoma, lakini Mameneja wa Wilaya kwa kweli, wanafanya kazi nzuri sana. Kwa mfano, wa Kiteto wameanzisha *WhatsApp group* la kutupa *information* kila wakati za kukatika kwa umeme na pale panapotokea hitilafu. Huo ni ubunifu kwa hiyo, kwa kweli, lazima tuwapongeze kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachowaomba tu, kwa sababu wateja wao wengi wana namba zao za simu, kwa wale ambao hawawezi kuingia kwenye *WhatsApp group,* hizi *message* zikiwa zinakwenda kwa wateja wao kupitia mitandao ya simu ninadhani itasaidia kuboresha huduma kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiteto miaka mine, mitano iliyopita tulikuwa na vijiji 29 ambavyo havikuwa na umeme, ikiwemo tarafa nzima anakotoka Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, tunavyozungumza sasa, vijiji vyote 29 vina umeme na vitongoji 161 vina umeme; tumebakiza kama 118 hivi. Kwa kasi inayoendelea mimi sina shaka kabisa kwamba tutamaliza hili jambo na Watanzania wengi wanapenda sana umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nilete ombi moja hapa. Kuna Kitongoji kinaitwa Kilimawanga, Kijiji cha Mbigili na Mwenyekiti wa kitongoji hicho anaitwa Nelson Elisha Chibada. Kwa nini ninamtaja huyu? *In fact,* kama kuna wenyeviti ambao wanafanya kazi nzuri sana kwa kutoa taarifa za wananchi huyu Mwenyekiti wa Kitongoji anaongoza, Kiteto nzima. Ninaamini hata anaweza akawa anaongoza nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wakati anapiga simu akisema habari ya umeme kwa wananchi wake. Umeme anaouhitaji ni wa kilometa 2.2 tu (umeme mdogo *LV*) na ni milioni 32 tu. Kwa hiyo, mzee wa kusema na Kutenda; mimi ninajua ameshaanza kuandika hapa na ninajua kuwa akwishaanza kutoa maelekezo. Milioni 32 ni kidogo sana na hawa wananchi wa Kijiji cha Mbigili ni wachapa kazi wazuri sana. Inawezekana hata leo wamejaa kwenye *TV* wanasikiliza, watapata majawabu yao leo na kwa kweli yeye mzee wa kusema na kutenda, ninajua atamaliza hili, la

hiki kitongoji. Hivi vingine tunaweza tukasubiri mpango wa Serikali, lakini angalau kwa hiki Kitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katikati, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa, Kiteto tumekuwa na shida ya umeme. Siyo kukatika, ni kukatikakatika, kwa muda mrefu sana inawaunguzia wananchi vifaa vyao na ilileta kero kubwa sana. Niliwahi pia kumpigia Mheshimiwa Naibu Waziri na Mkurugenzi wa *REA* kuelezea jambo hili. Ninajua kazi iliyokuwa inaendelea, ilikuwa ni kufanya mifumo hii ya zamani irekebishwe; tunaelewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sasa shida nyingine kubwa ya Kiteto, sisi tunapata umeme *line* moja tu kutoka huku Dodoma. Ikikatika sehemu moja miji yote ya Kiteto hakuna umeme. Kwa hiyo, tukizungumza na wataalam, kama watajenga *switching station* hapa kwa majirani zetu na mtambo wa kupooza unaotoka Kilindi na tukawa na *line* nyingi za Kiteto, watatusaidia sana. Ninaambiwa ni fedha ndogo tu, takriban bilioni tatu sijui. Wakitusaidia hilo angalau watafanya wananchi wa Kiteto siyo *button* moja tu ikikatika basi wilaya nzima inakosa umeme kwa sababu ya *line* moja. Kwa hiyo ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alichukue hili kwa uzito wake ili wananchi wa Kiteto nao wapate neema hii ambayo Dkt. Samia analeta kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingi sana zimefanyika Kiteto. miradi ya *REA IIII - Round II* imekamilika, Miradi ya UVIKO imekamilika, miradi ya ujazilizi inaendelea kwenye vitongoji 37, miradi ya ujazilizi *HE2A* kwa vitongoji 15 inaendelea. Kweli kazi inaridhisha kabisa na timu yao iliyopo huko inafanya kazi nzuri sana. Tukipata hii *switching station* na kituo hiki cha kupoozea cha Kilindi ili isaidie Kiteto kupata *line* nyingi, ninadhani watakuwa wamemaliza suala la umeme Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia amefanya kazi nyingi sana na tumepata miradi mipya mingi sana. Tumejengewa sekondari tano, minara ya simu takriban 14, na yote hii inahitaji umeme. Hivyo ningetoa ushauri kwamba tuwe na fedha maalum ambayo kazi yake ni kulenga hii miradi mikubwa iliyoletwa na

Mheshimiwa Dkt. Samia. Tulenge taasisi za dini na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto wanapata mnara wa *Radio Tanzania* kwa mara ya kwanza tangu uhuru. Sasa leo tusipopata huduma hiyo bora kwa sababu ya kukosa umeme; ninadhani ni ushauri wetu kwa unyeyekevu mkubwa sana. Hii miradi mipya ya shule shikizi takriban 20; kuna miradi mingi imekamilika ambayo inahitaji *transformer* kama sita au saba tu (Mbeli huko, Ndilali, Sunya, Olpopong'i, Mbigili, Zambia, Kisima cha Maji Engusero, Kibaya Mjini na Mafichoni). Pia minara ya simu katika maeneo ya Kinua, Partimbo, Loolera, Songambele, Loltepes, Olpopong'i, Makame, Orkiush; vyote hivi vikipata umeme na *transformer* hizi, hali ya umeme Kiteto itakuwa njema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sisi ambao tunaitikia mikoa mingi. Tuko Manyara lakini *ki-TANESCO* tuko Dodoma. Wakati mwingine kwenye mikutano hii ya *RCC* hatupati taarifa nzuri sana ya *ki-TANESCO* kwa sababu tunaitikia mkoa mwingine. Ushauri wetu, mawasiliano yawe bora kati ya mameneja wetu hawa ili na sisi tunaoitika Dodoma *Ki-TANESCO* tuwe tunapata taarifa hizi kupitia Mkoa wetu wa Manyara. Kwa mfano, Mkoa wa Manyara tu Simanjiro wanaitika Kilimanjaro na Kiteto wanaitika Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya kwa sababu hii ni kengele ya pili, niwatakie kila la heri na tupitishe bajeti hii haraka sana ili watu wakafanye kazi. Ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Wakili Edward Kisau. Sasa nimwite Mheshimiwa Ally Juma Makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Sofia Mwakagenda, ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hoja katika bajeti hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoturahisishia siasa zetu na

kazi zetu kule majimboni kwa kuleta fedha nyingi kwa ajili ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, kwa kazi kubwa wanazozifanya za kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanaondoka kwenye nishati chafu na kuingia kwenye nishati safi. Kwa kweli kazi wanayoifanya ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze na kumshukuru *Engineer* Hassan, *DG* wa *REA*, anafanya kazi kubwa sana. Pia Meneja wetu wa Mkoa Bwana Donald Shamba naye ni kijana mchapa kazi, amepiga mzigo mkubwa sana na bila kumsahau Meneja wangu wa Wilaya *Engineer* Bakari Kalulu. Kwa kweli ninawashukuru kwa sababu wamewatendea haki sana wananchi wa Jimbo la Kondoa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa na karoho ka kutaka kushika shilingi ya bajeti hii ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Hata hivyo, baadaye katika kuwaza na kufikiria nikakuta nikaangalia mambo mema mengi aliyoyafanya nikakuta kale karoho kanaondoka kenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika kwenye kiti cha Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wakati tunazungumzia kwenye masuala ya mitaa kupelekewa umeme kwa zile laki tatu, laki sita na kuendelea. Nilikwenda kumweleza juu ya hali mbaya ya wananchi wangu; kutokana na mitaa yao kuwa sawa na vijiji tunaomba tupunguziwe bei. Akatoa maelekezo kwa *Engineer* Hassan. Kwa kweli nilikwenda kwa maelekezo yake na nikapatiwa maeneo ambayo hayakuwa na umeme. Mtaa mzima haukuwa na umeme. Kata nzima ya Suruke ilikuwa haina umeme, lakini leo kata yote na mitaa yote hiyo imefikishiwa umeme na wamewashiwa umeme. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Judith.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuchoka, nikamwambia kuhusiana na suala la mitaa mingi kuwa haina umeme, akanichomekea kunipa vile vitongoji 15. Leo hapa

ninapozungumza mkandarasi yupo anavuta waya. Kwa hiyo, baada ya muda kwa kuwa nguzo zimesimama maana yake watu wale watawashiwa umeme. Ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sivyo hivyo tu, mwezi uliopita niliuliza swali hapa. Tulipeleka nguzo kwenye Mtaa wa Chemchem – Kingale na tukapeleka nguzo kwenye Mtaa wa Tampoli – Kingale wakati mitaa hii hata umeme mkubwa ulikuwa haujafika; wakasimamisha nguzo na tulikuwa tunasubiri kupata nguzo kwa ajili ya kufikisha umeme mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikauliza swali hapa, Mheshimiwa Kapinga akawa ameruhusu tupelekewe nguzo 88. Nilipokwenda kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu akakubali nguzo zote 188 ziende. Pia hivi ninavyozungumza zimekwishafika nguzo 110 jimboni. Maana yake ni kwamba, hii kazi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyaona hayo nikagundua kwamba yeye ni mchapa kazi, Naibu Waziri ni mchapakazi na watendaji wa Wizara yake ni wachapakazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, baada ya kwenda kwake akaniongezea tena vitongoji sita ambavyo ni Kwa Mtwara, Guruma, Churumai, Kunduchi, Guta na Gulai. Maeneo haya hayakuwa na umeme kabisa; leo tayari ameyaingiza kwenye tenda (mfumo). Ninajua kuwa baada ya muda mkandarasi ataingia na watu wale watawasha umeme. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na ninamshukuru pia msaidizi wake pamoja na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo ninadhani Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu akilifanya nitakuwa nimevunja rekodi yangu mimi mwenyewe. Akilifanya jambo hili atanisaidia kuwa nimevunja rekodi yangu mimi mwenyewe kwenye jimbo lile. Maana rekodi ya waliotangulia nilikwishaivunja muda mrefu sana. Sasa, tukishirikiana mimi, yeye pamoja na Mheshimiwa Rais, tutaivunja rekodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mtaa unaitwa Mongoroma kuna Kituo cha Afya kikubwa sana ambacho Dkt. Samia Suluhu Hassan alitupatia fedha tukakijenga, hakina umeme. Kwa hiyo, akinisaidia kupeleka pale nitakuwa nimevunja rekodi yangu mwenyewe…

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mtaa wa Hachwi na…

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Makoa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpembenwe.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, hiyo rekodi haitavunjwa kwake yeye tu; hata pale katika Jimbo la Kibiti, imevunjwa rekodi kwa Mheshimiwa Waziri kwa maelezo ya Mheshimiwa Rais kutupelekea umeme katika kata za visiwani ambazo tulikuwa hatutegemei kupata umeme. Sisi tunaendelea kushukuru kwa sababu watu wenyewe ni wale wale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Makoa, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa hiyo kwa sababu ninaona namna ambavyo mimi mwenyewe nilivyovunja hiyo rekodi. Ninaamini na wao watakuwa wamevunja rekodi katika maeno yao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na maombi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii mitaa mitatu; Mongoroma ambako kuna kituo cha afya kikubwa, Chandimu na Hachwi,

ambapo Hachwi ina maeneo mawili, Kutumo na Hachwi yenyewe. Ninaomba mitaa hii, kwa sababu tayari amekwishamaliza vijiji vyote nchi nzima, sasa siyo hekima tukasema tumemaliza vijiji halafu kuna mitaa imebaki. Kwa hiyo, nilikuwa ninamwomba atakapokuwa *ana-windup* hebu *just* awatajie hawa watu wa Mongoroma, Hachwi na Chandimu awaeleze ni namna gani nao utakwenda kuivunja hii rekodi ya kuhakikisha mji ule wote unang'aa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Ally Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Innocent Kalogeris, ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru wewe kwa nafasi. Vilevile, ninaomba pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uhai na kuendelea pale nilipoishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa mbali sana na wachangiaji waliopita, hususani katika kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na timu yake, pamoja na Mheshimiwa Rais. Kwa kweli tunayo mengi ya kuzungumza kuhusiana na masuala, acha tu umeme au nishati, lakini na mambo mengine ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosoa ni kichocheo cha tija ya maendeleo na ni kichocheo cha tija ya kufanya au utekelezaji. Tunapokosoa hatumaanishi kwamba hii Serikali labda ya Awamu ya Sita haijafanya mambo mema mazuri, hapana. Ukiangalia ni Serikali ambayo imefanya vizuri sana katika mambo mengi kama nilivyosema hapo, ukiacha nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa kazi zilizofanyika katika awamu hii kwenye Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na timu yake ya nishati, tunayo ya kuzungumzia, kwa maana ya kukosoa

kwa nia ile ile ya kuongeza chachu ya kuhamasisha kufanya jambo liwe jema zaidi; kwamba maendeleo yawe makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninataka nizungumzie dhana hii ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vya nchi hii. Ninakubaliana na hilo na sina shaka kwa hilo; lakini katika mazingira yangu niko tofauti. Ninaomba nitofautiane kidogo kwa lengo lile la kutia chachu kusudi tuweze kufikia lile lengo la kukamilisha vijiji. Mazingira niliyokuwa nayo mimi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na vitongoji vingi vikubwa ambavyo vyenye hadhi sawa kabisa na vijiji, lakini vitongoji hivi viko katika umbali mrefu kutoka kwenye makao makuu ya kijiji mpaka kuvifikia. Sasa unakuta umeme umeishia kwenye makao makuu ya kijiji peke yake, lakini wakati huo kule kitongojini umeme haujafika; na kama nilivyosema kwamba kuna idadi ya watu wengi, kuna vitongoji vingine kuna zaidi ya watu 600. Maana yake ni kwamba watu walioko pale wana hadhi ya kuwa kijiji. Kwa hiyo kuwa-*treat* kama ni kitongoji kwa kweli ninafikiri inakuwa siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwamba, hivi vitongoji vyote vyenye umbali mrefu kutoka kwenye makao makuu, vingine ni umbali wa kilometa tano, halafu vyenyewe havipewi umeme kwa kipaumbele; kwa minajili ya kuwa ni vitongoji vitakuja kupewa baadaye; kwa kweli ningeomba jambo hili lisiwe katika jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nitolee mfano. Vitongoji hivyo hivyo unakuta ni vitongoji ambavyo vina kazi au vina taasisi muhimu sana kama vile shule na zahanati ziko pale, lakini sasa unakuta havijapewa umeme kwa sababu tu ni vitongoji. Sasa hali hii inafanya hata zile taasisi zisifanye vizuri. Nikitolea mfano kwenye Kata ya Mkululu kuna Kitongoji cha Lusonje ambacho kina watu 700; na kuna shule pale. Halikadhalika Mkonde kuna takribani watu 600, na kuna msikiti hapo; Nanjota kuna Kitongoji

cha Mnazi Mmoja kuna watu zaidi ya 700 na kuna ujenzi wa zahanati kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Mchauru kuna Kitongoji cha Mkowo kina watu zaidi ya 500, lakini kuna kisima pale. Vilevile kuna vitongoji vingine vya Nanganga na Rivango. Kitongoji cha Nanganga kina wananchi zaidi ya 500 na Rivango zaidi ya 500 na kuna shule ya msingi pamoja na zahanati. Hata hivyo, vitu hivi vinakosa kupata umeme na kufanya sasa utekelezaji wa mapinduzi ya kimaendeleo kuwa ni ya chini na ya kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdavila katika Kitongoji cha Nalyongolo kuna watu zaidi ya 600, kuna ujenzi wa shule shikizi hapa. Halikadhalika kuna Kitongoji cha Mtolya kuna watu zaidi ya 400; Lipumbulu kuna Kitongoji cha Nnandembo kuna watu zaidi ya 500, Chikowedi kina zaidi ya watu 500, Umati, Lupaso watu zaidi ya 800 na kuna shule ya msingi pia. Mbuyuni pia kuna Kitongoji cha Chipindimbi kuna watu zaidi ya 400. Hawa wote ni watu ambao wamekosa umeme kwa kigezo cha kusema kwamba ni kitongoji. Kwa kweli jambo hili nafikiri tungeliangalia kwa umakini hususani katika jimbo langu. Ninaomba sasa hivi vichukuliwe kama ni vijiji, vifanywe kama kipaumbele na vipewe umeme mapema tena kabla ya kupeleka umeme katika maeneo ambayo tayari umeme upo kwa kisingizio hicho cha kitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ningetaka kulizungumzia hapa ambalo ni la msingi sana, ni jambo la Mradi wa *LNG*. Ningetaka kufahamu ni nini ambacho kimetokea kwenye mradi huu. Kiuhalisia mradi huu ni mradi muhimu sana hususani kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi au Mikoa ya Kusini kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia, mradi huu muhimu sana hususan katika mikoa ya Mtwara na Lindi au mikoa ya kusini kwa ujumla. Kumekuwa na hisia mara nyingi sana, watu wa mikoa ya kusini kujihisi kana kwamba mipango inayowahusu hususan inayohusiana na maendeleo imekwenda kwa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mifano mingi sana. Mfano ni huu mradi wa gesi, tangu mwanzo kipindi cha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete mradi wa gesi ulikuja ukaanza kuonekana kwamba ni mradi mkubwa ambao utakomboa mikoa ya kusini, lakini *from nowhere* huu mradi ulikwenda ukawa *stagnant,* umekaa kimya, haueleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Hassan, wananchi wamepata hamasa kubwa sana, wakati waliposikia kwamba miradi yao ya gesi inaanza, hususan katika mradi huu wa Likong'o wa *LNG*, mradi wenye thamani kubwa sana wa Dola za Kimarekani bilioni 30 ni mradi mkubwa sana, lakini sasa kumekuwa na ukimya mkubwa, lakini hatuambiwi tatizo liko wapi? Nataka tuulize Serikali, kuna jambo gani limejitokeza kwenye mradi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuambizane ukweli kama kuna jambo baya limetokea kwenye mradi huu, siyo vibaya tukaambiwa kwa sababu gani? Wananchi wamekuwa wakiwekeza kidogo kidogo katika eneo hili kwa pesa zao mfukoni, lakini na pesa pia kutoka benki. Pesa hizi zinapotea bure, lakini kama wangefahamu bila shaka wasingefanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa ni vizuri kuambiwa, kusudi tujue kwamba ni kitu gani kinatakiwa kuwaambia wananchi wanapotuuliza. Kuna wakati wanatuuliza tunakosa majibu sahihi. Sina ubaya wowote wa kusema kwamba kuna ubaya unafanyika katika hili, hapana, lakini nafikiri inatamani sana mradi uwe umetekelezwa ambapo watu wengi wa kusini wana utegemea mradi huu uwe ni chachu ya maendeleo na kuwakomboa katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu nakutegemea sana, sina shaka na wewe, utendaji wako ni wa hali ya juu, umefanya mambo makubwa sana ambayo nimeyaona kwa macho yangu, umetuletea *turbine* katika mkoa wa kusini ambako kulikuwa na changamoto kubwa sana ya umeme wa kukatikakatika, lakini hali kadhalika umeidhinisha mradi mkubwa sana ambao utajengwa kutoka

Tunduru kuelekea Masasi, sina shaka na hilo na sasa hivi watu wanalipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka mradi huu wa Likong'o Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu awekee nguvu zote watu wa mikoa ya kusini wanufaike na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Mchungahela, umesikika na *LNG*. Tunaendelea, tunakwenda kwanza kwa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, halafu mkandarasi Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Florent Laurent Kyombo.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara hii ambayo iko kwenye Kamati ambayo nipo. Katika Kamati ukurasa wa 15 tumetoa mapendekezo na maoni kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kabla sijaendelea, naomba nitoe pole kwa Naibu Waziri Mkuu kwa kifo cha Ndugu yetu Eng. Nyamhanga, ni kiongozi aliyekuwa makini, lakini Mungu amempenda zaidi, sisi tuliobaki kazi yetu kuiga pale alipotuachia tufanye kazi kwa uaminifu kama alivyokuwepo marehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naishukuru pia Serikali, kwa mara ya kwanza kufanikisha Mradi wa Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, suala la umeme sasa siyo tatizo tena, kilichobaki ni kuhakikisha miundombinu inatengenezwa na wananchi sasa mambo ya kukatika umeme yasiwepo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vitongoji takribani 32,000 katika nchi nzima lakini mpaka sasa ni vitongoji 927 ambavyo vimepata umeme. Kamati pamoja nami, tunaishauri Serikali kuongeza *speed.* Tunatambua wameongeza muda wa kuunganisha vitongoji kwa umeme mpaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *speed* ya kuongeza vitongoji kupata umeme, maana huko chini ndiko kwenye wananchi. Tunaomba sana *speed* iongezwe sawasawa na tulivyowashauri katika ukurasa wetu wa 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mikoa ambayo haijaingia kwenye gridi ya Taifa, tunashukuru Kigoma imeingia sasa katika *list,* kulikuwa kuna Kigoma, Katavi, Rukwa pamoja na Lindi na Mtwara. Tunaomba vilevile *speed* iongezeke kwa mikoa iliyobaki waweze kupata umeme, na uweze kuingizwa kwenye gridi ya Taifa kwa sababu kwa kuingiza umeme huko, basi hakutakuwa na matatizo katika mikoa hiyo tajwa nao watapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kubwa sana katika Wizara. Upande wa kibajeti sisi tunategemea fedha nyingine kutoka kwa wafadhili. Kuna ndugu zetu wa *IMF,* waliahidi kutoa zaidi ya shilingi bilioni 52, lakini imekuwa ikionekana kwenye bajeti halafu hatujaipata. Tuombe ndugu zetu waweze kuifuatilia kwa sababu *OC* mpaka sasa ina 16% peke yake. Ili uweze kuwa na maendeleo, ni lazima fedha za miradi au fedha za kazi ziwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tunaomba usimamizi wa upatikanaji wa fedha na tuombe Wizara kwa sababu kazi ya Bunge imesimama kuisemea Serikali, kuiambia, basi Wizara ya Fedha ihakikishe tunapata fedha kwa wakati kwa sababu Bunge likipitisha fedha, ni kazi ya Wizara kutoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kupata fedha nusu, 50% mnazuia watendaji wasiweze kutimiza wajibu ambao wamepewa na Serikali, kwa sababu Bunge ni chombo ambacho kina mamlaka ya kupitisha bajeti, sasa bajeti zetu tunakaa hapa miezi miwili au mitatu, tunapitisha bajeti, halafu fedha hazitoki. Hii inakuwa siyo sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Shirika letu la *TANOIL*. Hili Shirika kiukweli lina umuhimu kwa sababu Serikali isipokuwa na chombo cha kusimamia mafuta na kuhifadhi chenyewe inakuwa siyo sawa na kuwa na makampuni binafsi kunaweza kukatokea hujuma mbalimbali, lakini shirika hili limekuwa lina deni kubwa

sana zaidi ya shilingi bilioni 21. Ukusanyaji wa madeni kutoka *TANOIL* unaenda kwa kusuasua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namfahamu Mheshimiwa Waziri, weledi wa kazi alionao, fanya utaratibu mahususi kabisa wa kuhakikisha fedha zetu zaidi ya shilingi bilioni 21 ziko nje ya mfuko wa Serikali, zirudishwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ripoti inasema ni asilimai ndogo sana kama 6.8 ambayo tumekusanya ambayo ni shilingi bilioni 1.43. Hiyo ni hela ndogo sana. Tunaomba ufanyike utaratibu wa makusudi kuhakikisha Shirika hili linakusanya shilingi bilioni 21 ambazo ni pesa nyingi zinazohitajika kwenye Bajeti ya Mfuko wa Serikali na kwenye Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala la gharama za umeme. Tunajua kuna umeme wa *REA* ambao vijijini wanajiandikisha kwa shilingi 27,000, lakini umeme huo huo kuna sehemu nyingine zinasema, ikiwa ni mita 30, hiyo shilingi 27,000; ikiwa mita 70 ni shilingi 515,000, hiyo *different* ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutoe matabaka kati ya vijijini pamoja na mijini. Tunafahamu kwamba wakati mwingine ni pesa za miradi makusudi kusaidia wananchi wa vijijini kupata umeme, lakini ambaye anapita kwa mita 120 analipa shilingi 696,000. Wananchi kule chini wanaona kama ni tabaka kubwa sana. Basi tuna kazi kubwa sana, kama tunakuwa tunataka ibaki kama ilivyo, tuweke elimu kubwa sana ya wananchi waweze kuelewa, kwa nini huyu analipa shilingi 27,000, na huyu analipa shilingi 320,000 na mwingine analipa kiasi kingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tutoe elimu kitengo kinachohusika, basi kitoe elimu kuliko kutokusema inaleta lawama kwa wananchi. Pia kama Kamati, tunafikiri tukiweka angalau tukapandisha hiyo shilingi 27,000 na tushushe ile ya shilingi 500,000 na angalau hapo katikati tuweze kuona wananchi wetu wote wako katika tabaka moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kabisa matumizi ya nishati safi. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia hili na tumeona jinsi ambavyo wananchi wameanza kuelewa matumizi ya nishati safi. Tunafahamu kabisa majiko ya gesi ambayo mengine tuligawa, kama sisi wasimamizi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wametoa majiko ya gesi ya ruzuku ambayo yamemsaidia mwananchi wa kijijini kutokununua hiyo gesi kwa shilingi 48,000 kwenda kununua kwa shilingi 20,000 na maeneo mengine imeshuka hadi shilingi 18,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mahitaji ni makubwa, tayari tumeshafanya elimu kwa wananchi, na wako tayari kutumia nishati safi, lakini bado tunahitaji kuongeza idadi ya majiko haya ili yaweze kufika kijijini kwa watu wote. Nafahamu katika Wilaya ya Rungwe tulipata tu kiasi cha majiko 3,000. Kwa hiyo, yanakuwa siyo mengi. Kama siyo 300,000, *sorry*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuongezewe majiko na yapelekwe kwa kutumia Wizara na kwa kusimamiwa na Wakuu wa Wilaya ili watu wetu waweze kuendeleza pale walipoishia, lakini mwisho wa siku bado elimu inahitajika, zile gesi zikiisha wengine wanatupa yale mitungi na watu wabaya wasioitakia mema nchi yetu, wanauza kama vyuma chakavu. Kuna haja ya kuweka ukali zaidi na ulinzi kuhakikisha tunalinda rasilimali hizi za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kasi ya kuongeza umeme vitongojini, nimeshasema, lakini mwisho wa siku tunahitaji kusaidia maeneo ambayo ni ya kimsingi. Kwa mfano, vijijini wanahitaji mashine za kusaga kwa ajili ya pampu za maji, basi tuwekeze maeneo yale kama *speed* hiyo ni ndogo, lakini pale tunaita *center* za vijiji tuhakikishe tunaweka umeme angalau kusaidia jamii kwa ujumla wake kwa sababu kukiwa kuna mashine ya kusaga, kukawa kuna pampu ya maji au shuleni na vitu kama hivyo, tunaomba tuongezewe nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naamini kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa

Naibu Waziri wa Nishati wanayo kazi kubwa sana na wamefanya kazi kubwa sana, basi hapa ambapo wameishia kwenye bajeti hii tunaomba wasimamie haya ambayo tumeyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja bajeti hii kwa sababu kule kijijini wanahitaji umeme na tunahitaji kuwapitishia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia. Nimwite sasa Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa matamanio yake makubwa ya kutaka kuifanya Tanzania iendelee kung’ara na kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mafanikio makubwa kwenye *SGR,* tumeona mafanikio makubwa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo limo katika Wizara hii ambayo nataka kuizungumzia, na pia tumeona mafanikio makubwa kwenye Daraja la Kigongo Busisi, kwenye afya, shule na mambo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, japokuwa kuna wenzetu wengine wanasema kwa nini tunampongeza Rais? Wabunge tunajua jitihada ambazo amezifanya Mama huyu kwa Watanzania katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, lakini msaidizi wake *Advocate* Kapinga na watendaji wote wa

Wizara na taasisi zilizokuwa chini ya Wizara. Kiuhalisia, hakika wanamsaidia Mama katika suala la umeme na mambo mengine yanayohusu Wizara hii, tuna kila sababu ya kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Mameneja wa Mikoa wa *TANESCO,* na vilevile Meneja wangu wa Mkoa wa Morogoro, *Engineer* Fadhili, pamoja na Meneja wangu wa Wilaya ya Morogoro vijijini, ndugu yangu Oswald kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, nami niende kwenye suala la kuchangia. Nianze na kuchangia kwenye suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa. Mama wakati anachukua Madaraka, bwawa hili lilikuwa kwenye 14% au 15% hadi 16%, lakini leo tunaambiwa limekamilika, na bwawa hili liko kwenye Jimbo la Morogoro Kusini na Jimbo la Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uhalisia kwamba limekamilika mashine zote tisa zinafanya kazi na umeme umeingia kwenye gridi ya Taifa. Kwa kuingia kwenye gridi ya Taifa, maana yake nini? Tumeongeza kasi ya ukuaji wa uchumi katika Taifa letu, lakini vilevile kuna ongezeko la umeme kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kukupongeza Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko kwa kazi kubwa ambayo umemsaidia mama, kiuhalisia umefanya mambo makubwa na Taifa litakukumbuka katika kipindi ambacho umeongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio kwenye hili suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere, sisi Wanamorogoro na Wanapwani, nitaendelea kusema sitaweza kuliacha hili mpaka Serikali itupe majibu. Bwawa limekamilika, kuna suala la *CSR* ambayo *CSR* hiyo mimi toka naingia Bungeni naisema kila siku, lakini Serikali mnatuambia tutakaa Wanamorogoro, Wanapwani na tutatoka na majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kaka yangu, mdogo wangu wakati anapokuja kutoa majibu ya hoja ambazo zimewasilishwa na Wabunge, hebu naomba utupe majibu Wanamorogoro na Wanapwani, lini haki yetu hii ya *CSR* tutaipata? Sisi Wabunge tunakwenda kwenye uchaguzi, wananchi wetu watatuuliza maswali kuhusu suala hili, tunaomba utusaidie, utupatie majibu tukawaambie wananchi wetu *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani, na naachilia, naogopa kushika shilingi yake na kuheshimu sana, lakini napenda nishike shilingi ili kusudi nipate majibu yaliyokuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kuna suala tuliambiwa Wanamorogoro na Wanapwani tungepewa shilingi bilioni kumi kumi, sisi kwenye Halmashauri yetu tulizipangia mpaka matumizi, lakini tunapozungumza mpaka leo hakuna fedha hiyo. Nini hatma ya fedha hiyo walau itangulie wananchi wetu waweze kupata matokeo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza jambo hilo, nizungumzie kwenye suala la *REA*. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini kumpongeza yeye mwenyewe binafsi Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na wasaidizi wake. Pia kipekee sana, nampongeza Mtendaji Mkuu wa *REA Eng*. Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuhakikisha nchi nzima inawaka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu Morogoro Kusini nina kata 17, katika kata 17 nina vijiji 85, vitongoji 437. Leo tunapozungumza, kata 17 zote zinawaka umeme katika vijiji 85. Wakati tunaingia kwenye Bunge hili na kwa awamu yangu ya pili, vijiji vilivyokuwa na umeme vilikuwa ni 36 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo vijiji 85 vyote vinawaka umeme na kiuhalisia kazi kubwa iliyofanywa na *REA*, kazi kubwa iliyofanywa na Wizara na kazi kubwa ya kutoa fedha aliyotoa Mama, Jimbo langu katika kata 17, kata tisa ziko milimani na huko

milimani kutoka makao makuu ya barabara kuu kwenda kwenye makao makuu ya kata ndiyo kuna barabara, lakini kwingine kote ni milimani; mfano Rongwe, Ukwama, Kumba, Mgata, Bwakila Juu, Kigajila kote, Nyamila yenyewe ni milimani, lakini umeme unawaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kumpongeza Mama, lakini tunampongeza Mheshimiwa Waziri kama msaidizi wake Mama kwenye sekta ya nishati, lakini na Mtendaji Mkuu wa *REA* na watumishi wote wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu bado katika vitongoji 437, vitongoji vyenye umeme ni 191. Pia kuna vitongoji 15 vya jimbo tulivyopewa kwa Wabunge wote, bado havijafanyiwa kazi, lakini nashukuru na ninapongeza katika mgao ambao umetoka tayari nimepata vitongoji vingine 90 ambavyo vitaenda kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, vitongoji 121 vilivyobakia vifanyiwe kazi na wananchi hawa wapate umeme kwa sababu wana uhitaji sana wa umeme kwa maslahi mapana na matumizi kwa faida ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, kuna suala la Shule ya Sekondari ya Kolelo. Tulizungumza kwamba umeme ufike kwenye taasisi na umeme kwenye Sekondari ya Kolelo, haujafika. Nilizungumza na *Eng*. Cecila ambaye ni Mhandisi wa *REA* Mkoa wa Morogoro, amekwenda kuangalia na ameleta mahitaji kwenye *REA* Makao Makuu. Ombi langu, tuwapelekee umeme watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa ni ombi kuzungumzia suala la *substation*. Umeme katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini unakatikakatika, unatoka kwa kupitia Chalinze unatoka kwa kupitia Morogoro na hii ni kwa sababu hatuna *substation* ya kupoza umeme matokeo yote yanayojitokeza Halmashauri nzima inakwenda kuwa giza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, tunakoenda tuangalie jinsi gani tunaweza kufanya ili kusudi tupate *substation* kwenye eneo la Lukurunge kwa sababu watu wa *TANESCO* walikuwa wanasema wameshafanya *feasibility study* zao mara mbili lakini wanasubiri pesa, na pesa ikipatikana tutafanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze Serikali kwa kukamilika kwa kituo cha kupoza umeme cha Msamvu ambacho kinalisha karibu Morogoro yote. Tulikuwa na changamoto kubwa sana katika kipindi kilichokwisha lakini sasa hivi katika katika ya umeme kwa Morogoro tumekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi katika hili suala la kuhitaji *substation* kwa Morogoro, Morogoro vijijini sasa hivi hasa kwenye Kata ya Bwakila Chini, kwenye Kata ya Rundi kuna viwanda vikubwa vya uchenjuaji wa madini ya *graphite*. Sasa kama tutapata *substation,* tutashawishi wawekezaji wengine wengi wakajitokeza na wananchi wetu wakaendelea kupata maendeleo makubwa na uchumi kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naendelea kuipongeza *TANESCO,* katika bajeti ya mwaka 2024 nilizungumzia suala la Mkoa wa Morogoro kwamba ni mkoa wa kimkakati; una vyanzo vitatu vya maji: kuna Kihansi, Kidatu na hili Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mkoa wa Mororgoro ni mkubwa, nilizungumzia suala la magari na ninashukuru Meneja wangu wa *TANESCO* wa Wilaya amepata gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nilizungumzia suala la Ofisi ya Meneja wa *TANESCO* katika Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini ambayo mpaka sasa bado. Meneja yule anakaa kwenye kontena. Mheshimiwa Waziri hebu angalia kupitia *TANESCO* tumjengee nyumba yule ili aweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalogeris, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa nafasi uliyonipatia kuchangia katika bajeti yetu hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza kabisa, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo imefanyika ndani ya kipindi hiki ambacho sisi sote ni mashahidi tunaona kuongezeka kwa kuweka miundombinu ya umeme katika maeneo yetu na ni ushuhuda tosha kwamba katika vijiji vyote 12,318 umeme umeweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumeona ongezeko la uzalishaji wa umeme katika nchi yetu kufikia *Megawatts* 4,031. Kwa kweli ni mapinduzi makubwa ya kinishati ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Rais ambaye ni mbeba maono wa nchi yetu, niendelee kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kaka yetu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko kwa kuliongoza jahazi hili la Wizara ya Nishati kwa ufanisi mkubwa na tunaona mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko anao wasaidizi wake; tunamwona Mheshimiwa Judith Kapinga ambaye amekuwa msaidizi wake mahiri sana. Pia, Watendaji Wakuu wa Wizara hii akitangulia Katibu Mkuu, kaka yetu Felchesmi Mramba; tunawaona Naibu Makatibu wakuu wote: Dkt. Mataragio na Dkt. Khatibu Kazungu, pia, watendaji wakuu wa taasisi zote ambazo zinasimamia maeneo haya tukianza na kiongozi wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tutoe pole kwa kuondokewa na *DG* na tumpongeze *DG* wa *REA* ndugu yetu *Eng.* Hassan ambaye naye amekuwa akifanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi hawa wanafanya kazi na viongozi wetu wa mikoa. Tunao Mameneja wa *TANESCO* mikoa yote wakiongozwa na Meneja wa Mkoa wa Kagera na Mameneja wetu wa wilaya. Mimi mahususi nampongeza Meneja wangu wa Wilaya Bwana Peter Masanja kwa kazi kubwa pamoja na watumishi wote ndani ya Wizara ya Nishati, Taasisi zetu za *REA,* na *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo manne. Kwanza, pongezi ambayo imekamilika, lakini pia nitoe shukrani kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Missenyi. Pia, nitakuwa na changamoto ambazo zinawakabili wananchi wa Missenyi na mwisho nitakuwa na maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la shukrani, kama ambavyo tumeendelea kuona nchini, katika vijiji vyote 77 ndani ya Wilaya ya Missenyi kwa sasa hivi vyote vina umeme. Ni pongezi na shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais na kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambaye kwa kweli amekuwa ni *(pioneer)* rubani mzuri katika Wizara yetu hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona Wilaya ya Missenyi ina vitongoji 356. Katika maeneo hayo yote, vitongoji 184 sasa hivi vina umeme na kwa sasa hivi kazi inaendelea kwa kasi kubwa katika vitongoji 26. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Missenyi kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kiongozi wetu katika Wizara hii ambaye ameaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika usukani wa Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaendelea kushukuru kwa umeme sasa hivi katika vitongoji 15 unaendelea kufungwa. Nguzo zimeshaletwa kupitia kampuni ya *CCC* na tunaona kazi inaendelea. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali yetu na imekuwa ni historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo umeme ulipita juu ya vitongoji hivi kwenda maeneo mengine kwa miaka

takribani 10, lakini vitongoji hivyo vilikuwa havina umeme. Chini ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sasa tukiangalia vitongoji vya Nyungwe, Kakoni na maeneo mengine na vyenyewe viko katika orodha ya kufungiwa umeme. Nguzo zimeshashushwa katika maeneo hayo na wananchi wana matarajio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo letu kwa kweli tunaendelea kuipongeza Serikali. Historia imeandikwa, sasa hivi watu maeneo mengi wanapata mwanga kupitia umeme wetu na wanautumia katika shughuli za kiuchumi ikiwemo katika uzalishaji na maeneo mengine ya viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo letu pamoja na mazuri haya yote ambayo yamefanyika, lakini bado tunazo changamoto moja mbili tatu ambazo ninaamini ziko ndani ya uwezo wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuzitatua na zikaleta afueni kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza Mheshimiwa Waziri wetu wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu ni fidia ya wananchi wa Mradi wa Kakono. Tunajua kwamba Serikali imefanya kazi kubwa kuendelea kuzalisha umeme na mojawapo ya watu ambao waliathirika na eneo hili ni wananchi wa Wilaya ya Missenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wananchi wote ambao wako katika mkondo wa Mradi wa Kakono waweze kupewa fidia. Mwaka 2024 nilisimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuomba wananchi waweze kulipwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati alijibu kwamba Serikali imeshaainisha mahitaji ya wananchi hao na wanadai takribani shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ruhusa yako naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, wakati anahitimisha angalau wananchi wa Missenyi waweze kusikia hii fidia ya *1.6 billion* kwa wananchi ambao wako katika fidia ya Mradi wa Kakono italipwa lini kwa sababu mwaka 2024

tulisema mwezi wa Saba wangelipwa, lakini mpaka sasa hivi wanasubiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sababu wana imani na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninaamini tutakuja kupata majibu mazuri ili wananchi hawa waweze kupewa fidia hiyo na waendelee na shughuli nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wengine ambao wamesema maeneo mengine umeme unakatika. Hata hivyo, naamini kwa Wilaya ya Missenyi inawezekana umeme unakatika kuliko maeneo mengine yote, na ni kwa sababu Wilaya ya Missenyi na Mkoa wa Kagera kwa ujumla tumebarikiwa kuwa na mvua nyingi. Sasa hizo mvua zisiwe zinaleta athari kubwa, tuone jinsi gani ambavyo Serikali imejipanga. Pamoja na kupata mvua nyingi, isiwe ni sababu ya wananchi hao kupata adha ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia sana eneo hili. Ukifuatilia kwa wataalamu, wanasema ni *vegetation* kwamba miti inakua sana na migomba inakua chini ya waya, lakini ninaamini ule urefu wa mgomba hauwezi kufika hata nusu ya ule urefu ambao nyaya zetu zinakuwa zimefungwa. Pia, wanasema sababu ni vidhibiti radi; naomba kupitia Wizara hii ambayo iko makini chini ya Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko iweze kuja na suluhisho kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera na mahususi Wilaya ya Missenyi ambako umeme kwa kweli unakatika mara kwa mara na hasa kwa sababu tuna mvua nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona umeme unaendelea kukatika kila mvua ikitaka kunyesha, wataalamu wanakata umeme mapema ili kunusuru uharibifu wa miundombinu zaidi. Sasa tuwe na suluhisho la kudumu ili sasa wananchi hawa ambao wanaendelea kupata baraka ya mvua basi na umeme waendelee kuupata katika kipindi chote, hata kama mvua inanyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana katika eneo hili ambalo limekuwa ni changamoto, umeme upo katika maeneo ambayo umeshafika, lakini sasa wananchi waweze kusaidiwa na changamoto hii ya kukatika kwa umeme kuondoa uharibifu wa mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niendelee kuomba, pamoja na kazi kubwa ambayo inafanyika Serikalini ambayo imeendelea kusambaza umeme na mtandao, umeendelea kuongezeka, lazima kuwe na uhitaji wa rasilimaliwatu na vitendeakazi. Hili inawezekana likawa ni hitaji la nchi nzima. Naomba uangalie kwamba rasilimali za wataalamu katika maeneo yetu ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Missenyi sasa hivi ina takribani wataalamu 10, lakini tunaona mtandao umeendelea kuongezeka. Kwa hiyo, tunaomba sasa mambo mazuri ya kuendeleza mtandao wa umeme kuongezeka, basi iende sambamba na kuongeza wataalamu ili kazi mahususi iweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba, tuna mahitaji ya gari katika Wilaya ya Missenyi ambayo ina gari tatu zilizochakaa ili iweze kuwasaidia wataalamu wetu waweze kufanya kazi kwa weledi na kuwafikia wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la nne ni suala la bajeti. Wilaya ya Missenyi kuna baadhi ya maeneo yanapata umeme katika *line* inayotoka wilaya nyingine. Kwa mfano, katika kata zetu za Kashenye na Kanyigo, zinapata umeme kutoka wilaya nyingine ambayo Wilaya ya Bukoba, lakini usimamizi wa *technical support* yote inafanyika ndani ya Wilaya ya Missenyi. Wakati mwingine kuna mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua maendeleo ni hatua, lakini naomba itoshe kusema kwamba Wizara iangalie ni namna gani ya kuweza kutupatia bajeti ya kujenga *line* ya umeme ambayo itatoka Kyaka pale ambapo kuna *substation* ndani ya Wilaya yetu ili na usimamizi uwe ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba tena, tunacho Kiwanda cha *Kagera Sugar,* kinafanya kazi nzuri. Tunaomba kipate *dedicated line* yake kama kiwanda ili sasa ule umeme ambao unaenda kwenye kiwanda na unatumika kwa wananchi, basi kiwanda kiweze kuwa na *line* yake mahususi kuendelea kutekeleza kazi yake ambayo inafanyika vizuri. Pia, na wananchi waweze kuwa na *line* yao ili kuondoa ile kunapokuwa na hitilafu kiwandani na wananchi wanaathirika au kunapokuwa na hitilafu kwa wananchi na kiwanda kinaathirika. Hii itasaidia sana kuwasaidia wananchi wetu wa Wilaya ya Missenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine ni vitongoji 172 vilivyobaki. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati katika eneo letu la Missenyi analifahamu. Katika huu mradi wa vitongoji 30,000 vilivyobaki, basi naomba Wilaya ya Missenyi ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hivi vitongoji 172 vilivyobaki viweze kufikiwa na hao wananchi waendelee kufaidi matunda mazuri ya Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na hii inaenda sambamba na majazilizo katika vitongoji ambavyo vingine vimeshapata umeme, lakini umeme huo umeenda katika nyumba chache. Kwa hiyo, naomba sana tuweze kuyafikia maeneo yote ili wananchi hao waweze kufaidi nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine ni gharama za kuunganisha umeme. Wilaya ya Missenyi katika maeneo ya vijiji vyote 77 bado ina taswira ya vijiji na ndiyo usajili wake kwa mujibu wa sheria. Tukiangalia Sheria ya 282 ya Serikali za Mitaa bado vimesajiliwa kama vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ule utaratibu uliotumika kuainisha maeneo yaliyochangamka kidogo yamepita maduka saba au 10 yamechangamka na wakati mwingine lami imepita ikaonekana kwamba haya maeneo wananchi hawa wanaweza wakaunganisha umeme kwa shilingi 352,000/=. Naomba tufanye marejeo kwa sababu wananchi wa Missenyi bado wote wako katika vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii shilingi 27,000 ndiyo itumike katika maeneo yetu ambayo wananchi wanaweza kumudu kuliko maeneo mengine ambayo kidogo unaona umeme umepita pale na barabara ya lami imepita halafu wanasema kwamba eneo hili sasa ni eneo ambalo linalipa shilingi 352,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nakushukuru kwa nafasi, lakini naomba changamoto ambazo zimefanyika katika *REA* Na.1 na Na. 2 ndani ya Jimbo letu ziweze kusahihishwa katika mradi unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru kwa nafasi, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kyombo nakushukuru sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi leo ya kuweza kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia afya hata leo nimeweza kusimama hapa kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kipenzi Mama Jemedari, Mama wa Shoka, Mwanamke Chuma, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya ya kutuletea maendeleo kwenye nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu ya mema aliyotutendea Wanamsalala. Mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Msalala, ndiye shahidi namba moja ambaye ninatoa

ushahidi na ushuhuda wa mambo mazuri ambayo ameyafanya kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuwa shahidi wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anamteua Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko aliteuliwa wakati wa msukosuko mkubwa sana ndani ya Shirika la *TANESCO,* umeme ukiwa unakatikakatika, na kulikuwa kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuteuliwa kama alivyosema kaka yangu Olelekaita hapa KNK (Kusema na Kutenda), alikaa chini na kufikiria ni namna gani anaweza akatatua tatizo la upatikanaji wa mafuta kwa bei nafuu ambayo itamsaidia Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa tunavyozungumza habari ya mafuta imekuwa ni historia. Sasa upatikanaji wa mafuta kwenye nchi yetu uko salama na jambo limetulia kabisa na hakuna changamoto yoyote ile kwenye suala zima la mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, kwenye suala zima la umeme na penyewe ameweza kuona ni namna gani anaweza kutatua changamoto ya kukatikakatika kwa umeme akielekeza nguvu kazi kubwa sana katika kuhakikisha ya kwamba kuna uzalishaji, usambazaji na uuzaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Msalala tulikuwa na upungufu wa umeme takribani vijiji 64, lakini leo hii tunavyozungumza, kwenye Jimbo la Msalala lenye kata 18 na vijiji 92 upatikanaji wa umeme kwenye vijiji vyote, tayari umefika na wananchi sasa wanatumia huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa *REA,* kaka yangu Hassan; nampongeza pia Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. Kazi kubwa mliyoifanya *REA* kwenye Jimbo langu la Msalala, wananchi wamenituma niwaletee shukrani zao za dhati kabisa, wanawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, kwani Wanakahama tulipompelekea ombi la namna gani tunapata changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma, aliridhia ombi letu la kuhakikisha kwamba anaifanya Wilaya ya Kahama kuwa Mkoa wa Ki-*TANESCO,* na hivyo sasa kupelekea halmashauri zetu ikiwemo Halmashauri ya Msalala kuwa ni wilaya za Ki-*TANESCO* kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na nina imani ananisikiliza vizuri sana. Mheshimiwa tunakupongeza sana, tayari Meneja wa Wilaya wa *TANESCO* kwenye Halmashauri ya Msalala ameshariopoti kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, changamoto iliyopo kwa sasa, kwa sababu tayari tumepata wilaya, na kama unavyofahamu, na ninampongeza sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, kwani aliweza kutenga eneo la kujenga Ofisi ya Wilaya ya Ki-*TANESCO* kwenye Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwamba, tayari mimi kama Mbunge niko tayari kuchangia tofali na niliahidi tofali 5,000 tuweke hapo *site* na eneo lipo. Sasa naomba atakapohitimisha hapa kwa moyo wake ule ule ambao alitusaidia kupata Mkoa wa Ki-*TANESCO* na Wilaya za Ki-*TANESCO* aende sasa kutusaidia tupate fungu kidogo ili tuanze ujenzi wa ofisi ya Meneja huyu wa *TANESCO* ili aweze kupata ofisi ya kufanya shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Meneja huyu ameripoti, lakini hana usafiri. Naomba sana Mheshimiwa Naibu

Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, chonde chonde kwa udharura wake, naomba tupatiwe gari ambalo Meneja huyu litamrahisishia kutembea kwenye vijiji vyetu na kwenye maeneo hayo ya Jimbo la Msalala. Naomba sana, kilio chetu kwa sasa ni gari la kumwezesha Meneja kutembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nishauri jambo kwenye suala zima la usambazaji umeme. *REA* wanafanya kazi nzuri sana ya kupeleka na kuunganisha umeme, lakini mtandao ambao wanaunganisha ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia sasa watu wa *TANESCO* kwenda kuhakikisha ya kwamba wanatoa elimu kwa wananchi namna ya kuvuta umeme kwenye nyumba zao ili wananchi sasa waweze kutumia haki yao ya msingi ya kuvuta umeme kwenye nyumba zao, kwani kwenye maeneo mengi *REA* wanapokamilisha mradi wanaondoka, kunakuwa hakuna mtu mwingine kwa ajili ya mwendelezo wa kwenda kutoa elimu ili wananchi hao waweze kuvutiwa umeme kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuweze kuboresha sasa huduma bora itakayotolewa na watu wa *TANESCO* itakayoenda vijijini kutoa elimu namna ya kuweza kulipia. Kama unavyofahamu Mheshimiwa Naibu Waziri nawapongeza sana, wameanzisha huduma ya NIKONEKT kwenye mtandao, lakini sasa kwenye maeneo yetu kama unavyofahamu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, asilimia kubwa ya maeneo yetu wananchi hawawezi kutumia hizi simu za kiganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanahitaji sana kupata elimu na wanahitaji watu wa *TANESCO* waweze kutenga muda kuwafikia wananchi kwenye maeneo hayo ili waweze kuwasaidia kujaza fomu na kuwasaidia kuwapa namna ya kuwaonesha wananchi waweze kutumia haki yao ya kuvuta umeme kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kazi aliyoifanya kwenye Jimbo la Msalala

kwenye umeme ni kubwa mno. Nafahamu tayari tumeshapitisha bajeti ya kwenda kupeleka umeme kwenye vitongoji na baadhi ya vitongoji bado umeme haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini na ni matumaini yangu makubwa juu ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu katika kuhakikisha kwamba baada ya bajeti hii (na niseme tu ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja), sasa kazi ya kwenda kuwapelekea wananchi umeme kwenye vitongoji vyetu iweze kufanyika kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri ikimpendeza, siyo mbaya akatoa maelekezo wakaanzia kwenye Jimbo la Msalala ili waweze kusambaza umeme kwenye vitongoji hivyo kwa sababu kama unavyofahamu sisi ni wazalishaji wa madini na ni wakulima kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji umeme ili tuweze kutumia umeme huu kwenye shughuli zetu za uzalishaji madini. Tunahitaji huduma ya umeme ili tuweze kutumia kwenye umwagiliaji na kwenye kuchakata mazao kwenye maeneo yetu haya ya Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, na ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, endelea kupambana, tuna imani kubwa na wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Iddi ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii muhimu mchana huu

katika kuchangia bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa nchi yetu, na sisi Watanzania wote, yote hayo ni kwa mipango yake, nchi ni salama, tuna amani, upendo na mshikamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa nchi nzima pia kwa Jimbo la Mbulu Mjini. Kwa kweli pamoja na Serikali nzima ya Awamu ya Sita, tunampongeza, tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu, Mheshimiwa Rais na Serikali nzima, pia wananchi wa Mbulu tunaahidi kumlipa kwa fadhila na utendaji uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kutoa pongezi nyingi kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwanza, ni msikivu, pia kila unachomweleza kinaenda kutekelezwa na ikishindikana anakupa mrejesho kwamba hii imekuwa na wakati mgumu tuitafutie wakati ujao kwenye mipango yetu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbulu Mjini kwa niaba yao pia nitoe pole nyingi kwa msiba wa Mtendaji Mkuu wa *TANESCO* pia na Watanzania wote waliotangulia mbele za haki, Mwenyezi Mungu awapokee kwenye ufalme wake wa milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee hali halisi ya sura ya Jimbo la Mbulu Mjini. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, unisikilize rafiki yangu, kwa kweli Mbulu Mjini ina jiografia ya aina yake. Mimi natoka Jimbo la Mbulu Mjini, lakini napakana na Halmashauri nne. Napaka na Karatu, Mbulu Vijijini, Babati Vijijini, pamoja na sehemu kidogo ya Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo langu nusu au karibu 80% ni sura ya vijiji. Katika mitaa 58 ukitafuta mji wenye uhalisia, inaweza kuwa pengine kama 20% tu ya katikati ya mji lakini hutashangaa ukitoka kilomita moja tu kutoka Mjini unakuta nyumba nyingi hazina umeme. Hii ni kwamba, jitihada kubwa zilichukuliwa, vijiji vyote sasa hivi vimeunganishwa na umeme, lakini sehemu iliyoguswa na umeme kwa maana ya wanufaika ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maombi yangu kwa eneo hili? Kwanza, ni kama alivyoniahidi Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwamba, atarudia kuona upya na wataalam kuangalia sura ya Mji wa Mbulu na mitaa yake, basi timu yake iendelee kufanya ile kazi tuliyokubaliana, ili walau eneo kubwa la Mbulu Mjini lirudishwe kwenye gharama ya shilingi 27,000/= na pia sura ya Vijiji kwa nchi nzima kwa sababu unaweza kukuta umeme umefika pengine kwa miaka kumi, miaka nane, miaka saba katika eneo la Kijiji, lakini wanufaika ni kaya 20 ama 30. Hali hii inafanya wanufaika wanakuwa wachache na Serikali imetumia gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nchi na kama Wizara, tunawaomba tuangalie namna ya motisha ama mpango kabambe wa uingizaji wa umeme katika maeneo yote ambayo yanahitaji ujazilishi kama ilivyo Jimbo la Mbulu Mjini. Nakushukuru kwa sababu maeneo mengi toka tulivyozungumza kwenye bajeti ile ya mwaka 2024, tumepata vitongoji 15 vimesambazwa umeme, japokuwa baadhi ya maeneo, kaya ziko chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba tu kusema kwamba, safari ya kupeleka umeme kwenye vitongoji na vijiji isingefanikiwa bila mpango mkubwa wa Kitaifa wa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa lazima tutambue jitihada za waasisi wa nchi yetu walioanzisha wazo hili la ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, pia sasa na ambaye ametekeleza maono haya, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na sasa umeme unapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia eneo lingine ambalo ni muhimu kama nchi. Eneo hili ni la utafiti wa kuongeza vyanzo vya umeme. Tukitegemea asilimia kubwa ya vyanzo vya umeme wa maji, huwezi kujua tabianchi inaweza ikatubadilishia hali kiasi gani baadaye kwa maana ya ukosefu wa mvua na mabwawa yakashindwa kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunapozungumza umeme kila kitongoji, umeme kila kaya, umeme kwenye viwanda, hali hii baada ya miaka kumi wataalam watazame ikoje? Je, mahitaji ya wakati huo yatakuwaje kwa jinsi ambavyo umeme tulionao tutautumia na utakidhi haja ya matumizi ya nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumze eneo lingine la miradi hii ya *REA*. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ni msikivu sana. Kwenye eneo hili la *REA* miradi hii haina uwazi sana kwa wananchi. Kijiji kinapelekewa mradi kwa mfano nchi nzima kama ilivyo vijiji vyetu, Mbunge hawezi kujua mradi huu ni wa muda gani? Utakuwa una walengwa wangapi kwenye matarajio? Thamani ya mradi na mwajiri ni nani? Pia mtekelezaji ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaweza kwenda ofisi ya *DC,* wakaenda pengine *site* tu wakafanya kazi zao, lakini wananchi wanauliza maswali mengi. Ndiyo hali inayopelekea katika kijiji ambako umeme umepelekwa unakuta waliounganishiwa umeme pengine ni wananchi kumi ama 20, kumbe mradi ule ungeweza ku-*cover* wananchi pengine 40 ama 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inaifanya miradi kutokuwa na tija. Pia wale wapokea mradi kama wazawa hawatafahamu mradi wao, kwa sababu ni kodi ya Watanzania na fedha za Watanzania, mfumo huu ubadilishwe. Waheshimiwa Wabunge, wafahamu mradi uliopo kwenye eneo lake, ni wa gharama gani? Unalenga walengwa wangapi? Wa thamani gani? Kwa sababu fedha bado ni za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kwamba, mara nyingi wakandarasi wanalalamika,

kwa mfano, Mbulu Mjini tuna vijiji 34 vyote vimeunganishwa umeme na vyote vimewashwa pengine nyumba tano, kumi lakini unakuta upelekaji ule wa kuingiza umeme kwa shilingi 27,000 unasuasua. Yawezekana wakandarasi hawakulipwa ama pengine usimamizi siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama inawezekana, tufanye tathmini ya wale tuliowapa kazi mradi huu wa kupeleka umeme kwenye vijiji, kupeleka umeme kwenye vitongoji, kupeleka umeme wa ujazilishaji umeleta tija kwa kiasi gani katika mafanikio yaliyotarajiwa? Hii itasaidia walau wale wote wanaotarajia kupata umeme na wale ambao wamepewa hiyo miradi watekeleze miradi kwa wakati, lakini kwa manufaa ambayo yametarajiwa kwa lengo kuu la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutake tusitake, taasisi nyingi bado zinahitaji umeme. Shule za sekondari, shule za msingi, tuseme sekta ya elimu kwa maana ya taasisi za elimu, makanisa na maeneo mengine ya huduma katika maeneo mbalimbali watu wanaotegemea visima vya maji, kwa maana ya visima vilivyochimbwa, zahanati pamoja na maeneo mengine ambayo kwa namna moja au nyingine wananchi wanapokea huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, tathmini ikifanyika, yale yasiingizwe kwenye vitongoji; yaingizwe kama mradi kabambe wa kuingiza taasisi hizo kupata umeme na kwenye mradi wa uhakika, kwa sababu taasisi hizo zinaweza kuwa za mashine za kusaga, uzalishaji ni mkubwa, unaweza kuleta tija kwenye mapato pia na unaweza kuwa ni huduma nzuri kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba, mara nyingi wale wakandarasi wakija wanakuta vitongoji tulivyoomba tayari vimeguswa na umeme, nasi tulishapendekeza. Sasa nashauri kwamba kama inawezekana, maombi ya Wabunge na maoni ya Wabunge yasikilizwe. Je, kwa kuwa kitongoji chako hiki tayari kina umeme, mradi wake ni wa ujazilizi, huu mradi ambao ni wa kufikisha umeme kwenye kitongoji, tunaomba maoni yako ili walau kitongoji gani sasa kwa maoni yako kina tija na sisi tukienda

tutatambua ili kuona majengo yaliyo pamoja na maeneo ambayo yana tija kama nchi, hii itasaidia sana katika kuleta tija na manufaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la mwisho ni kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu najua amebanwa sana, ana kazi nyingi. Aliahidi kwenda Mbulu, lakini haikuwezekana, yote heri kwa Mwenyezi Mungu. Pia kuja kwake kunahitaji nini? Kunahitaji sana sana kusaidia yale maeneo ambayo kwa sasa yaahitaji umeme kwenye vijiji kama Aicho, Gidamba, Hasama, Boboa na Gedamar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaya zilizofungwa umeme ni kaya nane, Mheshimiwa Waziri awaelekeze watendaji wa *TANESCO* kupitia *REA* waende kwa wananchi, waseme tunahitaji kaya 40 na kaya tunazohitaji ni hizi hapa. Kwa jiografia ya nguzo zetu ili ninyi mfanye *wiring* na tuweze kuwaunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangaliana tu, muda wa mradi unakwisha, umeme umepelekwa kwenye kaya kumi, ishirini badala ya arobaini, tija ile ya kusema kilomita moja kutoka *center* ya kijiji tunaikosa. Nadhani kazi kubwa imefanyika, tunawapongeza sana na pia bado mahitaji ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni umeme ule usio wa waya. Zamani mlikuja na UMETA, sasa hivi sijui mmebatiza jina gani? Najua kuna nyumba ambazo hatutaweza kufikia, kwa sababu unaweza kukuta nyumba ya mwananchi pengine ni nguzo kumi zinahitajika kwenda kwenye nyumba moja, kumbe yule anahitaji umeme wa taa, anahitaji umeme wa kuchaji simu, anahitaji umeme wa matumizi madogo madogo, lakini yule tukifunga hicho chombo ambacho akihitaji waya atatumia kwa muda, akalipia kama bili ya mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana kupunguza baadhi ya maeneo na baadhi ya kelele, lakini kwa namna ambavyo yeye tunajua hataweza kufikiwa, kwa sababu hizo nguzo kumi mjini inaweza kuwa nguzo arobaini katika eneo hilo. Hizo nguzo arobaini katika eneo hilo kwa namna ya pekee

ingeweza ku-*cover* hizo nyumba na wakazalisha haraka kuliko tukaenda kwa mwananchi mmoja ambaye atahitaji nguzo kumi na yeye yuko mmoja na matumizi yake ni madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu huu niendelee kuipongeza Serikali, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul. Hawa watachangia dakika zisizozidi sita kila mmoja.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara yetu hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliyetujalia uzima na kufika katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasema moyo usiokuwa na shukrani hukausha mema yote. Nianze kwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kubwa iliyotukuka anayotufanyia Watanzania. Kila Mtanzania anaelewa na ameona kazi anazofanya Mheshimiwa Rais, ndiyo maana katika sekta hii ya nishati amefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Kaka yangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara hii ya Nishati. Pamoja na hilo, nampongeza pia Naibu Waziri, mdogo wangu Judith Kapinga, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu wote, Wakuu wa Taasisi na wote ambao wapo katika Wizara hii ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kuchangia mchango wangu pasipo kuwasahau *Engineer* Habibu ambaye ni Meneja wa Wilaya wa *TANESCO,* Wilaya ya Rungwe, anafanya

kazi nzuri sana pamoja na *Eng.* Sabaya ambaye ni Meneja wa Mkoa wa *TANESCO,* anafanya kazi nzuri sana kule Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie katika mchango wangu kwa ajili ya kuishauri Wizara. Jambo la kwanza, wenzangu wengi Waheshimiwa Wabunge pia naungana na Kamati kushauri juu ya kuimarisha zaidi gridi imara pamoja na miundombinu ya kusambazia umeme, kwa sababu hivi sasa tuna umeme wa ziada zaidi ya megawati 4,000, lakini namna ya kuwafikia watumiaji ndiyo changamoto. Kwa hiyo, Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi naiomba iendelee kuongeza kasi katika kusambaza umeme na kuiboresha miundombinu hii ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano rahisi, ukienda kule Jimboni kwangu Busokelo, kule tunapata mvua mwaka mzima, takribani miezi 10 mpaka 11. Kwa miezi miwili tu ndiyo tunakuwa hatuna mvua. Sasa ukipeleka nguzo za kawaida ambazo ni za mbao, tafsiri yake ni kwamba, zinaoza haraka. Kwa hiyo, tunatamani sana maeneo haya na maeneo mengine yote oevu katika nchi hii ya Tanzania wasambaze miundombinu ya nguzo za zege. Najua *TANESCO* wameshaanza kufanya kazi hii, lakini waongeze kasi iwe kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kushauri huu mradi wa Rumakali ambao utazalisha megawati 222 wenye thamani ya trilioni 1,058. Mradi huu ni wa muda mrefu, lakini mradi huu utakuwa na manufaa makubwa sana kwa nchi yetu, na ni mradi ambao unapatikana katika Mikoa miwili ya Mbeya na Njombe, hususan katika Wilaya ya Makete na Halmashauri ya Busokelo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu kule waliambiwa kulipwa fidia tangu miaka ya 2018/2019 takribani shilingi bilioni 264 kwamba, wasiendeleze maeneo yao kwa sababu itapita gridi kubwa ya umeme. Naiomba Serikali yangu kwamba, wananchi hawa wameendelea kusubiri fidia hizi katika Kata za Lufilyo, Itete, Lwangwa, Isange, Mpombo, Kandete. Fidia hii wangelipwa

mapema ingesaidia sana ili waanze maisha mapya maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ni Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)*. Najua mnafanya kazi nzuri sana, lakini kwa bahati mbaya sana katika vile vitongoji 15 kwa Mikoa miwili ya Mbeya na Tanga wakandarasi wale hawakupatikana kwa wakati. Hivi ninavyosema, nimeambiwa kwamba, wiki iliyopita ndiyo amesaini vile vitongoji 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba *REA* wasimamie vizuri hawa wakandarasi ili waanze kazi hii kwa sababu wananchi tulishawaaminisha muda mrefu, na vitongoji hivi 15 na vilikuwa *budgeted* miaka miwili mfululizo. Kwa hiyo, naomba sana wenzetu wa *REA* jambo hili walisimamie kwa ukaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kushauri kwamba, hivi sasa mfumo ama sera ya Serikali upande wa kusambaza umeme inahitaji ulipie kwanza ndipo upate huduma. Naungana na Kamati kwamba, laiti kama tungekuwa na sera mpya ya kwamba Serikali ipeleke umeme kwanza kwa wananchi, halafu mwananchi yule ataendelea kulipa kidogo kidogo ili gharama zile ziweze kufidiwa wakati wa matumizi atakapokuwa ameunganishiwa umeme kwa maana tunaita *postpaid. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Serikali itakusanya fedha nyingi, pia huduma hii itakwenda kwa wananchi wengi. Huu ni ushauri wangu kwa Serikali na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri; ni msikivu sana, naamini hili atalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, kuna umeme huu wa joto ardhi ama jadidifu. Kule Jimboni kwangu Busokelo ni miongoni mwa maeneo ambayo Mungu ametubariki kuwa na umeme wa jotoardhi *(geothermal)*, tayari wenzetu kupitia kampuni tanzu ya *TANESCO* wameshachoronga visima kule na vinatoa maji yenye kasi kubwa sana. Sasa ombi langu kwa Wizara ni kwamba Wizara itenge fedha ili umeme huu uanze sasa kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka ni mwaka 2024 kulikuwa na kongamano kubwa sana la Afrika kwa masuala ya jotoardhi hapa nchini. Sisi tunajivunia kwamba tayari maeneo haya, visima hivi vimeshachorongwa, basi umeme uanze kusambazwa kwa maana ya umeme jadidifu hususan katika mradi huu Mbaka, Kyejo, na Mbambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, kuna hili jambo la vituo vya mafuta. Kumekuwa kuna vituo vingi sana vya mafuta ambavyo kila baada ya hatua kadhaa kuna kituo cha mafuta. Naomba Serikali yetu ione umuhimu wa kuweka usalama muhimu katika maeneo haya, kwa sababu hata ikitokea ajali unaweza kukuta jambo hili linakuwa hatari kwa wananchi wanaokaa maeneo hayo, zaidi pia na usalama wa wafanyakazi katika vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya bajeti ya Serikali kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Atupele. Nimwite sasa Mheshimiwa Pauline Gekul, naye aweze kutoa mchango wake.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa hizi dakika sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu pia kwa kutujalia afya njema ili tuendelee kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge, lakini ni kwa neema zake siyo kwamba sisi tunastahili sana, ni Mungu ametujalia nimshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nia yake njema ya kutaka kila Mtanzania afikiwe na umeme, ndiyo maana tunaona kwamba Bwawa la Mwalimu Nyerere sasa liko mbioni kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Yeye pamoja na Naibu Waziri mdogo wetu, Mheshimiwa Judith kwa kazi ambayo wamekuwa wakiwafanyia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia njema ya Mheshimiwa Rais inaonekana katika bajeti hii. Hii ni bajeti ambayo 95% ya bajeti wanayopewa inakwenda kwenye maendeleo, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Ni asilimia tano tu inaenda kwenye *OC* na mishahara na mambo mengine, lakini 95% ya *1.8 billion* ambayo hii wanatekeleza inaenda *1.5 billion* kwenye maendeleo. Ni nia njema kabisa ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nia njema ya Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu imeonekana katika bajeti hii, wameongeza tena shilingi bilioni 50 nyingine. Kwa hiyo, bajeti inaenda shilingi trilioni 2.2. zote. Ukiangalia, zaidi ya 90% inakwenda kutatua mahitaji ya Watanzania ya umeme. Nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Rais, wetu Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini vitongoji hivyo 32,000 ambavyo vimesalia na hivi ambavyo wanaendelea navyo vitongoji zaidi ya 900 kupitia *increment* hii, bajeti ya *50 billion plus* itakwenda kugusa vitongoji vingi, na Watanzania watafikiwa kwa umeme. Kwa hiyo, hii bajeti ni ya kuungwa mkono, ni bajeti ambayo inaenda kugusa maisha ya Watanzania, kwa sababu umeme umekuwa ni uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, ameliona hili na ndiyo maana bajeti yao imepanda, imeenda zaidi ya shilingi trilioni mbili. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kwa usikivu ule ule na busara zile zile kwako pamoja na Mheshimiwa Rais wetu, mwangalie gharama hizi za kuunganisha umeme. Tunawaomba, lengo ni jema kabisa,

mnapambana, lakini kwenye vijiji mtu ambaye hazidi mita 30 anaunganishiwa kwa shilingi 27,000; ambaye anazidi mita 70 toka miundombinu ya umeme ulikofikia, anaunganishiwa kwa shilingi 515,000, lakini mita 120 ni shilingi 696,000.666.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi wale wa mijini, kama mimi natokea Jimbo la Mjini, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, anaunganishiwa kwa takribani shilingi 320,000. Nawaomba m-*synchronise,* mwangalie hizi gharama za kuunganisha kwa sababu, miji midogo kama Babati, kama Mbulu, kaka yangu Mheshimiwa Issaay amesema na maeneo mengine, ile miji haitofautiani na vijiji na hata huko kwenye vijiji, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wetu, Doto Biteko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona kwamba, gharama hizi zimetofautiana, lengo ni jema. Mmeongeza bajeti, basi tunaomba Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri waangalie jicho la kiruzuku katika maeneo hayo, ili gharama za kuunganisha zisilalamikiwe, ili uweze kugusa watu wengi, kwa sababu, Mtanzania wa kawaida aliyeko kitongojini akilipa hizi shilingi laki sita, tayari anakuwa ameishiwa nguvu. Nia yenu ni njema kabisa, nia ya Serikali ni njema, kwenye gharama za kuunganisha mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala zima la miradi ya ujazilizi. Naipongeza Serikali, jambo hili linaenda vizuri. Kwa sisi ambao tunaongoza majimbo ya mijini, wakiona nguzo imevuka imeenda kijijini halafu yeye anaomba pale nguzo moja, nguzo mbili, tatu, anakata tamaa na tumekuwa tukiwatia moyo. Nampongeza Meneja wetu wa Mkoa wa Manyara, amekuwa akitupa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu atuongezee fedha kwa ajili ya umeme jazilizi. Mimi nakaa pale mjini, utakuta mtu anakaa *Oysterbay*, au Ngarenaro, nguzo mbili, tatu, hawezi kuzipata, anaomba, anatembea mpaka anakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamefanya *wiring* tangu mwaka 2019. Nimekuwa nikiwasiliana na ofisi ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, nimekuwa nikipewa sana ushirikiano, tangu 2019 mtu kafanya *wiring,* anaomba pale *TANESCO, TANESCO* wanakwambia bado hatujapata fedha. Naiomba Wizara ya Fedha waweze kufanya *disbursement* ya hizi bilioni, bajeti yao ilikuwa ni *1.5 trillion*, lakini imetolewa *one trillion* kwenye bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ile 59% ambayo imetolewa, *it is okay,* zile zilizobaki waweze kutoa sasa Wizara ya Fedha. Kwa sababu, *disbursement* yao imekuwa ni 59%. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ikimpendeza, basi bajeti yake hii iweze kutolewa kwa asilimia zote. Naamini na kwenye umeme jazilizi watakuwa wamefikiwa baada ya 59%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vitongoji hivi 15 katika kila Jimbo, napongeza sana, kazi inafanyika na Mameneja wa *TANESCO* na Ma-*engineer* wa *REA* wako *site*. Kwetu Babati wamefika, wameanza kazi, nawapongeze sana. Ombi langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kwa vile vitongoji ambavyo vipo mbali na miundombinu ya umeme, kama ambavyo *TANESCO* wametuelekeza, sasa wasogeze umeme pale, ili yule mtu wa *REA* asiache vile vitongoji 15 kwa kila jimbo kwa sababu, tulishawatangazia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila sasa *line* kubwa ya umeme ikiwa iko mbali, basi tunaomba Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, wenzetu wa *TANESCO* waweze kusogeza hizo *line,* ili hivyo vitongoji 15 ambavyo kazi ilikuwa inatakiwa ianze, viendelee na kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la tatu, kwenye taasisi, nimeona hapa ni kipaumbele katika bajeti, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ikiwapendeza wenzetu wa mamlaka za maji waangalie gharama zao zile ambazo wanalipa kwa *TANESCO,* kwa sababu, nitolee mfano Mji wangu wa Babati; visima vyote

vimezunguka Ziwa Babati na ule mji umekaa kama bakuli. Maji tunatoa huku bondeni tunayapandisha kwa umeme.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba pia, mawasiliano ya karibu ya *TANESCO* kupitia bili za maji na *units* ambazo mamlaka za maji nchini wanatakiwa kulipa, ili waweze kutoa hizo huduma, itasaidia kupunguza bili za maji kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nilitamani kusema ni hii mitungi ya gesi, ambayo tumepatiwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mkoa wetu wa Manyara bado tunaomba tupatiwe ile mitungi ya gesi ya ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi ambayo anafanya. Vinginevyo, nawatakia kila heri na hii bajeti tunaiunga mkono ili kazi iendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha, lakini kuna wenzetu wawili wana dharura kidogo, kwa hiyo, nimewaruhusu wachangie kwa dakika zisizozidi sita sita. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Francis Mtinga na wa mwisho kabisa atakuwa Mheshimiwa Regina Ndege. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi dakika sita za nyongeza ili niweze kuchangia. Naamini kwa mambo makubwa mawili tu, ambayo nilitaka kuyasema zitanitosha kufikisha ujumbe kwa niaba ya wananchi wa Tanzania na hasa wananchi wa Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongelea vitu viwili tu. Nitaongelea suala la *access* na *connection, access* ya umeme

vijijini na *connection* kwa wananchi, na pia nitaongelea suala la *tariff* ya D1 na T1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *access,* nchi yetu imetumia fedha nyingi sana bila kujali inapeleka wapi umeme? Kwa mfano, Serikali imepeleka umeme kijiji cha zaidi ya kilomita labda 100 bila kujali kwenye kijiji kile inakopeleka umeme kuna nyumba ngapi na watu wangapi watapa umeme? Suala lake lilikuwa tu ni kufikisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa fedha hizi nyingi ambazo zimetumika, lile lengo hasa la kutaka wananchi wapate umeme linahusiana na suala la *connection*. Serikali imefanya jambo hili zito la kufikisha umeme vijiji takribani 12,000 vya nchi hii, umeme umeshafika kijijini au kwenye mji, lakini wananchi wanautazama kwa macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa inayochangia ni suala zima la bei za ku-*connect* umeme. Iko miji midogo midogo, mfano katika Jimbo langu, pale Iguguno na miji mingine ya Nduguti, umeme anaambiwa achangie shilingi 352,000 ili aweze kuvuta umeme wakati Serikali imetumia fedha nyingi sana kuufikisha ule umeme pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba, yako mambo mawili makubwa ambayo yanaweza yakafanyika katika kuhakikisha kwamba, hii *access* ambayo tumeifanya kubwa katika nchi hii ya kufikisha umeme kwenye vijiji, basi iendane na *connections* kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu ni bingwa wa ruzuku na ninaamini mwezi wa Kumi wananchi wa Tanzania wanakwenda kupigia kura hizi ruzuku kubwa kubwa. Kuna ruzuku kwenye mbolea, mabilioni; kuna ruzuku kwenye viuatilifu vya dawa na mimea, mabilioni; na sasa ruzuku mpaka kwenye gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jana tumefungua *Coop Bank,* Rais ametoa fedha pale kuhakikisha kwamba, hii benki ya ushirika inaenda. Kwa hiyo, namwomba Rais huyu bingwa, mpenda watu

wake, aangalie tena suala la ruzuku katika hili suala la *connection,* ili wananchi waweze kupata umeme kwa bei ya shilingi 27,000 nchi nzima bila kujali mjini, vijijini au miji midogo kwa sababu, fedha aliyotumia kufikisha umeme vijijini ni kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ruzuku ikitizamwa pia kwenye *connection* itakuwa ni jambo jema kabisa ili wananchi wapate umeme. Hiyo ni kwa upande wa Rais, lakini na Shirika lenyewe la *TANESCO*, linayo namna ya kuwafanya wananchi wafanye *connection*. Shirika linakopesheka, linaweza kutafuta fedha mahali popote wakapeleka *connection* kwa wananchi wote wa Tanzania ambao wanataka umeme. Halafu inapoanza matumizi, kwenye zile *tariff,* wakamwekea mwananchi kiwango kidogo kidogo akawa analipa kila mwezi kwa kulipa ile shilingi 352,000 kama wanayoitafuta, wala hata-*feel.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *TANESCO* wanafanya kazi ya kukusanya ushuru wa *property tax,* tena wanawakusanyia tu watu wengine, siyo zao. Sembuse wakiwafanyia wananchi, wakawa-*connect* na umeme, halafu matumizi wakawawekea pesa kidogo kidogo wakawa wanarudisha ile fedha ya *connection!* Watashindwaje kukusanya pesa yao kama leo wanamkusanyia mtu mwingine pesa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Shirika la *TANESCO*, kwa sababu ruzuku zimezidi, kama itashindikana kwenye ruzuku, basi Shirika lifanye utaratibu wa kuwa-*connect* watu kwa umeme *then* anapoanza matumizi, kwa mfano wale wa D1 ni shilingi elfu tisa sijui na mia ngapi? Akiongezewa pale labda shilingi 5,000 au shilingi 6,000 kila anaponunua umeme mpaka atakapomaliza deni lake, wala hatakuli-*feel* hawezi. Kwa hiyo, naomba sana hii *access* ya umeme iliyokwenda vijijini iungane na *connection*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme sasa ni jambo la nne katika mambo muhimu ya anayohitaji mwananchi. Mwananchi anahitaji chakula, mavazi, malazi, lakini sasa la nne ni umeme. Zamani umeme ilikuwa ni anasa. Ukiona kwa mwenzako

unawake, unaona kawaida, hao ni matajiri bwana, lakini sasa hivi umeme ni suala la msingi, ni *basic* ya nne kwa maisha ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana mama, naiomba sana *TANESCO;* Mheshimiwa Waziri ni mtu wa Mungu, ni mchapakazi, ni mtu rahimu, akisimama tu kuongea, watu wanajua sasa yanashuka madini. Hili la kuisimamia *TANESCO* iunge umeme kwa watu, halafu iwa-*charge* kwenye matumizi, linawezekana, liko ndani ya uwezo wake, naomba sana aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilisema nitaongelea suala la *tariff* D1 na T2. Sheria inasema mwananchi wa kijijini akiunganishiwa umeme *direct,* ataunganishwa kwenye D1 na mwananchi wa mjini *direct* ataunganishwa kwenye T1, lakini ikaja Sheria ya *Amendment* ya *GN* ya Mwaka 2016, ikafanyiwa *amendment* Mwaka 2020, ikaongezwa kipengele kwamba, kila mwananchi ambaye anatumia umeme usiozidi *kilowatts* 75 achajiwe kwa D1. Kwa hiyo, bila kujali ni wa mjini au ni wa vijijini, ila kama atatumia *kilowatts* zisizozidi 75 *per month* achajiwe kwa *tariff* ya D1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa taratibu wananchi wa mjini wanaondolewa kwenye hii D1. Ukipiga simu *TANESCO* ukiuliza wanakwambia hii inawahusu wananchi wa vijijini, lakini hii Sheria ya *Amendment* wanaisahau. Kwa hiyo, naomba sana kama mwananchi anaweza kujibana akatumia *tariff* siyo chini ya *kilowatts* 75 kwa mwezi basi achajiwe kwa D1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii dhana kwamba, wananchi wa mjini ni matajiri tuiondoe. Mjini ndiyo kuna watu wana shida kweli kweli. Wapo wajasiriamali wamepanga kwenye chumba kimoja kimoja na bili ya umeme wanajilipia, siyo kwamba, analipa *landlord*. Kwa hiyo, wanaweza kujibana wakatumia umeme chini ya *kilowatts* 75 kwa mwezi, wasiondolewe kwenye hiki kitu ili waweze kuufaidi huu umeme ambao nchi yetu imeutafuta, ili wananchi waweze kuutumia. Naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa muda wako, lakini haya mambo mawili naamini yamefika na yamesikilizwa, na Wabunge ndiyo wamesema mengi sana. Ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja nikiamini kwamba, hili linakwenda kuwagusa Watanzania na litafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtinga, ahsante sana kwa mchango mzuri kabisa. Nikuite sasa Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani amekuwa mfano wa kuigwa, ni mama jasiri ambaye amewatumikia Watanzania bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, msaidizi wake, Naibu Waziri, Mheshimiwa Judith Kapinga pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Nishati kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba, hii Sekta ya Nishati inakwenda kusonga mbele. Niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya dhati kabisa kuhakikisha Watanzania wanakwenda kuondokana na matumizi ya nishati chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa kinara katika Afrika kuhakikisha kwamba, Watanzania wanatoka kwenye matumizi ya nishati chafu na kwenda kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kwa kufanya hivyo, amekwenda kuokoa maisha ya Watanzania walio wengi, hasa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu kwamba, wanawake wengi maeneo ya vijijini wamekuwa wakitumia kuni katika kupikia, lakini wanawake wa mijini wamekuwa wakitumia mkaa. Haya yote yanasababisha uharibifu sana wa mazingira, lakini siyo hilo tu pia, wanawake wengi wamekuwa waathirika wakubwa katika afya kwa sababu ya matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumshukuru sana na sisi, kama wanawake na Watanzania wote, tukamuunge Mheshimiwa Rais kuhakikisha ajenda yake ya Nishati Safi ya Kupikia inakwenda kutimia kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameanza kuelewa matumizi sahihi ya nishati safi ya kupikia na tayari imeanza kufika mpaka maeneo ya vijijini. Sisi Wabunge, kama wawakilishi wa wananchi tumekwenda kugawa nishati kwa wananchi, hasa katika makundi maalum, lakini bado kuna changamoto, tunaomba Serikali iende kuongeza kasi katika kuhakikisha nishati safi ya kupikia inapatikana katika mazingira ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi ambao wana mwitikio na wameelewa matumizi ya nishati safi ya kupikia, lakini changamoto ni upatikanaji. Mtu ananunua mtungi wa gesi kituo cha kubadilishia mtungi wa gesi, anatumia gharama kubwa kuliko gharama ya kwenda kubadilisha gesi. Kwa hiyo, naomba sana mawakala wetu wasogeze huduma karibu na wananchi, ili wananchi waweze kupata huduma ya kubadilisha gesi kwa wepesi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Serikali kwa kuongeza kasi kuhakikisha kwamba, vijiji vyote vimekwenda kupata umeme na sasa hivi Serikali ina mpango wa kuelekea kwenye vitongoji na tayari kazi imeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna vijiji vyenye sura ya miji, bado gharama ya kuunganisha umeme imekuwa kubwa. Mfano, Mkoa wangu wa Manyara tuna Kijiji cha Magugu, kuna Kijiji cha Matui, bado gharama iko juu sana, badala ya shilingi 27,000 leo wananchi wanaunganishiwa umeme kwa shilingi 320,000. Ukiona hivyo, ujue kasi ya kuunganisha umeme kwa wananchi imekuwa ndogo ni kwa sababu, wananchi wanashindwa kufikia gharama zile za kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, dhamira ya Rais ni kuhakikisha kila Mtanzania anakwenda kupata umeme, naomba sasa Serikali iweke mkakati kuhakikisha vile vijiji vyenye sura ya miji

umeme upungue gharama ili wananchi wote waweze kuunganishiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi ambao wana utayari wa kujiunga na umeme wa *three phase,* lakini wanashindwa kulingana na gharama. Naomba sasa, Serikali iweke mkakati wananchi hawa wapewe mikopo wanapokwenda kuunganisha umeme ili wakipewa mikopo hii watakuwa wanalipa taratibu, kadiri anavyonunua *units* za Luku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama amenunua *units* za shilingi laki moja, yule mwananchi apewe nusu, ili nusu ilipie deni la *TANESCO*. Hii itasaidia wananchi wengi kuendelea na umeme, kujiunga na hiyo nishati safi ya umeme, lakini pia, itasaidia kwenda kuibua viwanda vyetu kuzalisha kwa wingi. Hii ni kwa sababu, gharama itapungua, lakini wananchi wengi watajiunga kwa gharama ambayo akijiunga kwa bei ya mkopo, gharama ya ulipaji haitakuwa na maumivu makali kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi, kama Babati, tuna kituo kile cha kupozea umeme, *substation*. Kituo hiki toka kimeanza kutumika mpaka leo matumizi yake yako chini ya 50%. Hii ni hasara kwa Shirika. Shirika liangalie namna ambayo inaweza ikapunguza bei ya *unit,* ili wananchi waweze kuunganisha umeme kwa wepesi kwa sababu, gharama inapokuwa kubwa, ile *substation* pale uzalishaji wake ni mkubwa, lakini matumizi yanakuwa chini ya kiwango, maana yake, inazalisha chini ya 50%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la umeme wa kupikia katika maeneo yetu ya vijijini. Ili kuendelea kulinda afya ya Mtanzania ni lazima kila mwananchi atoke kwenye matumizi ya nishati chafu kwenda nishati safi ya kupikia, lakini changamoto kubwa tunayoipata kwa sasa, tunaomba Serikali, kwa kuwa, imeshaleta ruzuku kwenye mitungi ya gesi, iongeze ruzuku kwa sababu, bado wananchi wengi wana uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya upatikanaji ni kubwa, kwa hiyo, ikiendelea kuongeza ruzuku; kwanza nishukuru kwa

sababu ruzuku imewekwa, lakini bado tunahitaji iongeze zaidi, ili wananchi waende kutumia gesi safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba sana ipunguze gharama za *unit* ya umeme ili wananchi waweze kutoka kwenye matumizi ya kuni na kupikia majiko ya umeme katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, naona umewasha taa, lakini niseme kwamba, naiunga mkono bajeti. Nawatakia kila la heri Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, sisi tunaendelea kuwaunga mkono ili dhamira ya Mheshimiwa Rais iende kutimia kwa 100%, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu hiki cha michango. Tutakaporejea tutaanza na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, atafuatia Mheshimiwa Kavejuru Felix, atakuja Mheshimiwa Leah Komanya na tutaendelea kutangaza kadiri tutakavyoendelea.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaondoka, ndani ya ukumbi wetu wa Bunge tulikuwa na Wageni ambao walikuwa wanatuangalia na kujifunza. Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wa kwanza kabisa ni mgeni wa Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Twaha Ally Mpembwene, Mbunge wa Kibiti. Huyu ni Ndugu Yusuph Mbinda, ambaye ni Diwani Kata ya Dimani, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Mkoa wa Pwani. Karibu sana Mheshimiwa Diwani. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 50 wa Waheshimiwa wawili, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu. Hawa ni viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika kutoka Tunduru, Mkoani Ruvuma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 12 wa Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge mwenzetu. Hawa ni viongozi wa Halmashauri

ya Chama cha Ushirika, *MAMCU* na *AMCOS,* kutoka Masasi Mjini, Mkoani Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 75 wa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge. Hawa ni Wakuu wa Shule za Sekondari, Babati Mjini na Walimu wa Sekondari Bagala kutoka Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 21 ni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, hii ni Kwaya ya Yesu Mwema ya Kanisa la Anglikana kutoka Bahi, Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kuna Ndugu Good Chansi Mbise, huyu ni Katibu Mwenezi wa CCM, Kata ya Imbasenyi, Meru, Mkoani Arusha. Karibu sana, yuko pale. *(Makofi)*

Tuna viongozi 42 wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 40 wa Chuo cha Serikali za Mitaa, Kampasi ya Dodoma Mjini, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni leo.

*(Saa 7.18 Mchana, Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata fursa hii ya kuchangia hii Bajeti yetu ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii kupata fursa ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo anazifanya na kuhakikisha kwamba, anamwaga fedha nyingi katika miradi mingi mikubwa ya maendeleo katika nchi yetu, miradi ambayo ni kielelezo cha kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza na kumshukuru Rais Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kwa kazi kubwa anayoifanya Zanzibar kwa ajili ya kutekeleza miradi mingi mikubwa ya maendeleo ambayo inaenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, lazima nimpongeze na kwa kishindo kikubwa sana ndugu yangu Dkt. Doto Biteko, naye kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba, anamsaidia Rais katika majukumu aliyompatia na lile la Wizara ya Nishati ambapo

tunaona hasa kule Zanzibar nishati ya umeme na gesi *imetindimaa*. Kadhalika sitaweza kumsahahu Naibu Waziri wake Mheshimiwa Judith Kapinga naye kwa kazi kubwa ambayo anamsaidia Mheshimiwa Doto Biteko kadhalika na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili la nishati sitaweza kumsahau Mheshimiwa Shaib Hassan Kaduara, Waziri anayeshughulikia nishati kwa upande wa kule Zanzibar. Pia, sitakusahau wewe Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa ambayo unaifanya wakati ukiwa ni Spika wa nane wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini ukiwa Spika wa Pili Mwanamke. Hiyo kama haitoshi, ukiwa Spika wa Pili wa Mabunge ya Dunia, kwa kweli na wewe unahitaji pongezi zako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tuseme unatuendesha vizuri na unatuongoza vizuri. Wakati mwingine wapo ambao kidogo wanataka kupotea, lakini busara inakutawala na unatuendesha ukiwa kama mama, kwamba huwezi kukubali mtoto wako apotee. Hili kwa kweli tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia matukio mengi hapa, unajua kabisa kwamba huyu hapa anakwenda vibaya, lakini kama mama unasimama unaona hapa acha nimweke sawa Mheshimiwa ili mambo yaende vizuri. Kwa hiyo, kwa jambo hili, ni lazima tukupongeze, na tukushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeanza na Mheshimiwa Rais, kwa nini? Rais huyu Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba miradi yote mikubwa na ya kimkakati anaikamilisha kama ambavyo mtangulizi wake Mheshimiwa Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli aliiacha. Tunapozungumzia Bwawa la Mwalimu Nyerere, kama zilivyo hadidu huko kwamba lilikuwa na 18% au 20% lakini sasa limefika asilimia kubwa. Jambo ambalo hata kwa upande wa Zanzibar umeme huu sasa *umetindimaa* vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunapata mgao wa umeme kwa sababu ya upungufu wa umeme ambao tumeunganishwa nao

kutoka gridi za Taifa. Kwa mfano, kama Kisiwa cha Pemba kimeunganishwa kutoka Majani Mapana Tanga hadi Ndagoni Wesha, ambapo umeme huo unatusaidia sisi wananchi wa Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba umeme huo ndiyo ambao kwa upande wa jimbo langu umemaliza vijiji vyote kuungwa baada ya ule umeme wa mwanzo, ambapo tulikuwa tunatumia vinu vya majenereta kwa ajili ya kupata umeme ule. Tunamshukuru na tunampongeza sana kwa jitihada zake Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko za kuhakikisha kwamba nishati ya umeme Kisiwani Pemba *inatindimaa*.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili lazima tuseme, kuna kitu kimoja ambacho kinahitaji kipatiwe marekebisho kidogo. Umeme unaotoka Tanga kwenda Pemba kuna kituo pale Majani Mapana ambacho ndicho ambacho kinasoma *units* zote ambazo zinapelekwa Pemba. Sasa, kwa sababu ya usafirishaji wa mkondo huu mkubwa wa *Kv* 33 ambazo zinasafiri ndani yake, kuna umeme unapotea.

Mheshimiwa Spika, umeme huu unaopotea unapopokelewa katika Kituo cha Ndagoni kule Pemba, unapokelewa ukiwa tayari kuna asilimia kadhaa za umeme ambao umepotea, lakini, hesabu pale zinachukuliwa hizi za huku Majani Mapana jambo ambalo kidogo linaathiri kule kwa wenzetu *TANESCO,* kwamba wanalipa umeme ambao unapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Biteko, na kwa heshima sana hesabu za umeme kwa maana ya *units* zinazopokelewa kule Ndagoni Wesha pemba ndizo hizo ziingie kwa *ZECO* ili yale mahusiano yaendelee kwenda vizuri. Sisi kama Wabunge tunafahamu sana kwamba kuna mahusiano makubwa sana kati ya *ZECO* na *TANESCO*, na kati ya Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Maji, Nishati ya kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tunaona katika *forum* mbalimbali viongozi wa Wizara ya Nishati Zanzibar wakishiriki kwenye

makongamano na shughuli mbalimbali zinazotayarishwa na Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kadhalika *ZECO,* kwa maana ya viongozi, nao tunawaona wakishikiri katika makongamano, mambo na shughuli mbalimbali za kiufundi na za kiuongozi kwa wenzao wa *TANESCO*. Jambo hili linaleta faraja kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia, Wizara ya Nishati siyo Wizara ambayo ni ya kimuungano, lakini tunaona mahusiano yaliyopo, hata safari za nje wanatoka Zanzibar wakiambatana na wenzao wa Wizara ya Nishati ya huku wakienda kule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunashukuru sana kwa jitihada hizi ambazo Mheshimiwa Dkt. Biteko anazichukua, za kuhakikisha kwamba mahusiano ya hizi Wizara mbili yanakuwepo kwa sababu ndani yake kuna jambo muhimu sana la nishati ya umeme ambapo umeme ndiyo maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika kwa upande wa Zanzibar tulipokea majiko ya gesi zaidi ya 10,000 ambayo yanatumiwa na wajasiriamali, akina baba na akina mama. Tunajua Mheshimiwa Rais hapa alifanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba kila Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kila mwakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar anapata majiko 100. Ndiyo maana kwa upande wa Zanzibar majimbo 50 tunasema kwamba zaidi ya majiko 10,000 yalitolewa. Majiko haya yamewasaidia sana wajasiriamali akina baba na akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ni lazima tukumbushane au tuombe jambo hapa. Hili suala la bei ya ku-*refill* ile gesi, hapa ni lazima kuwe na bei elekezi. Hii ni kwa sababu tumegawanyika katika maeneo mbalimbali. Utaikuta ile chupa ambayo tulipatiwa wenzetu wengine wanainunua kwa shilingi 22,000/=, wengine shilingi 23,000/=, lakini maeneo mengine inafika mpaka shilingi 32,000/=. Sasa, hili siyo jambo zuri sana kwa wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba, kama yalivyo mafuta kwa bei elekezi kwa kupitia *EWURA* na kule Zanzibar mafuta kwa kupitia *ZURA*, kwamba kuna bei zinatolewa, hizo ndizo bei elekezi. Haya majiko, kwa maana ya kwenye hii gesi ni lazima kuwe na bei elekezi, kwa haya majiko. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, Maana yake ni kwamba, zile chupa ambazo zimetolewa kwa nia safi na Mheshimiwa Rais kupitia Mheshimiwa Waziri zitumike, na siyo baada ya kutumika hizi chupa ziendelee kubaki ndani ya nyumba bila kutumia. Lazima hapa kuwe na bei elekezi ili wananchi waweze kujaza gesi na kuendelea kutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali za wananchi zimeboreka, na mazingira yameboreka kupitia gesi hii. Kwa hiyo, ni lazima jambo hili tulifanyie kazi vizuri ili tuweze kuweka ustawi mzuri wa bei hizi za hii nishati ya gesi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, najua sasa hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuna mchakato wa kuongeza *cable* nyingine ya kutoka Tanga kwenda Pemba kwa sababu ile iliyopo, uwezo wake ni mdogo kwa sasa, kwa sababu ya maendelo makubwa ambayo ameyaleta Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Zanzibar kuna viwanda vingi, hasa Pemba, kuna viwanda vingi na majengo mengi makubwa yameongezeka. Sasa ile *cable* iliyopo inayobeba mawimbi ya *Kv* 33 haitoshelezi tena. Kwa hiyo, wapo na mkakati huo, tunaomba pale ambapo watakuwa wamekwama, basi tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda, naomba kuunga mkono hoja hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipatia fursa hii kuwa mchangiaji wa pili jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Nchi kwa baraka zake anazotujaalia kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nakushukuru kwa kutuongoza vyema, hongera sana. Vile vile nampongeza kwanza kabisa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu. Hongera sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pili ni ndugu yangu Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Mkuu na Waziri wa Nishati. Kazi kubwa ameifanya na inaonekana. Waswahili wanasema, wali wa kushiba huonekana kwenye sahani. Hakika matunda na matokeo ya kazi hii inaonekana hata kwa macho. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, pongezi za tatu zimfikie dada yangu Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, msikivu, mwerevu, mchapakazi, simu yake ipo wazi saa 24, ukim-*beep* ameshapiga, unatakaa nini? Ukimwelezea, tayari ameshaingia kukutatulia tatizo hilo. Ahsante sana na Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingine ziwaendee Watendaji Wakuu wa hii Wizara ya Nishati. Zifike kwa Mramba F. Joseph na Naibu wake James Peter Matarajio na Khatib Malimi Kazungu. Vilevile, niwapongeze watendaji wetu waliopo mikoani, nikianza na Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Kigoma Ndugu Julius Sabu pamoja na Meneja wa *TANESCO* Wilaya ya Buhigwe Ndugu Abdallah Khamis Mulamuzi kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kule Mkoani Kigoma. Tumepata miradi mingi, umeme unaendelea katika vitongoji. Sasa Mkoa wetu umeungwa kwenye gridi ya Taifa. Tunasema ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo haya nayo yamechangiwa na uundaji wako wa Kamati nzuri ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na

Madini. Nawapongeza; haya mafanikio tunayoyaona ni pamoja na mchango wao, wanakamati hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, nianze na kutoa ushauri. Tumepiga hatua, na tunaipongeza Serikali yetu kwa kukamilisha mradi mkubwa wa umeme hasa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tumefikisha megawati 4031.71. Hongereni sana. Ni kazi kubwa na ni mapinduzi makubwa sana. Tumeonesha tunao uwezo kwa sababu nia ilikuwepo na uwezo umeonekana na tumefika hapo tulipokuwa tunapatarajia.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hii ukiangalia kazi ambazo anaendelea kuzifanya Rais wetu kwa kila Wizara, ukianzia na hii Wizara ya Nishati, ukiangalia na shughuli zinazofanyika kwenye Wizara ya Kilimo, utaona hii nchi yetu inakwenda kufanya mapinduzi makubwa sana hususan kwenye kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, umeme ndiyo moyo wa viwanda. Tumeshuhudia Kigoma tu baada ya kuungwa kwenye gridi ya Taifa tayari tumepata viwanda vinne. Tumepata Kiwanda kikubwa cha Sukari, kinajengwa Kasulu. Pia tumepata tena kiwanda cha kuchakata mazao ya chikichi. Vilevile tuna kiwanda kitakachofunguliwa mwezi Mei cha kutengeneza *cement;* na tuna Kiwanda cha Magodoro. Haya ndiyo tuliyokuwa tukiyapigania na tuliyotamani kuyaona siku zote katika mkoa wetu. Bila umeme wa uhakika huwezi ukapata viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba hizi megawati 4031.71 tulizozipata hazitoshi. Ili tujenge uchumi wa viwanda hatuna budi kufanya juhudi kubwa zaidi kwa kujilinganisha na nchi ambazo zimepiga hatua. Nimejaribu kuangalia katika nchi zetu za ulimwengu wa tatu, nikianzia na Bara la Afrika. Nimejaribu kuiangalia Afrika Kusini ina-*produce* umeme umeme wa kiasi gani? Ina-*produce* umeme wa megawati 58,095, ni nchi ya pili.

Mheshimiwa Spika, nchi ya kwanza ni *Egypt*, ina umeme wa Megawati 59,442, na nchi ya tatu ni *Nigeria*. Ukiziangalia hizi nchi zimepiga hatua kimaendeleo kwa sababu wana umeme wa

kutosha na ndiyo ume-*stimulate*, umechechemua ukuaji wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuja kuangalia kwenye Afrika Mashariki na Kati, sasa hivi pongezi kubwa sana kwa Tanzania tunaongoza. Baada ya sisi, wanaofuatia kwenye Afrika Mashariki ni Kenya ambao wana Megawati 3,300, na nchi ya tatu ni *Congo DRC*, inazalisha umeme Megawati 2,819, lakini wanao upungufu, wana *deficit* ya umeme wa Megawati 1,036. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi Tanzania kama tutaongeza juhudi, na kwa sababu tuna vyanzo vingi ambavyo tunaweza tukaongeza tukazalisha, tayari tunaweza tukawauzia Wakongo na Warundi ambao wanazalisha umeme wa Megawati 39 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikaangalia nchi ambazo zina uchumi mkubwa katika dunia ya leo, ya kwanza yenye umeme mwingi ni China, ina Megawati bilioni 3.43; nchi ya pili ni *United States of America*, inazalisha umeme wa Megawati milioni 1.3; nchi ya tatu ni India, ambayo inazalisha umeme wa Megawati 470,448.

Mheshimiwa Spika, nikajaribu kuangalia vyanzo ambavyo vimezisaidia hizi nchi kupata huu umeme mwingi, sisi tunavyo. Mfano mzuri ni India, wananunua makaa ya mawe, ikiwa wananunua kutoka Tanzania na nchi nyingine. Hao wanazalisha umeme mwingi sana. Ukiangalia hizi nchi nyingine, kwa mfano Morocco, Ethiopia ambao wana-*produce* umeme wa Megawati 5,200 na wameweka *plan*, kati ya miaka 10 ijayo watafikia Megawati 17,000. Ukiangalia vyanzo walivyonavyo, sana sana ni maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunayo *biomass* ya kumwaga! Tunayo *natural gas*, *hydro*, *coal* ambayo ni makaa ya mawe ambayo tunayauza. Bado tuna *geothermal,* tuna *solar*, tuna upepo, na tuna *uranium*. Kwa hiyo, ni mpango tu wa maamuzi wa kupanga na kuweka mikakati ya pamoja. Endapo kutakuwa na *plan* ya kuongeza umeme ndani ya miaka 10 kwamba tuzalishe zaidi ya Megawati 10,000 kwa Tanzania, uwezo huo upo. Tukishazalisha

umeme mwingi tutakuwa tumetengeneza mazingira mazuri ya kuwavuta wawekezaji kuja kuwekeza kwenye nchi yetu, kwa sababu tayari tutakuwa na umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo tunatakiwa tushushe bei ya umeme ili viwanda vitakavyozalisha gharama yake iwe chini. Tukifanya hivyo, tutakuwa tume-*accelerate* mapinduzi makubwa kwenye viwanda vyetu, na kwenye kilimo ambacho tunazalisha. Badala ya kusafirisha malighafi nje, tutakuja kuwa na viwanda vingi ambavyo vitakuwa hapa nchini, na nchi yetu itakuwa imesonga mbele, na itakuwa imefikia lile lengo la kuwa na uchumi wa viwanda. Huo ndiyo ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili pamoja na shukrani kwa Mkoa wa Kigoma, kuna mradi wa kuzalisha umeme kutoka Mto Malagarasi Megawati 49.5. Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ongeza jitihada, umeme ule unahitajika kwa majirani kwa sababu tayari kuna *deficit* kwa majirani zetu wa *Congo DRC* na Burundi.

Mheshimiwa Spika, tukizipata zile Megawati 49 zikaingia kwenye gridi ya Taifa na ukijumlisha tena na *kilovolt* 400 ambazo tayari wameshatuunganishia kutoka Nyakanazi, tayari ziko Kigoma na wakakamilisha tena mradi mwingine wa ile *line* ya *kilovolt* 400 ambayo wanataka sasa kuitoa Sumbawanga na kuileta Mpanda na kuileta Kigoma, kwa hiyo, tutakuwa na ziada ya umeme mwingi na tutapata fursa ya kwenda kuwauzia majirani.

Mheshimiwa Spika, tutajenga uchumi wetu na tutakuwa tumetengeneza Kigoma kuwa *hub* na geti la kibiashara, lakini itakuwa ni *hub* ya kujenga viwanda ambavyo tayari viko karibu na masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana kwa umeme ambao unaendelea kwenye vitongoji, miradi yote ambayo iko kwenye vitongoji vya Wilaya ya Buhigwe. Wakandarasi wapo wanaendelea na kazi. Ahsante sana Naibu Waziri Mheshimiwa Judith, umeifanya kazi. Nimekuwa nikikusumbua, na kule kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa mwisho; juhudi na mpango wa kutengeneza na kujenga vituo vya kupozea umeme kwa kila wilaya ni jambo la maana na zuri ambalo litaokoa upotevu wa umeme. Itafutwe fedha ili kukamilisha miradi hiyo. Umeme unaokuwa umezalishwa, basi uweze kusafirishwa kwenda kwa wahitaji, kwa maana kila siku mahitaji ya umeme yanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, huu umeme ambao tumeupata, tumeufikia wa Megawati 4,000, ndani ya miaka mitatu, miaka minne, miaka mitano unaweza ukawa mdogo kwa sababu ule uhitaji wa viwanda vinavyoenda kujengwa na umeme unaokwenda sasa kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini pamoja na kwenye makazi ambapo kila Mtanzania ana kiu ya kupata umeme nyumbani, unaweza usitosheleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunahitaji kufanya mapinduzi na kufanya maamuzi, tena ya kijasiri ya kutumia sehemu zile ambazo *sources* ambazo hatujazi-*detect*, kwenye *uranium*, kwenye makaa ya mawe, hata kwenye jua, bado hatujazitumia. Kwa hiyo, tuwekeze zaidi ili tuzalishe umeme mkubwa utakaotengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa maoni yangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, toka walipoingia pale wametatua changamoto nyingi, lakini kubwa zaidi nawashukuru wao Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia sisi Wabunge wenzao, wamekuwa

wepesi wa kutusikiliza. Siyo kusikiliza tu, pamoja na kutatua changamoto zinazotukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa *slogan* yake ya kunena na kutenda. Amekuwa akiitekeleza vilivyo; anasikiliza pamoja na kutenda, haishii kusikiliza tu, baadaye mnaanza kupishana kwenye makorido na kutazamana pembeni. Nakupongeza sana Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu alipoingia madarakani, Jimbo la Meatu utekelezaji wa umeme katika vijiji ilikuwa ni 40%. Hivi tunavyoongea, toka mwaka 2024 umeme huo umesambazwa katika vijiji kwa 100%. Kata saba kati ya 16 ambazo tulipoingia madarakani zilikuwa hazijapata umeme, ikiwemo Kata ya Mwamanimba, Mwamalole, Mbushi, Mwabuzo, Mwamanonga, Imalamako, pamoja na Kabondo, sasa hivi wanawasha na wananchi wananufaika na umeme huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna siku tulikutana na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, tukatoa kero zetu. Mojawapo ya kero katika Jimbo la Meatu ilikuwa ni kukatikakatika kwa umeme ambako kulikuwa kunatokana na wilaya hii kuwa pembezoni.

Mheshimiwa Spika, sisi Wilaya ya Meatu tulikuwa mbali na kituo cha kupozea umeme kwa sababu kituo hiki kilikuwa kinapatikana Ibadakuli Shinyanga, na Mkoa wa Simiyu bado tulikuwa hatujapata kituo cha kupozea umeme. Nilipomtolea hii hoja Mheshimiwa Waziri alifanya utekelezaji mara moja. Tunachukua umeme kutoka katika Kituo cha Kupozea Umeme Singida, ambacho kinaingilia Mkalama mpaka Bukundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unafuu upo, pamoja na kukatikakatika kwa umeme, lakini kuna unafuu. Wakati mwingine Ibadakuli wanapofanya matengenezo tunawasha ule wa kutokea Singida. Inapotokea Singida kuna matatizo, tunawasha ule wa Ibadakuli, na wakati mwingine wote kwa pamoja unafanya kazi. Huu wa Singida unanufaisha Kata ya Bukundi, Kata

ya Mbushi, Kata ya Mwanjolo, na Vijiji vya Mwabagalu na Itaba, vilivyoko Kata vya Nkoma. Nashukuru sana sana kwa hatua aliyoichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa vitongoji 15 tulivyoipewa vya ujazilizi, ambavyo mkandarasi sasa anaendelea. Ameshaanza kusimika nguzo, ameshafikisha *transformer* pamoja na nyaya zinazotakiwa tayari kwa utekelezaji. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vitongozi 15 kwa jimbo, mkandarasi alikuwa ana changamoto za kimkataba. Zile changamoto zimeisha, sasa hivi ameanza kazi ya kuchimba mashimo kwa ajili ya kusambaza umeme huu. Tayari ameshaanza kusomba nguzo pamoja na *transformer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kushukuru sana kwa kazi nzuri zinazofanywa. Katika tenda iliyotolewa ya kutangaza kazi, sisi Jimbo la Meatu tutanufaika na vitongoji 55. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini nitoe ombi langu. Kipaumbele chetu katika Jimbo la Meatu, kwanza ni kufikia umeme katika taasisi za Serikali. Katika vile vitongoji 15 tulishindwa kufikisha katika taasisi za Serikali kutokana na kwamba hakukuwa na *line* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwenye hivi vitongoji 55 vilivyotangazwa kuwepo na *main line* ambayo itatusaidia ku-*supply* katika taasisi za Serikali, na hata sekta kubwa, vitongoji vikubwa vilivyochangamka ambavyo vilipitwa na umeme kutokana na kukosa *line* kubwa. Nafahamu, pamoja na changamoto tulizonazo, tunatekeleza mradi mkubwa wa kituo cha kupozea umeme katika Mkoa wetu wa Simiyu, kilichopo Imalilo, Wilaya ya Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024 wakati ninachangia katika hotuba hii, mkandarasi alikuwa ametoka *site*. Yule wa *line* kubwa alikuwa anadai shilingi bilioni saba. Leo kwa moyo wangu wa dhati niko mbele yako nikiishukuru Serikali. Mkandarasi huyu tayari ameshalipwa hili deni na amerudi *site* kwa ajili ya kuanza kazi. Kwa kuwa tulikuwa 30%, basi asimamiwe naye ajitume, twende

kwa kukimbia kwa sababu ameshalipwa lile deni lake alilokuwa anadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba yule mkandarasi wa *substation* naye alipwe ili waende pamoja, kwa sababu zile *substations* zitawezesha wilaya zilizoko pembezoni ziweze kupokea umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kushukuru kwa Mradi wa Utafiti wa Mafuta unaofanywa katika Wilaya ya Meatu katika Ziwa Eyasi, Wembele. Kazi inaendelea vizuri, lakini sisi wananchi tulitamani kuona sasa tunanufaika na huu mradi kwa sababu umechukua muda mrefu, utafiti unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia bajeti hii ya nishati, lakini ninachukua nafasi hii vilevile kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema na rehema ambazo amenipatia hata kufika na kuweza kuongea mbele ya hadhara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo Sekta ya Nishati kwa kiasi kikubwa imepiga hatua katika nchi yetu. Nchi yetu sasa katika habari ya umeme imekuwa historia kwa sababu tuna umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru tena na kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu kwa weledi na umadhubuti katika kuchangia *stability* katika Sekta ya Nishati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nollo hebu subiri. Mheshimiwa Getere sogea pale kwa Mheshimiwa Almas Maige.

*(Hapa Mhe. Boniphace M. Getere alipita kati ya Kiti cha Spika na Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Nollo, endelea.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kushukuru kwa kazi kubwa iliyofanywa na Waziri wa Nishati, lakini ninashukuru kwa namna ambavyo vitongoji vyangu ambavyo Serikali iliahidi, vile 15, tayari kazi ya kuweka umeme katika maeneo yale inaendelea. Vijiji vyetu vyote 59 katika Wilaya ya Bahi tuna umeme, na sasa matarajio yetu makubwa, kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji iweze kuongezwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo matatu. Jambo la kwanza ambalo nataka nichangie, sasa tuna umeme wa uhakika lakini kubwa zaidi zipo tozo ambazo tunachangia kwenye mifuko hii. Mfuko ambao unaenda kuchangia katika kusambaza umeme katika maeneo yetu, fedha hizi, ile asilimia tatu, haziendi zote kama ambavyo tunatarajia. Fedha zile ziko *ringfenced.*

Mheshimiwa Spika, sasa, leo nimeuliza swali kuhusu Wizara ya Maji, kwamba fedha hizi zinakuwa na ukomo wa bajeti, ile *ceiling*. Sasa hizi ni fedha ambazo zinawekwa katika sekta maalumu kama hivi kwenye Nishati. Naishauri Serikali kwamba fedha hizi zitumike kama ambavyo tumekusudia kwenda kuendeleza Sekta hii ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu kuunganishiwa umeme *(Connectivity)* kwa mteja wa mwisho, ninadhani tutoke kwenye mazoea. Mteja sio kazi yake kununua nguzo zinazokuja kuunganishwa kwake. Duniani kote, mimi siwezi nikatoa *capital investment* ya shirika lile linalosambaza umeme. Kwa hiyo, tusifanye mazoea na *TANESCO* ibadilike, kwamba, inavyoniunganishia umeme mimi nitanunua umeme baadaye,

lakini unavyokuwa na wateja wengi unatengeneza *base* ya kuweza kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata ile tofauti ya shilingi 27,000 kwa shilingi laki tatu mijini na vijijini, mimi ninadhani tungekuwa na *flat rate* walau ya shilingi 50,000, ambayo ile tunalipa kwa ajili ya *administrative* na *labour cost*. Habari ya mimi ninunue nguzo, ninunue *material* za kuunganishia umeme, nadhani siyo sahihi. Kufanya hivyo tutaweza kuruhusu Watanzania wengi waweze kupata umeme katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni habari ya matumizi ya gesi. Nchi yetu tunaagiza gesi hii tunayopikia majumbani. Gesi hii haifanani na gesi inayotoka Mtwara. Hii ni gesi ambayo ni *LPG* ambayo tunanunua, tunatumia fedha nyingi. *LNG* ndiyo gesi ambayo tunatoa Mtwara, siyo lazima tutoe bomba kutoka Da es Salaam ije mikoa mingine katika miji. Tunaweza tukafanya kama tunavyosafirisha mafuta. Tukaweka *deport* kubwa ya gesi hapa Dodoma na gesi ikaletwa hapa na ikaweza kusambazwa katika majumba.

Mheshimiwa Spika, siyo lazima Serikali ifanye kazi hii; tangazieni kampuni kubwa waje wawekeze, tuweze kusambaza gesi katika majumba.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa, taarifa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasamu.

**TAARIFA**

**MHE. TAMASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kubeba gesi hiyo ya *CNG* kuisafirisha, gari moja lenye ukubwa wa tani 40 inabeba mzigo wa tani tatu tu peke yake. Sasa, kuisafirisha kuitoa Mtwara mpaka

kuileta Dar es Salaam kwa kutumia magari itakuwa ni hasara ambapo nchi itaingia katika hasara kubwa. Mheshimiwa endelea na mchango wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kenneth Nollo, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa yake kwa maana ya kwamba mimi nimelinganisha *LPG* na Gesi Asilia. Utaalamu wake kwanza unaisafirisha ikiwa *condensed*, ikifika hapa inakuwa *processed* inakuwa ni gesi. Sasa hii tunayotoa nje ni sawasawa unajenga ghorofa kwa kutumia maji ya kwenye ndoo. Sasa hiyo ghorofa utaimaliza saa ngapi?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sasa tuna reli. Unaweza ukasema kwa mfano *central zone* unaitoa Dar es Salaam, ukaweka *special train* ambayo itafikisha Dodoma hapa na mikoa mingine hivyo hivyo. Pia, Serikali kama inavyosambaza umeme kupitia *TANESCO*, itangaze kwani zitapatikana kampuni ambazo zinaweza kuwekeza na wananchi waunganishiwe katika nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kupitia Rais wetu, tumekuwa kinara katika kunusuru uharibifu wa mazingira. Sasa jambo hili kama nilivyosema, tukisambaza gesi katika nyumba zetu na kukawa na *distribution* nzuri, kwanza tutaondoa uharibifu wa mazingira. Miji yetu mikubwa; Dar es salaam, Dodoma na majiji mengine ndiyo yanayoongoza kwa kuchukua mikaa. Kwa hiyo uharibifu ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo *TPDC* wameanza pale Dar es Salaam kusambaza gesi, basi hata Dar es Salaam ingekuwa mfano. Jambo hili tukilifanya litasaidia kwa ajili ya kuondoa matumizi makubwa ya mkaa ambao unaleta uharibifu mkubwa wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumepata umeme wa kutosha na ipo haja ya kujadili. Je, ile 75 kwa *unit* tuendelee nayo au kuna haja ya kufanya mjadala vilevile kwamba tunaweza tukashusha. Ukishusha unaruhusu majumbani watu waweze

kutumia nishati ya umeme, tusiuogope sana umeme. Hoja yangu tusiuogope sana umeme. Kama ambavyo Serikali ime-*subsidize* kwa sababu tuna umeme wa kutosha, bado tuna nafasi ya kuweza ku-*subsidize* katika suala zima la kupunguza gharama za umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Judith Kapinga ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nitajitahidi...

**SPIKA:** Haya, ngoja nitakupa nafasi baadaye kidogo Mheshimiwa. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Nishati kwa ujumla wake, na kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. Kimsingi sisi watu wa Kanda ya Ziwa uwepo wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ni hazina kubwa katika watu wa Kanda ya Ziwa, na ni moja ya vijana wenye matumaini katika nchi yetu, lakini pia ni moja ya Mawaziri watulivu sana wanaoweza kusikiliza mtu na kuamua kile wanachoamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri, ameteuliwa hivi karibuni, lakini ameshika nafasi kama mtu wa siku zote. Ni moja ya wanawake jasiri sana hapa Tanzania, tunampongeza kwa usikivu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Rais wetu kwa kutoa umeme kwa nchi yetu ilivyokuwa *megawatt* 2,600 mpaka elfu nne na *poin*t na nchi ikatulia, akamaliza miradi yote ambayo yanahusika

na umeme hasa mradi mkubwa wa Bwawa la Nyerere; tunampongeza sana sana sana Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusema kweli uwepo wa mama umeonesha kwamba mwanamke anaweza kutenda matendo yoyote bila kusaidiwa, anaweza kusimamia miradi mikubwa na ikawezekana. Naishauri *TANESCO* na watu wa Wizara ya Nishati, kuna jambo naliona hapa. Mradi mkubwa wa mapato ya Serikali ni umeme, lakini umeme huo tunavyouendesha ni kama vile bidhaa adimu hivi.

Mheshimiwa Spika, amezungumza hapa Mbunge aliyekaa sasa hivi hapa, yaani kumpelekea mtu umeme ni kama vile unampelekea vitu vya anasa sijui, umwambie anunue sijui *NEAT,* atengeneze sijui vitu gani, afanye mambo gani, alete gari ya kuleta umeme, asafirishe; ni kitu gani hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu watu wote wa Tanzania wanahitaji umeme. Wote wanahitaji umeme. Siku hizi hakuna mtu anataka kukaa giza, hakuna. Watu wangu wa jimboni, ule umeme wanapelekewa wa *REA* imekuwa vita. Watu wanaenda wanauliza sasa umeme huu Mbunge amekatalia, umeme Mbunge amekatalia, umeme Mbunge amekatalia, umeme Mbunge amekatalia.

Mheshimiwa Spika, nimewauliza, mimi kazi yangu ya Ubunge ni kupeleka umeme kwenye Kijiji A au kwenye kitongoji A; kazi ya kugawa umeme kwa watu, uende wapi, siyo yangu, ni ya Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji, lakini mtu anapiga simu Mbunge umeninyima umeme, umeninyima umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kabisa biashara kubwa hapa Tanzania ni umeme. Tufanyeje? Tukopeshe watu umeme, watalipa. Si wanalipa *TANESCO!* Wanalipa umeme, si walipe! Si tupeleke hata tufanye *pilot area* hata Mkoa mmoja hata wa Mara? Tufanye *pilot area,* watu wote wanaouhitaji umeme wapewe halafu walipe, tutafute fedha benki watu walipe umeme, wakopeshwe umeme watalipa humo humo kwenye umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu umeme sasa tukienda nao hivi hatutafika. Tumeongeza umeme wa Bwawa la Nyerere, sasa huu unatosheleza. Tugawe umeme kwa kuwapa watu wenye uwezo, hivi kiwanda kinakosaje umeme? Si kipelekewe kilipe? Mtu anafanya biashara, ana mashine ya unga, ana mashine nyingine, ana viwanda vidogo, si wapelekewe walipe kwa mkopo? Kwani shida iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ni wateja wetu, kiwanda hakina umeme. Mtu anasema shilingi milioni 38. Yaani kupeleka maji kwenye kisima cha *pump* cha kijiji ni shilingi milioni 38; anatoa wapi? Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Dkt. Doto, nadhani sasa hivi amefika hatua nzuri, nami nilikuwa naelewa kidogo, sasa nimeelewa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Waziri wa Nishati na baadaye akapewa Naibu Waziri Mkuu? Kumbe nikakuta fedha nyingi zinazoendesha hii nchi zipo Wizara ya Nishati, miradi mikubwa ya mabilioni na matrilioni ipo Wizara ya Nishati. Kwa hiyo, ana nguvu zote Mheshimiwa Dkt. Doto, sasa watu hawamkaribii. Yeye aamue anachoamua, watu wapate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, nafarijika sana na kauli yako, uliwahi kusema, jamani hapa *TANESCO*, watu hawajui *optical fiber*, sijui hawajui umeme wa *Megawatts* 200 au 300 hawajui, wanataka umeme. Sasa na wewe hiyo lugha yako umeifanya imetusaidia sasa tutafute *alternative* ya kukopesha watu umeme ili watu wapate umeme. Mashine zote zipate umeme, viwanda vyote umeme, shule za sekondari zilipe kwa sababu wanapewa ruzuku, na shule za msingi walipe. Kwa hiyo, naomba watu wote wapewe umeme.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kushauri ni moja tu. *REA* wanapeleka umeme kwenye vitongoji na kwenye vijiji. Sasa hoja inakuja, ni nani aliyejua kitongoji A kinahitaji kilometa mbili, kitongoji C kinahitaji kilometa tatu, kitongoji A sijui ngapi? Au kitongoji hiki kinahitaji kilometa nne; nani aliyejua? Kwa nini tusiende kufanya *survey* kwenye vitongoji na vijiji halafu tukarudi kuja kuwapelekea umeme?

Mheshimiwa Spika, unaweza kukuta eneo moja lina nyumba ambazo zipo msongamano wa karibu ukawapelekea kilometa mbili, ukakuta nyumba zenye msongamano wa mbali mbali ukapeleka kilometa tatu, sasa unakuta unaleta vita kubwa. Tunaomba sasa *REA* waende kwanza wakaangalie mazingira yaliyopo kwenye kitongoji A, na kitongoji B, wapime halafu wakirudi waamue pale tupeleke tatu, pale tupeleke nne, pale tupeleke tano. Itasaidia kujua kwenye eneo ambalo linahitaji umeme mwingi wapelekewe umeme mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusema kweli watu wa *REA* wanafanya kazi nzuri sana, lakini Wakandarasi wa *REA* hatujui ni kitu gani kinatokea? Tunapima umeme mwezi wa Kwanza, kazi inakwenda kufanyika mwezi wa Sita. Wananchi wanaona kama vile wameenda kudanganywa. Tumekwenda kufanya hiyo *survey* mwezi wa Kwanza, tunakaa mpaka mwezi wa Sita ndio tunaenda kutekeleza umeme na hata wakati tunatekeleza tunatekeleza kitongoji kimoja, hapa viwili, hapa vitatu, hatuendi kwenye kasi inayohitajika, na tatizo kubwa wanasema ni nguzo.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwambia Mheshimiwa Dkt. Doto, tuna miti mingi, tuna zile nguzo sijui wanaita za zege, kwa nini sasa tena tunakuwa na matatizo makubwa kama haya? Tunaomba kama tumeamua kupimiwa umeme, tupelekewe kwa wakati muafaka ili wananchi waone kwamba kazi gani inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Mkuu, mwisho nakuomba, ile Bunda ni ya kwako na bahati nzuri wewe inaonekana wazazi wako walitokea maeneo yale. Sasa nakuomba, nina vitongoji vya Kata ya Kitale vingi havina umeme, vitongoji vya Kata ya Mihingo vingi havina umeme, vitongoji vya Kata ya Mgeta vingi havina umeme, vitongoji vya Kata ya Hunyari vingi havina umeme, vitongoji vya Kata ya Mang'uta vingi havina umeme, na vitongoji vya Kata ya Salama vingi havina umeme. Nakuomba kama mzaliwa wa Bunda pale, tafadhali utusaidie umeme.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Waziri wa Nishati ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nitaleta kwa maandishi mchango wangu. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote

wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri imejaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Nishati, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimazi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kuendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya umeme ikiwemo Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini *(REA)* kwa 100% na ujenzi mkubwa wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere *(JNHPP)* lenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 2115. Miradi hii ya kusambaza umeme vijijini umeiweka Tanzania katika nafasi ya juu Afrika na umeweza kuchochea kasi ya ukuaji wa viwanda na uchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za vita ya Ukraine na Urusi na kupelekea kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, naipongeza Serikali kwa kuishirikisha Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, *EWURA* na wadau wengine, kuimarisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta *(Fuel Price Stabilization Fund)* ili kukabiliana na kupanda kwa bei za mafuta.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ichukue hatua stahiki za kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kimkakati ya Mafuta *(Strategic Petroleum Reserve - SPR)* ili kukabiliana na dharura na kuimarisha usalama na uhakika wa mafuta kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuchochea upatikanaji wa *US$* hasa kutoka vyanzo vya madini na kilimo na ikiwezekana kuanzisha utaratibu wa biashara ya Serikali kwa Serikali na nchi rafiki zinazozalisha mafuta kwa makubaliano ya kulipa baada ya makusanyo ya mauzo ya madini na kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza kuratibu mfumo mzuri wa kununua dhahabu yote toka kwa wachimbaji wadogo kwa shilingi na kulipa bei nzuri zaidi kuliko hata ya soko, na ikifanya hivyo kwa mazao ambayo yamekuwa yanatoroshwa kinyemela nje ya nchi; dhahabu na mazao yaliyonunuliwa kwa shilingi yapate soko zuri kwa wanunuzi kwa dola za Kimarekani kusaidia uagizwaji wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kununua mafuta kwa pamoja *(BPS)* umeonesha mafanikio makubwa na napendekeza uendelee ikiwa ni pamoja na kuvutia kutumika kwa mahitaji ya mafuta kwa nchi jirani. Mfumo huu uboreshwe hasa katika kuweka vinasaba kwa kutumia mashine *(automation)* na pia kuwepo na ulinganifu wa taarifa ya kila siku kati ya kiasi cha vinasaba vilivyotumika na kiasi cha mafuta yaliyopakiliwa na pia magari ya kubeba vinasaba yafungwe kamera kwa ajili ya udhibiti mafuta yanayoenda nchi za nje pasipo kutorudi kinyemela kutumika nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za kupakua mafuta bandarini, napendekeza kupanua na kuboresha miundombinu ya kupakulia na kupokelea mafuta ikiwemo kupakua mafuta kwa saa 24. Napendekeza pia kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwa matumizi ya ndani na pia kwa nchi jirani na usafirishaji uwe wenye tija kubwa ikiwemo kusafirisha kwa treni.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iangalie uwezekano wa kujenga bomba la mafuta kwenye MKUZA wa *TAZAMA* na kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwenye bandari kavu Mbeya kwa matumizi ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na nchi jirani za *DRC*, Zambia, Malawi na hata Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kufikisha umeme kwa 100% kwenye vijiji vyote na pia kwa mkakati wa kufikisha umeme kwenye vitongoji vyote vya Jimbo la Mbeya Vijijini. Napendekeza kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mradi wa Ujazilizi *(Densification)*.

Mheshimiwa Spika, napendekeza utekelezaji utoe kipaumbele kwa vitongoji kwenye idadi kubwa ya wakazi na maeneo yenye shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwemo Shule ya Sekondari Lwiji. Katika vijiji vilivyopatiwa umeme kwa kiasi kikubwa imechochea ukuaji wa viwanda hasa vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Nashauri *TANESCO* iongeze *speed* ya kuunganisha umeme na pia kushughulikia maombi ya wateja wengi wanaosubiri umeme ikichukuliwa kuwa hii ni fursa pia kwa *TANESCO* kuongeza mapato ya shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na vyanzo vya sasa, napendekeza Serikali itekeleze miradi ya vyanzo vingine, kama vile vyanzo vya jotoardhi, umeme wa jua, upepo na makaa ya mawe ili nchi yetu iendane na mahitaji makubwa ya umeme kwa hapa Tanzania na hata kuuza kwa nchi nyingine za Afrika.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa, *TANESCO* kupitia Kampuni Tanzu ya Uendelezaji wa Jotoardhi Nchini *(TGDC)* inaendelea na tafiti katika maeneo mbalimbali nchini kama vile eneo la Ziwa Ngozi lililoko Mkoani Mbeya ambapo ndipo yalipo makutano ya Bonde la Ufa la Upande wa Mashariki na lile la Magharibi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iharakishe utekelezaji wa miradi huu wa jotoardhi na ule wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Kiwira ili tuweza kuzalisha umeme zaidi kwa mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu kwa maandishi. Kwanza, natoa pongezi kwa Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa wanayofanya katika kuhakikisha nchi yetu inakuwa na umeme wa uhakika, kipekee katika Jimbo la Iringa Mjini ninaloliwakilisha.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa suala la kusambaza umeme ni kutoa huduma chochezi ya ukuaji wa uchumi nchini na kwa kuzingatia kuwa mipaka ya ugawaji wa kiutawala wa nchi yetu huwa hauzingatii kipato cha wananchi wetu, basi ni muhimu *TANESCO* wakatengeneza *formula* yao ya usambazaji wa umeme ukilinganishwa na kipato cha kiuchumi halisi cha wananchi kwamba wale wananchi wanaoishi ndani ya miji, lakini wana kipato kidogo waunganishiwe umeme kwa bei ya vijijini zikiwemo *peri urban areas.* Mfano, maeneo ya Mitaa ya Ugele, Msisina, Mtalagala, Kigungawe, Mosi, Wahe, Ulonge ndani ya Jimbo la Iringa Mjini.

Mheshimiwa Spika, tatu, maeneo ya mijini yaliyoanishwa kama vitongoji 15 au mitaa 15 katika maeneo ya mijini na kutakiwa kupewa umeme yafikishiwe umeme au ule mpango wa *peri urban* utekelezwe. Mfano maeneo ya Mitaa ya Ugele, Msisina, Mtalagala, Kigungawe, Mosi, Wahe, Ulonge ndani ya Jimbo la Iringa Mjini.

Mheshimiwa Spika, nne, tunaomba *TANESCO* iongezewe fungu la usambazaji umeme kama ilivyo kasi ya kufikisha umeme, basi iende sambamba na usambazaji wake. Kwa kuwa, maendeleo nayo yanaibua changamoto nyingine, watu wanavyoona umeme umefika haujasambazwa inazua tena malalamiko.

Mheshimiwa Spika, tano, suala la mafuta tunaomba ukaguzi ufanyike kwa uhakika kwa kuwa baadhi ya vituo vya kuuzia mafuta vinauza mafuta machafu yanayowatia hasara wananchi kwa kuharibu vyombo vyao vya usafiri. Hii inadumaza ukuzaji wa uchumi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuendelea kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Temeke.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika kwa kasi kubwa na hasa hii ya nishati na kutambulika kama *champion* wa nishati, hakika amegusa wananchi wote ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Biteko kwa kazi kubwa na nzuri akisaidiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Spika na Naibu Spika pamoja na Katibu wa Bunge pamoja na Wenyeviti wote wanaotuongoza katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana kwa jinsi gridi ya Taifa ilivyosambazwa nchini kwetu, hakika ni hatua kubwa kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusiana na suala la watu wa mijini kuwekewa umeme. Pamoja na kwamba kuna baadhi ya kata nyingine ni sawa na vijijini, lakini kwa bei iliyowekewa watu wa mijini hali siyo nzuri kwa wengine. Naomba sana tuweze kuunganishiwa umeme kwa bei hiyo ya shilingi 320,960 kwa kulipa kwa awamu hata kama ni mara nne, lakini ilimradi iweze kukatwa kwenye *bill* za mwezi.

Mheshimiwa Spika, nisiwe mchoyo wa fadhila, hakika kwa sasa umeme wetu jimboni Temeke umerudi vizuri, kukatikakatika kwa sasa ni kwa ajili ya marekebisho ya nguzo tunazowekewa. Naamini baada ya kazi hiyo ya kuwekewa nguzo za zege, jambo litakaa sawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza wewe kwa kuliongoza vyema Bunge. Pia nampongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, nielekee katika mchango wangu. Wapo wananchi mpaka leo bado umeme haujafika. Naomba Serikali ichukue juhudi za makusudi ili waweze kupata umeme. Serikali imejielekeza kuboresha nishati ya kupikia ili wananchi hasa akinamama waachane na kupikia kuni ili waendelee kutunza mazingira, Serikali kufanya utaratibu wa kuongeza majiko ya gesi kwa wale ambao hawajafikiwa waweze kufikiwa na tuwaombe wanaouza mitungi ya gesi, wapunguze bei ili waweze kununua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Bajeti hii ya Nishati ya mwaka 2025/2026 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi anazoendelea kuzifanya za kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naungana na Umoja wa Afrika *(AU)* kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa ajenda ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya nishati safi ya kupikia ni muhimu katika kuokoa ukataji holela wa misitu kwa matumizi ya kuni na mkaa. Ukataji ovyo wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa unachangia sana mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuleta mafuriko ya mara kwa mara, jangwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, wananchi tukilinda misitu yetu, mito yetu, na Bahari, nchi yetu itakuwa na neema ya mvua nzuri, uvuvi bora na ustawi wa chakula.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuimarisha Sera ya Nishati Safi Kupikia, tutalinda afya za wanawake dhidi ya magonjwa mbalimbali kama vile Kifua Kuu na Kansa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili, najielekeza kuhusu Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere lililopo kule Rufiji. Naendelea kumpongeza tena Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana ya ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na kulikamilisha kwa wakati pamoja na miradi mbalimbali inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, bwawa hili ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Kule Zanzibar kuna uwekezaji mkubwa wa hoteli kubwa na ndogo ndogo katika mkoa wangu wa Kaskazini Unguja. Ujenzi wa hoteli hizo kwa kiwango kikubwa utakwenda kusaidia wananchi kwa kupata ajira na fursa za biashara.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kuipongeza Wizara ya Nishati chini ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko na Naibu Waziri Mheshimiwa Judith Kapinga na watendaji wote wa Wizara hii ya Nishati kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya katika kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kule Mkoa wa Kaskazini Unguja wanawake bado wanateseka na matumizi ya kupikia kuni na mkaa, nilikuwa naiomba Serikali, mkaa mbadala uweze kuingia Zanzibar na uanze kutumika ili wanawake hawa wapate kutumia kwa matumizi ya kupikia, pamoja na gesi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kazi nzuri sana anayoifanya

katika Wizara hii na nchi yetu kwa ujumla. Ametupa imani kubwa sana, tunaendelea kumwombea.

Mheshimiwa Spika, pia tunampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Judith Kapinga, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, ninayo mambo machache katika mchango wangu. Kwanza napongeza kazi nzuri iliyofanywa na Wizara hii hasa katika Mkoa wangu wa Iringa. Mkoa wetu wote tumeshapata umeme katika vijiji vyote na sasa bado vitongoji tu baadhi bado, tunaiomba Serikali itenge fedha za kutosha ili wananchi wote waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna maeneo yaliyokuwa ya vijijini baada ya upanuzi wa miji yakaingia mijini na ilikuwa chini ya mpango wa *REA*. Naomba Serikali ifanye upembuzi yakinifu ili maeneo hayo yapate umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama ya usambazaji umeme, gharama za uunganishaji zimekuwa kubwa sana. Kuna baadhi ya malalamiko ya wananchi. Kumekuwa na tofauti kubwa sana ya kuunganishia umeme wananchi mfano wananchi wa vijijini, wanaunganisha kwa shilingi 27,000 na walio umbali wa mita 70 wanaunganisha kwa shilingi 515,617 na umbali wa mita 120 shilingi 696,669.64. Tunaomba Serikali iangalie upya hizi gharama za kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu ujenzi wa vituo vya mafuta umeonekana kufanyika kwa namba, vipo jirani sana vingine karibu na makazi ya watu na inahatarisha sana maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuipongeza Serikali, ilitangaza *tender* ya kujenga vituo vidogo vijijini na mikopo ya ujenzi wa vituo hivyo na ukaguzi na vibali vilitolewa, lakini hatujajua mpango huo ukoje? Umefikia wapi? Kwa kuwa ni mpango mzuri wa kuhakikisha wananchi wa vijijini wanapata mafuta ya uhakika

na kutekeleza ukuaji wa uchumi nchini, nampongeza sana Mkurugenzi wa *REA* kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni mpango wa Serikali wa kuzalisha umeme kwa kutumia Mto Ruaha ni wa muda mrefu sana. Je, lini sasa mpango huo utakamilika ili kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha Kv 400 kutoka Iringa mpaka Sumbawanga kupitia Tunduma?

Mheshimiwa Spika, kuhusu usambazaji gesi, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kwa kupata tuzo kuwa kinara wa nishati safi ya kupikia. Najua hiyo yote ni juhudi ya Wizara hii. Tunaomba sasa Serikali iwe na mpango mkakati wa kuhakikisha bei ya gesi ya kupikia inakuwa ndogo na gharama ya mitungi ili ile dhamira ya kutunza mazingira na kumtua mwanamke kuni kichwani iweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kuhakikisha sekta ya nishati inaendelea kufanya kazi kwa kuipatia fedha za kutosha. Pia nampongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Judith Kapinga pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro una mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Kupitia bajeti hii, tunaomba Serikali iweze kukamilisha usambazaji wa umeme katika vitongoji ambavyo bado havijaunganishiwa umeme. Hii itasaidia kuinua kipato na kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza mambo yafuatayo yazingatiwe katika bajeti:-

(a) Kuongeza uwekezaji wa umeme vijijini *(REA)* ili kuunganisha umeme kwenye yale maeneo ya Mwanga-Same na Rombo ambayo bado havijafikiwa na umeme na kuhakikisha upanuzi wa miundombinu ya umeme vijijini unatekelezwa kwa kasi.

(b) Kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya nishati mbadala Mkoa wa Kilimanjaro una fursa kubwa ya kutumia nishati jadidifu kama jua na *biogas*. Bajeti itenge fedha za kusaidia wananchi hasa wakulima na wafanyabiashara wadogo kupata teknolojia hizo.

(c) Kugawa majiko ya gesi kwa kaya za kipato cha chini ili kulinda mazingira ya Mlima Kilimanjaro dhidi ya ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa. Serikali itenge bajeti mahsusi ya kugawa majiko na mitungi sambamba na elimu ya matumizi salama. Hatua hii itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira kuhifadhi vyanzo vya maji na kukuza utalii endelevu.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kampeni yake kabambe ya nishati safi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, kupitia hamasa hii ya Mheshimiwa Rais, naomba niishauri Serikali yangu sikivu kuendelea kuongea na wadau kushusha bei ya gesi ili kila Mtanzania aweze kutumia nishati safi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, pia, naishauri Serikali kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya makaa ya mawe ili kuendelea kutunza mazingira yetu na kulinda afya za Watanzania kwa ujumla.

**SPIKA:** Namwita sasa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati, atafuatiwa na mtoa hoja, Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya kuchangia hoja. Awali ya yote naomba nianze kwa

kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na baraka zake na kutujalia tuwepo hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa sana, naomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu, lakini kwa mahususi kwa kazi kubwa inayofanyika katika Sekta ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya misingi ya ukuaji wa kiuchumi na maendeleo katika Taifa lolote ni uwekezaji katika Sekta ya Nishati. Uwekezaji usipofanyika vizuri katika Sekta ya Nishati, unaweza kuchangia kupungua kwa pato la Taifa kwa hadi asilimia mbili na ndiyo maana tunaona leo Mheshimiwa Rais, ameweka nguvu kubwa sana katika kuwekeza katika Sekta ya Nishati kwa ajili ya kutegemeza sekta nyingine katika ukuaji wa kiuchumi wa Taifa letu na vilevile, katika kutegemeza sekta zinazotoa huduma za kijamii katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli tunaendelea sana kumpongeza Mheshimiwa Rais na hata pongezi hizi zote ambazo zinatolewa kwa kweli ni pongezi zinazostahili sana kwa jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo mingi wanayotupatia katika utekelezaji wa shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba pia nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kwa namna ambavyo unatuongoza vizuri sana hapa Bungeni. Kwa kuwa nami ni kiongozi mwanamke, naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wengi tunamfahamu kwa sifa zako kama Spika wa Bunge, lakini Spika wa Mabunge Duniani, lakini wengi hawafahamu kwamba Spika huyu pamoja na shughuli nzuri za

kuwalea wanawake *TWPG,* lakini ndio mlezi wa Wabunge vijana wanawake kwa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na shughuli zako za Bunge tunaendelea kukupongeza kwa mchango mkubwa unaouweka katika kumwinua mwanamke kiongozi. Ahsante sana na Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote ambao kwa kweli wanafanya shughuli zao vizuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba niipongeze Kamati yetu ya Kudumu ya Nishati na Madini inayoongozwa na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. David Mathayo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati. Kwa kweli kwa kipindi chote hiki ambacho mimi nimekuwa Naibu Waziri, tumefanya kazi vizuri sana na kwa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Judith, Waziri mchapakazi kabisa kwamba, uzalendo na utendaji wake mzuri wa kazi ambao ninajua ameurithi kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, umeimarisha diplomasia ya mabunge na juzi Bunge lako limeweza kutoa mtu ambaye amechaguliwa kuwa Katibu wa Maziwa Makuu katika Ukanda wa Nchi 12.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampa taarifa mdogo wangu Judith kwamba diplomasia aliyoimarisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Kimataifa umeirithi kuiimarisha kwenye mabunge ya Afrika na Dunia, jambo lililopelekea Tanzania juzi

kupata nafasi ya kushinda kiti cha Katibu wa Maziwa Makuu katika ukanda wa Afrika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa nzuri ya kaka yangu Mheshimiwa Kingu. Naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Kamati, kwa kweli tumefanya kazi vizuri na tunaendelea kuishukuru kwa miongozo yao ambayo imekuwa ikitupatia wakati wote.

Mheshimiwa Spika, jana wakati tumeanza kuchangia bajeti hii, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge kuanzia jana mpaka leo tumewasikia vizuri sana, nami ningependa kipekee niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli michango yao imegusa mioyo yetu, pongezi walizozitoa kwa Mheshimiwa Rais, kwa kweli ni michango yenye uungwana mkubwa sana kwa kazi nzuri iliyofanyika katika Serikali ya Awamu ya Sita; na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kweli hatuna la kuwalipa zaidi ya kuwatakia mema kuelekea 2025 mwaka huu muhimu. Ninaamini wote tutarudi hapa Novemba na tutaapa tena hapa na tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Watendaji wetu Wizarani; Katibu Mkuu pamoja na Naibu Makatibu Wakuu, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi na Wafanyakazi wengine wote ambao tunafanya kazi kwa pamoja katika Wizara ile ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, ninapomalizia sehemu yangu ya kwanza ya utangulizi, wakati ninaanza kazi yangu ya Unaibu Waziri ambayo nimepewa dhamana na Mheshimiwa Rais na ninamshukuru sana kwa kuniamini kwa nafasi hiyo, kazi hii nimeifanya vizuri sana kwa sababu ya kiongozi mahiri, mwalimu

mwema ambaye anatuongoza wote katika Wizara ya Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nimshukuru sana bosi wangu Mheshimiwa Waziri kwa miongozo ambayo amenipa kwa kipindi chote hiki ambacho nimekuwa Naibu Waziri. Nimekuwa bora sana kwa sababu nipo chini ya kiongozi kama yeye ambaye kwa kweli anapenda hata sisi wa chini wake tuendelee kuwa bora. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa namna ambavyo anaendelea kutuongoza vizuri Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hayo ya utangulizi na shukrani, naomba sasa nijikite kwenye kueleza baadhi ya hoja ambazo zimeongelewa hapa na Waheshimiwa Wabunge. Mojawapo ya masuala ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaongea kwa nguvu sana ni kuhusiana na ile mikoa ambayo bado haijaunganishwa katika gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia Waheshimiwa Wabunge kutoka katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Rukwa, Katavi pamoja na Mkoa wa Kagera. Nikianza na mkoa mmoja mmoja, katika Mkoa wa Rukwa, Serikali tayari imeshaanza kufanyia kazi. Tunao mradi mkubwa ambao unapeleka umeme katika Mkoa wa Rukwa kwa kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Iringa - Tunduma hadi Rukwa, na vilevile kujenga kipande ambacho kitatuunganisha na Zambia.

Mheshimiwa Spika, mradi huu sio kwamba tu unapeleka umeme katika Mkoa wa Rukwa, ni mradi ambao unaenda kunufaisha na mikoa mingine ambapo ipo Nyanda za Juu Kusini, kwa sababu inaenda kujenga vituo vya kupooza umeme katika maeneo haya ambapo mradi unapita. Vipo vituo ambavyo vinaenda kujengwa ikiwemo Kisada pale Mafinga, Iganjo - Mbeya, Nkangamo - Tunduma pamoja na Malangali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mradi ambao pamoja na kwamba unapeleka gridi katika Mkoa wa Rukwa, utatusaidia vilevile kujenga vituo vya kupooza umeme katika namna ya

kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Songwe, na Rukwa. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Mkoa wa Rukwa, Serikali ipo kazini kuhakikisha kwamba gridi inafika katika Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mikoa ya Mtwara na Lindi, tayari mkandarasi yupo *site* na tumemsikia Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru Kusini akisema jana, kwamba Mkandarasi alikuwa ameondoka *site* kwa takribani miezi minne. Mradi wa kupeleka umeme katika Mkoa wa Mtwara na Lindi ni kipaumbele katika Serikali ya Awamu ya Sita. Mkandarasi sasa amerudi *site* na mradi huu umeanza kwa kujenga njia ya umeme kutokea Songea kwenda Tunduru, Masasi hadi Mahumbika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi, suala la kupeleka gridi katika mikoa hiyo kwa kweli ni suala la kipaumbele na Mkandarasi yupo *site*. Taarifa njema ni kwamba tarehe 25 tumeanza kulipa fidia katika eneo la Tunduru hadi Masasi, takribani shilingi bilioni 4.6 na eneo lililobakia la Songea kuelekea Namtumbo na Tunduru tutaendelea kulipa fidia hiyo ya takribani shilingi bilioni 2.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa mikoa ya Mtwara na Lindi, bado suala la kupeleka gridi katika mikoa hiyo ni kipaumbele na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kagera, kazi pia inaendelea kupitia kujenga njia ya kusafirisha umeme ya Benaco – Kyaka, huko pia miradi ya kupeleka gridi inaendelea. Katika Mkoa wa Katavi kwa kweli mradi upo katika hatua za mwisho kabisa, tunayo imani ndani ya mwezi mmoja *maximum grid* itakuwa imefika katika Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika Mikoa yote, kazi hii inafanyika na inakamilika katika Serikali ya Awamu ya Sita, ni kuonesha *commitment* ambayo Mheshimiwa Rais anayo ya kutaka Watanzania wote waendelee kupata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kushukuru sana katika Awamu hii ya Sita ndipo ambapo pia na gridi imefika katika Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, nikuendelea kuwathibitishia suala la kupeleka umeme katika mikoa ambayo haijaunganishwa na gridi ni kipaumbele katika Serikali ya Awamu ya Sita, wakandarasi wapo *site* na umeme utafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya hoja ambazo zimezungumzwa pia na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusiana na umeme wa visiwani. Tunavyo visiwa takribani 118 ambavyo kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamikia kuhusiana na masuala ya umeme, nami nakubaliana pia.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tumewasikia Wabunge wa Ukerewe wakisema, na ni kweli kabisa kulikuwa kuna visiwa pale takribani 20, kulikuwa kuna mkandarasi anaitwa Jumeme, Serikali ilimwezesha kwa fedha takribani shilingi bilioni 2.1 miaka ya 2017 huko nyuma kwa ajili ya kuweka mifumo jua, lakini sasa mradi ule umekuwa una changamoto kiasi cha kufanya wananchi wasiendelee kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, tumewasikia Waheshimiwa Wabunge, na ndiyo maana Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kupeleka mifumo mingine ya jua ya umeme katika visiwa 118. Visiwa hivyo havitakuwa tu Mwanza, ni visiwa ambavyo vipo katika Mikoa zaidi ya mitano ambayo yote watapelekewa mifumo ya umeme jua, lakini mahsusi kwa ajili ya Ukerewe ambapo Waheshimiwa Wabunge takribani wawili wamezungumza. Ukerewe pale tunao mradi kupitia gridi imara katika awamu ya kwanza ambao unalenga kujenga kituo cha kupooza umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme kutoka Bunda hadi Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, mradi huu upo na mkandarasi amepatikana, tunaendelea kufanyia kazi ili sasa mradi uweze kuanza. Kwa hiyo, kwa ndugu zangu wa Ukerewe tunataka tuwahakikishie kwamba mikakati ipo kwa ajili ya kujenga kituo cha kupoza umeme na njia ya kusafirisha umeme kutoka Bunda hadi Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanatokea katika visiwa vingine vyote, tayari Serikali imetoa fedha takribani shilingi bilioni 9.89 kwa ajili ya kupeleka mifumo ya jua kwa ajili ya kuimarisha umeme. Tutatoa mifumo karibia 20,000 katika visiwa vyote hivi 118. Kwa hiyo, kwa kweli tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha ili wananchi hawa ambao wapo katika visiwa hivi 118 waendelee kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya mwisho ambayo ningependa kuizungumzia ni kuhusiana na maboresho ya umeme katika Mkoa wa Dar es Salaam. Tulisikia Mheshimiwa Mbunge akizungumzia kuhusiana na umeme katika maeneo ya Mbagala pamoja na Temeke. Nami nataka niseme, ni kweli tulikuwa na changamoto ya kukatikakatika kwa umeme, lakini katika kufanyia kazi suala hili katika kituo chetu cha kupooza umeme cha Mbagala kilikuwa kimezidiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna transfoma pale yenye uwezo wa *MVA* 50, kwa sasa kwa kweli wataalam wetu wanafanya kazi usiku na mchana, tunaweka pale *transformer* mpya yenye uwezo wa *MVA* 120 kwa ajili ya kuongeza ukubwa wa kile kituo ili wananchi wa Mbagala, Temeke, Yombo, Mkuranga pamoja na baadhi ya maeneo ya Kigamboni waendelee kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hususan wale ambao wanatokea katika maeneo ya Mbagala na Temeke pamoja na Yombo, Mkuranga na baadhi ya maeneo ya Kigamboni, kazi hii imefikia mwishoni muda wowote kuanzia sasa *transformer* ile itaanza kufanya kazi na kwa kweli tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya kukatika katika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Kigamboni kwa kweli tuliwasikia wananchi pia wakilalamika katika *feeder* yetu ya Mwongozo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alitoa maelekezo na tulitenga fedha pale kwa ajili ya kuboresha matengenezo kinga lakini vilevile maboresho ya *voltage,* vilevile kubadilisha baadhi ya

mifumo kwa ajili ya kusaidia wananchi wa Kigamboni kupunguza tatizo la umeme. Kazi hiyo imefanyika, na kwa kweli kuna maboresho na uwezeshaji mkubwa sana katika *feeder* ile ya Mwongozo pale Kigamboni na wananchi kwa kweli wamefurahi kwa mabadiliko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapomalizia, kwa mara nyingine tena kazi hizi zimefanyika vizuri sana kwa miongozo ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na ndiyo maana tunaona mafanikio makubwa ambayo yapo katika sekta ya nishati. Tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kipindi ambacho miradi ya umeme hususan ya uzalishaji imekamilika, katika historia ya Taifa letu ni katika kipindi cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaisema hapa, Mradi wa Rusumo, *Kinyerezi One Extension,* Bwawa la Mwalimu Nyerere na miradi mingine inayoendelea kama Malagarasi ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaisema, ni miradi ambayo imekamilika na ni miradi ambayo inaendelea kutokana na uwekezaji mkubwa na *commitment* ambayo Mheshimiwa Rais anayo katika sekta ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavyomalizia kabisa, tunaendelea kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao mnaendelea kutupatia, nasi tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu basi atujalie ili tuendelee kufanya vizuri shughuli zetu, vilevile nawatakiwa kila la heri katika uchaguzi ambao unakaribia hapa karibuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu

Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kuwepo hapa kwa siku hizi mbili ambapo tumeendelea na mjadala huu muhimu sana unaohusiana na uchumi na maendeleo ya watu wetu, lakini muhimu zaidi katika harakati ya kuwapatia nishati wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema lolote, naomba nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo umetuendesha kwenye mjadala huu kwa muda wa siku mbili, umekuwa mjadala wa tija sana kwetu kwenye sekta lakini na kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wameona namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanazungumza masuala yanayowahusu, toka mzungumzaji wa kwanza hadi wa mwisho, hakuna ajenda waliyokuwa wanaizungumza zaidi ya nishati kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwani kwa hali ya kushangaza kabisa, asubuhi nilivyoacha kukuona hapa, nilijua hutaweza, maana nilikuona kwenye *TV* ukiwa Dar es Salaam, lakini wakati Mpambe wa Spika anakuingiza humu ndani nilitarajia atasema Mheshimiwa Naibu Spika au Mwenyekiti, nikasikia anaita Mheshimiwa Spika mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni ishara kuwa unaipenda kazi yako na unapenda kuwahudumia Watanzania. Ulikuwa na sababu zote kabisa za kusema kuwa ulikuwa na majukumu mengine, na unao wasaidizi wengi ambao wangefanya hiyo kazi, lakini umeamua kuwahi ili kuja kuhitimisha hoja hii. Kwa niaba ya wenzangu Wizarani tunakushukuru sana kwa heshima hiyo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge imeonesha ukubwa wa sekta hii namna ilivyo muhimu katika maendeleo ya uchumi, maendeleo ya kijamii na pia namna wananchi kupitia Wawakilishi wao walivyo na kiu ya kuona huduma zinazotolewa katika Wizara na Taasisi zake hususan upatikanaji wa nishati ya umeme gesi

pamoja na huduma nyinginezo zinawafikia kikamilifu na kutatua changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, nitumie fursa hii kusema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati itahakikisha kuwa ushauri na maoni yote tuliyoyapata kutoka kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge yanafanyiwa kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa mchango wake kwenye hotuba yetu ya bajeti ya mwaka 2025/2026, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hotuba hii kwa kauli na kwa maandishi. Tumeona Waheshimiwa Wabunge waliochangia jumla ni 49. Waliochangia kwa kusema ni 42 na Waheshimiwa Wabunge saba wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kuwa mchango yao yote waliyoitoa tutaizingatia. Tupo katika kujenga nyumba moja na hatuwezi kuendesha hii sekta peke yetu, tunahitajiana wote wakati wote, nami nataka nitoe ahadi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba yote waliyosema Waheshimiwa Wabunge tutakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Aidha, niseme kuwa hoja zote tutaziandalia majibu ya maandishi na kuziwasilisha kwenye Ofisi yako kwa ajili ya rejea yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza iliyozungumzwa kwa nguvu sana na Waheshimiwa Wabunge ni Mradi wa *LNG*, umeanza kusemwa kwa muda mrefu, kila mmoja angetamani mradi ule ukamilike jana; lakini mradi huu pamoja na kuanza muda mrefu, tukubaliane kuwa lazima tujadiliane ili tupate kilicho bora. Tunatamani mradi huo uwepo, lakini majadiliano haya ni lazima yatupe tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka hapo nyuma Serikali baada ya kukamilisha majadiliano awamu ya kwanza ilirudisha majadiliano hayo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata maoni. Baada ya kupita kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ukweli ni kwamba kuna maeneo mengi ambayo yalikuwa wanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili kupata mkataba ulio mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, leo tunaweza kusema mradi huo uanze, lakini nataka niseme kwamba mkataba ulio mzuri leo, kesho unaweza kuwa mkataba mbaya. Nchi hii ina historia ya kupita kwenye mikataba hiyo inayolalamikiwa. Tumejifunza mengi kwa safari toka tumeianza *extractive* kwenye nchi yetu, yapo mambo na maeneo kadhaa ambayo ni lazima yafanyiwe kazi kabla ya mkataba huo kusainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukuhakikishia ni kuwa Serikali pamoja na wawekezaji, timu zinaendelea na majadiliano ili kuondoa changamoto zilizopo ambazo zimebaki chache sana na tunatarajia kuwa ndani ya mwaka huu 2025, kama tutakuwa tumemaliza mambo matatu yaliyosalia, nataka nikuhakikishie kuwa mkataba huo utasainiwa na mradi huo uanze mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wito wangu kwa Waheshimiwa Wabunge, naomba mtupe muda. Tunajua kuwa hili jambo linahitajika kwanza kwa uchumi wa nchi yetu, lakini kwa maendeleo ya watu wa Mikoa ya Kusini ambako gesi ipo. Ingekuwa ajabu sana siku moja tuingie mkataba, tumekubaliana na mwekezaji ndani ya mkataba ule, mwekezaji awe ameruhusiwa *local content* ya Tanzania isitumike, hakuna mtu angetuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu angetuelewa kwamba bima zote ambazo zinatakiwa ku-*cover* huu mradi zote zitoke nje ya nchi bila ushiriki wa Watanzania; hakuna mtu ambaye angetuelewa kwamba tutachimba gesi, lakini *domestic gas,* yaani gesi ya matumizi ya ndani iwe angalau asilimia tatu, hakuna mtu angetuelewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yapo mambo mengi ya kiuchumi na ya kisheria ambayo tunayapitia. Jambo la kutia moyo ni kwamba wawekezaji wetu hawa tumekubaliana mengi sana, yaliyobaki ni machache, na hivi ninavyozungumza timu zetu zipo Arusha zinaendelea na hayo majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie, Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati ananiteua kuwa Waziri wa Nishati aliniambia angetamani sana kuona mradi huu unakamilika kabla hatujaenda kwenye uchaguzi. Nataka nirudie hilo, mwenye kiu namba moja ya kuona mradi huu unakamilika ni yeye mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika na Ndugu zangu wa Mtwara na Watanzania pamoja na watu wa Lindi, naomba tuwe na subira, tunahitaji kilicho bora. Isingefaa leo tupitishe mkataba, na baada tu ya kupitisha mkataba tuanze kujitetea tena kwa miaka yote maisha yote mpaka mkataba uishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mikataba mingi tuliyopitia mnaifahamu, ambayo ilikuwepo baada ya kuwa imefungwa ina maisha ya miaka 20 huwezi kuivunja, tumebaki kulalamikiana humu ndani kuunda Kamati na kadhalika, lakini mkataba upo. Makosa ambayo tuliwahi kuyafanya huko nyuma, nafikiri ni muda muafaka sasa kuyarekebisha na kupata kilicho bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, iliyozungumzwa ni ongezeko la vituo vya mafuta vinavyojengwa karibu karibu. Kanuni ya viwango vya upangaji miji za mwaka 2015, iliyotengenezwa chini ya Sheria ya Mipango Miji Sura ya 355, inaelekeza kuwa umbali wa mita 200 kutoka kituo kimoja hadi kingine kama vituo hivyo vipo upande mmoja wa barabara na kama vituo hivyo vipo pande tofauti wa barabara, umbali huo unakuwa unatengenisha vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wasiwasi ambao umekuwa ukioneshwa na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuhusu ongezeko la vituo hivyo vya mafuta kuwa karibu sana kutoka

kituo kimoja hadi kingine, Wizara ya Nishati imeanza mazungumzo na Wizara ya Ardhi ili kubadilisha kanuni hizo ili kuwezesha kuongeza walau umbali kidogo unaotakiwa kati ya kituo kimoja na kingine kwa kuzingatia masuala ya afya, usalama mazingira na shughuli za kijamii. Hili jambo lipo kwenye sheria, kwa hiyo, tunalifanyia kazi tuone namna gani tunaweza kuichukua michango ya Waheshimiwa Wabunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameeleza haya mambo kwa uzito mkubwa sana, hatuwezi kuyachukulia kwa wepesi tukayaacha yakapita. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, toka tumeanza kwenye Kamati, Kamati yenyewe ilikuwa na msukumo mkubwa wa jambo hili. Tayari tumeshaanza kazi ya kuzungumza na Wizara husika ili hili jambo lipitiwe tuweze kurekebisha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa msamaha wa kodi mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa *CNG* katika matumizi ya vyombo vya moto ikiwemo magari. Serikali ilishatoa msahama wa kodi ongezeko la thamani (*VAT)* kwa vifaa na mashine mbalimbali zinazotumika katika mnyororo wa thamani kwa miradi ya *CNG* na matumizi ya magari.

Mheshimiwa Spika, mashine na vifaa hivyo pamoja na mashine nyingine zinazotumika katika ujenzi wa vituo hivyo vyote hivi, vina msamaha wa kodi ya *VAT.* Mitungi ya *CNG* pamoja na vifaa vya kufunga mfumo wa kuwezesha magari kwa kutumia *CNG* vyote vina msamaha wa kodi wa *VAT. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imewasilisha Wizara ya Fedha mapendekezo ya maboresho ya *VAT* katika gesi asilia ambayo inatumika katika magari ili kuhamasisha matumizi ya *CNG* kwenye magari ili wawekezaji waweze kupata faida na waweze kurudisha gharama wanazowekeza kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeombwa vilevile kupitia Bunge hili kuwa, ilekeze nguvu zaidi katika uzalishaji wa umeme wa joroardhi na vyanzo vingine vya umeme. Nakubaliana kabisa na

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni hatari kuwa na chanzo kimoja cha umeme pekee yake, lakini pili chanzo cha maji kinaweza kukumbwa na changamoto yoyote kama ambavyo hata chanzo cha gesi kinaweza kukumbwa na changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tumeuona kwa wenzetu wa Zambia, walikuwa na umeme wa kutosha lakini wakapata ukame misimu miwili mfululizo uliowapeleka kwenye mgao. Kwa kulifahamu hilo, Serikali imeamua kwa makusudi kuchukua hatua ya kuongeza vyanzo mbalimbali. Ndiyo maana mtaona kwenye hotuba yangu nimeeleza vyanzo mbalimbali ambavyo tunaviendeleza mbali na vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo Kampuni ya *TGC* ambayo ilianzishwa mwaka 2013 na kuanza rasmi mwaka 2014 inaendelea na kufanya utafiti kwa ajili ya kuongeza *reserve* ya jotoardhi ili tuweze kuendeleza miradi hiyo. Tunayo maeneo zaidi ya 50 nchini kwetu ambayo yamebainika kuwa na joroardhi. Nataka nieleze miradi ya jotoardhi kwa asili ina sifa mbili. Moja, inahitaji muda mrefu sana wa utafiti, lakini pili inahitaji mitaji mikubwa ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, wamejaribu wenzangu kueleza hapa Waheshimiwa Wabunge kwamba tuige mfano wa Kenya kwamba wao wanatumia jotoardhi. Ni kweli, lakini Kenya walianza lini, na miradi ya jotoardhi? Mara ya kwanza nchi ya Kenya kuanza miradi ya jotoardhi ilikuwa mwaka 1950. Wamekuja kupata *plant* ya kwanza mwaka 1981 miaka 31, maana yake ni kwamba hizi ni *project* ambazo ni *capital intensive* na *time intensive* huwezi kuanza leo kesho ukaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo linalotutia moyo kwetu sisi, pamoja na kwamba tumeanza mwaka 2013, tumeshapiga hatua ya mbali sana. Hapa ninaposimama tayari mkandarasi wa kufanya *drilling* yupo *site* na tayari *reserve* ile imeshaonekana. Nataka niwaeleze, hata kwenye bajeti hii tunayoiomba leo ni kwa ajili ya kazi hii. Tumeomba shilingi bilioni 34 ambazo tumetenga kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *geothermal.*

Mheshimiwa Spika, *potential* tuliyonayo kwenye nchi yetu kwenye miradi ya *geothermal* ni Megawati 5,000, maana yake Megawati 5,000 ni mradi mkubwa ambao Julius Nyerere inaingia karibu au zaidi ya mara mbili. Nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge miradi hii mkubali kwamba tunaendelea nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme jua, kwa mara ya kwanza kwenye nchi yetu hatukuwahi kuwa na mradi mkubwa wa *solar*. Sasa hivi tunajenga mradi wa Kishapu Megawati 150 ambao ujenzi wake na utekelezaji wake upo 51%. Serikali inakaribisha sekta binafsi nyingine katika Mfumo wa *IPP,* wale wanaotaka kuja kujenga miradi ya *solar* waje, tunawakaribisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja tuliyoiona hapa ni *tariff*. Wengine wanakuja na *tariff* ya senti 24 hakuna mtu atanunua umeme huo. Hapa Bunge zima linazungumza umeme tunaouza bado ni ghali, akija mwekezaji anataka kuleta umeme kwa *tariff* ya senti 15, 20, haiwezekani, tutakuwa hatuwatendei haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie kuwa miradi hiyo tunaendeleanayo kwa wingi. Miradi ya upepo kwa mfano, mradi wa jua hapa Zuzu megawati 130; Singida, Manyoni megawati 100, Same megawati 100, Singida, Ikungi ya kutumia upepo megawati 100. Hii yote ni miradi ambayo tunaifanyia kazi. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtukubalie tuendelee kufanya hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameeleza kwa uchungu sana kuhusiana na kupeleka umeme vitongojini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Ibara ya 63, Kifungu Kidogo cha (b), kimeeleza hivi, "kukamilisha usambazaji wa umeme katika vijiji vyote na maeneo ya pembezoni mwa Miji ya Tanzania Bara kupitia mpango wa umeme vijijini, pamoja na kuandaa mpango kabambe wa umeme vijijini *(Rural Energy Master Plan)* kabla ya Mwaka 2025." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna eneo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anapaswa kupongezwa sana ni eneo hili. Nasema hivyo kwa nini? Chama cha Mapinduzi mkataba wake na wananchi mpaka kufika 2025 haukuwa vitongoji, ulikuwa ni vijiji tu. Vijiji vimemaliza kabla ya wakati na kabla ya wakati imehamia vitongojini, na vitongoji 64,000 vitongoji 33 vyote vina umeme. Yaani kwa maneno mengine Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi mpaka ikapitiliza kile ilichoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* imeweza kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote 12,318 sawa na vile ilivyoahidi kwenye Ilani yake ya Uchaguzi ya Mwaka 2020. Aidha, katika Ilani ya Uchaguzi 2020, malengo tuliyokuwa tumewekewa sisi ya kuhakikisha kuwa, maeneo ya pembezoni tunayapelekea umeme, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza, visiwa 181 vyote vile tunapambana kuvipelekea umeme katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kuwa mpango tulionao kwa sasa ni kwamba tunaendelea na mpango wa kuongeza vitongoji 9,000 ambavyo vimetangazwa, na wakandarasi wameshapatikana. Nataka niwahakikishie kuwa, hatujui Ilani ya Uchaguzi itatueleza nini baadaye? Sisi tumeanza hata kabla ya hiyo ilani kupeleka umeme vitongojini, ili wananchi waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake kwenye kupeleka umeme. Hili labda niwape ushuhuda Waheshimiwa Wabunge kuwa katika kitu kimojawapo kilichofanya Tanzania kuwa mwenyeji wa *Energy Summit Africa* na kuwaleta wakuu wa nchi wote Afrika, tulivyopimwa na *World Bank,* nchi iliyoongoza kwa kupeleka umeme vijijini tulikuwa sisi, Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa kupeleka umeme kwa wananchi kupitia kile kinachoitwa *Mission 300*, mpango unaochukuliwa kwa mfano, ni Mpango wa Tanzania. Hivi ninavyozungumza hapa, Katibu Mkuu wetu alikuwa Marekani, kwa ajili ya kupeleka mpango wetu kwenda ku-*present,* maana

hiyo ndiyo *model* inayotumiwa na wengine. Inawezekana hapa ndani tukajidharau, lakini huko kwingine nje wanatuona sisi ni wakubwa mno, tunahitaji kuigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tembeeni kifua mbele, tembeeni mkijiamini kuwa Sekta ya Nishati ipo mikono salama chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na sisi wasaidizi wake hatutamwangusha kwenye jambo hili. Tutasimama wakati wote kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata umeme. Huwa ninawaeleza wenzangu kwenye sekta ya nishati, kama kuna sekta haihitaji kusema sana ni hii ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme ukikatika huhitaji maelezo, umekatika. Hayo maelezo mengine baki nayo, watu wanachotaka ni umeme, basi. Hata ungekuja na misamiati yoyote unayoijua, ukajieleza kwa ufundi unaoujua, kama watu hawaoni umeme ni kama tu unapiga gitaa kwa wimbo ambao watu hawaujui. Nataka nikuhakikishie kuwa, tutahakikisha kwa kila linalowezekana kazi ya kupeleka umeme inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imeelezwa kwa uchungu sana, bei ya kuunganisha umeme kwa wananchi vijijini na mijini na mapendekezo yaliyotolewa na kamati. Labda nieleze la kwanza, kwamba, Serikali bei ya kuunganisha umeme kwa sasa ni shilingi 97,000 kwa maeneo ya vijijini na vijiji miji. Serikali inaendelea kuunganisha umeme kupitia mpango mahususi wa nishati *(National Energy Compact)* kwa mwaka wa fedha 2025/2026, yaani bajeti hii tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *REA* imetenga shilingi bilioni 40, ili kuanza kuunganisha umeme wa wananchi kwa shilingi 27,000 katika maeneo mbalimbali yenye sura ya vijiji miji. Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya wastani wa 58% ya gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi, lakini wananchi hulipia kiasi fulani ambacho bado Wabunge wamesema ni kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa tumejadili jambo hili kwa kina kwenye Kamati tuliamua kuunda Kamati kwa sababu, hili ni

jambo linalohusiana na uchumi na linahusiana na fedha, haliwezi kutamkwa bila uchambuzi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa heshima na unyenyekevu mkubwa mtupe muda. Tuna timu tumeiunda ya kwenda kuangalia namna gani tutapunguza gharama ya kuwaunganisha wananchi vijijini kwa ajili ya kuwapelekea umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwenye Mradi wetu wa *Compact* ambao Benki ya Dunia, *FDB,* wanatufadhili pamoja na wafadhili wengine. Tumepewa *target* ya kuunganisha wateja milioni nane, ukijumlisha na wale waliokuwepo, milioni tano, tunatakiwa itakapofika mwaka 2023 tuwe tumeunganisha wateja zaidi ya milioni 12.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeambiana Wizarani kuwa, kwa hali ya kawaida, kama tumeunganisha wateja 5,200,000 kwa kipindi chote toka tumekuwepo, ni muujiza gani huu tutakaokuwanao wa kuwaunganisha wateja milioni nane ndani ya miaka mitano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba, lazima kuwe na utaratibu ambao siyo wa kawaida uliozoeleka, tuliokuwa tukiufanya miaka yote katika uunganishaji wananchi. Mojawapo ni kuangalia ni kitu gani kinachowakwamisha wananchi kuunganishwa na huo umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Mbunge ameeleza hapa kwamba, moja ni gharama, lakini pili ni hizi gharama zote hawaziwezi wananchi. Tumeunda hiyo timu ikatufanyie uchambuzi ituletee majibu na ninaamini wakati fulani tutawahusisha na Waheshimiwa Wabunge, ili mweze kujua ni kitu gani mnachokifanya.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kuwa, tunalifanyia kazi jambo hili, ili uunganishaji uweze kuwa rahisi na hili linalozungumzwa la watu kuweza kuunganishiwa umeme kwa bei nafuu tutalifikia. Niunganishe hilo hilo pamoja na gharama za umeme. Gharama za umeme *(tariffs)* kwenye nchi yetu hazijapitiwa kwa muda wa miaka 10. Kwa sasa tunazipitia kupitia *EWURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba mnikubalie, kwamba jambo hili ni la kiuchumi, ni la kisayansi, linahitaji uchambuzi na kuwashirikisha wadau mbalimbali watoe maoni yao. Naomba tuwape nafasi *EWURA*, kama *regulator independent* afanye kazi yake bila kumwingilia, ili atuletee taarifa hizi za gharama ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini, na nini kifanyike, ili wananchi waweze kupata nishati ambayo inahimilika? Kwa hiyo, hili na lenyewe tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imeelezwa hapa habari ya vituo vya kupooza umeme, ili kukabiliana na changamoto ya kukatika umeme. Serikali ilikuja na Mpango wa Gridi Imara kwa kujenga vituo vya gridi vya kupooza umeme kwa kila wilaya. Hatua zifuatazo zimechukuliwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja, tumeshanunua viwanja, kwa ajili ya kujenga vituo, kwa ajili ya wilaya zote nchini. Pili, tumeamua kujenga kwanza vituo 14 vya kuanzia na Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, Wakili Olelekaita, ni mmojawapo wa watakaoanza kujengewa katika awamu ya kwanza, lakini utekelezaji utaendelea katika wilaya nyingine kadiri tunavyoendelea na wilaya nyingi zinahakikishiwa kuwa, tunazijengea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji vituo 216 vya kupoozea umeme katika nchi yetu. Vilivyopo ni vituo 132. Maana yake ni kwamba, tuna upungufu wa vituo 84. Kituo cha kupoozea umeme cha *grid (grid substation),* gharama ya kujenga kituo kimoja ni shilingi bilioni 35, *it's expensive* na kituo cha kawaida, kile kinachopokea umeme kwenye msongo wa kilovoti 33, kituo kimoja ni shilingi bilioni nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba, zinahitajika fedha nyingi ili tuweze kujenga. Hatuwezi kufanya vyote mara moja, tunachohitaji ni mahali pengine tutaweka *switching station,* ili tugawanye njia. Kwa mfano, pale Mto wa Mbu kwa sababu, ile *line* ya kutoka Arusha kwenda mpaka Ngorongoro ni ndefu sana, ile *line* peke yake ina urefu wa kilometa 1,400. Maana yake ni

kwamba, *line* yote ile haina *substation*, haina chochote, hata akitokea mtu anaendesha gari akagonga nguzo moja, maana yake ni wote walio upande mwingine wanakosa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeamua kuweka mkakati maalumu wa kuweka *switching station* kwenye maeneo ambayo tunadhani ni nafuu, ili tuweze kutenganisha hizo njia, watu waweze kupata umeme. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hasa wa Mkoa wa Lindi, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Kuchauka, ni kweli, Lindi kule wanachukuwa umeme kutoka kwenye Kituo chetu cha Makumbika, ni mbali sana. Ukienda Liwale kwa Mheshimiwa Kuchauka umeme unakatika sana. jamani Waheshimiwa Wabunge, umeme haukatiki kwa sababu, hakuna umeme, unakatika kwa sababu ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwape taarifa ndogo. Juzi tumezindua Taarifa ya *EWURA* hapa, wakati tumezindua ile Taarifa ya *EWURA* tumeonesha kwa mwaka mmoja tatizo la kukatika umeme limepungua kwa kiasi gani? Hili tulikuwa tunazungumza mpaka tunakuja kumaliza mwaka 2024. Kukatika kwa umeme katika nchi yetu, kwa Taarifa ya *EWURA* iliyofanyiwa utafiti, kumepungua kwa 48% na dakika za kukatika umeme zimepungua kwa 64%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipotoka hali ilikuwa mbaya zaidi kuliko tulipo hivi sasa. Sehemu nyingi ukiona umeme unakatika ni mahali ambapo tunatengeneza miundombinu. Lazima tukubali kwamba, hatuwezi kula keki na tukabakinayo. Wakati tunajenga hii miundombinu ni lazima tutazima umeme mahali fulani, ili tuweze kujenga hiyo miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tumetoka kwenye dakika 1,536 mwaka 2022 mpaka dakika 5,554 mwaka 2024, tumepunguza kukatika kwa umeme kwa 68%. Naomba mtuamini kuwa, hili jambo tunalifanyia kazi, tena hakuna jambo linawakera wananchi kama kukatika umeme, hasa kama hawajapewa taarifa. Ndiyo maana tumeamua kituo chetu cha huduma kwa wateja tukiimarishe, umeme unapokatika watu wapewe taarifa.

Mheshimiwa Spika, tulizoea kutoa tangazo tu mara moja, tunawapa taarifa kuwa umeme umekatika kwa sababu hizi na hizi. Tumeamua, kila wilaya, kila Mkoa, kuwe na ma-*group* ya *WhatsApp*, meneja kazi yake awe *admin* kwenye yale ma-*group* kuwapa taarifa watu maana siku hizi wananchi, hata mimi wananiandikia *message*. Umeme ukikatika wanakuandikia *message*. Natamani sana waendelee kufanya hivyo kwa sababu, kwa kufanya hivyo, wanatu-*hold accountable* kila mmoja kujua wajibu wetu, kuwapatia umeme Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja lenye upekee ambalo nimelisikia hapa ni kuhusu *transformer* tano ambazo zimeungua, Ngara. Imenisikitisha na ikaniogopesha kwamba, *transformer* tano zinaungua halafu hatujafanya kazi. Baada ya kufuatilia pia, nimegundua kuwa, mkandarasi aliyepewa hizi *transformer* zilikuwa chini ya uangalizi wake kwa hiyo, alipewa wajibu wa kuzibadilisha ili aweke *transformer* nyingine.

Mheshimiwa Spika, nimewaelekeza leo *TANESCO* kwamba, sisi tupeleke hizo *transformer,* wananchi wasihangaike, halafu ninyi *TANESCO* mdaiane na huyo mkandarasi. Kwa sababu hiyo, wananchi wa Ngara ndani ya wiki hii mpaka wiki inayokwisha *transformer* zote zile ziwe zimebadilishwa na wananchi wapate umeme bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni upungufu wa wafanyazi ambao Waheshimiwa Wabunge wameueleza. Nataka kutoa taarifa tu kuwa, tumepata kibali cha kuajiri watumishi 570 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Utaratibu unakamilishwa watumishi hao waweze kupangiwa majukumu hayo. Vilevile Serikali imepanga kuajiri watumishi wengine 1,000 katika mwaka wa fedha 2025/2026, ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadiri tunavyoendelea kusambaza umeme ndivyo mahitaji ya watu wa kuhudumia hizo *line* yanavyoongezeka. Kwa hiyo, tumepata nafasi ya kuajiri watu wengi zaidi ili tuweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza suala la vitendea kazi, hususan magari, ili kupunguza changamoto ya usafiri huo katika Wilaya za ki-*TANESCO* mwaka huu wa 2024/2025. Serikali imefanya manunuzi ya magari 50 ambapo magari haya yamesambazwa katika mikoa na wilaya zenye uhitaji mkubwa. Magari hayo yanatarajia kupelekwa mwezi Agosti na aidha itakapofika Septemba, 2025 magari haya yatakuwa yamefikishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye mwaka huu wa fedha, kwenye bajeti hii tunayoomba, *TANESCO* imetenga fedha za kununua magari 200, ili kuendelea kupunguza changamoto hii ya kuwapatia huduma wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo machache nilitaka nichangie na kujibu hoja kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini nimalizie kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwamba, mmetutendea wema mwingi mno kwa kutusimamia na kutushauri. Nawashukuru sana na kwa kweli, nawaombea kwa Mungu, kila mmoja aliyemo humu, wananchi wake mahali popote walipo, waangalieni Wabunge hawa kwa jicho la wema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, kama kuna mtu anapewa kazi, kwa kawaida anadaiwa hesabu mikononi mwake. Waheshimiwa Wabunge hawa hawadaiwi kwa sababu kazi wameifanya, wamezungumza, wengine wakati wanaingia kwenye uongozi walikuwa na maeneo hayana umeme, wamesema hapa vijiji vyote vina umeme.

Mheshimiwa Spika, kama walikuwa wanasema kuna maeneo hayakuwa na zahanati na vituo vya afya, wanaeleza wakiwa Bungeni, sasa vijiji hivyo vina zahanati na vituo vya afya. Kama walikuwa wanasema kuna maeneo hayakuwa na *high school,* wakiwa humu Bungeni, sasa wanasema maeneo yao yana shule na *high school.* Kama walikuwa wanasema, wanatamani kujengwe Vyuo vya *VETA* kwenye maeneo yao, wakiwa kwenye nyumba hii, kunajengwa Vyuo vya *VETA* kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walikuwa wanasema, wananchi walikuwa wanahangaika na ruzuku ya mbolea na pembejeo za kilimo, pamoja na usimamizi mzuri kwenye sekta ya kilimo, wakiwa kwenye nyumba hii, leo wanasema ruzuku ya kilimo inapelekwa. Kama walikuwa wanasema mitandao ya barabara ilikuwa kidogo kwenye maeneo yao, wakiwa kwenye nyumba hii, wanasema mitandao imeongezeka na wanahitaji fedha zaidi barabara ziboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamefanya kazi yao, ikiwa mwanadamu hataona, basi mbingu zitaona. Nawaombea Waheshimiwa Wabunge kwamba, tembeeni kifua mbele mkiamini kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuijenga hii nchi, tena siyo kwa maneno. Mheshimiwa Rais anapenda kusema kidogo na kutenda zaidi. Ametufundisha falsafa, "nia njema haishindwi." Tembeeni mkiwa na nia njema ya kuwahudumia Watanzania, nami ninaamini kwa sababu, nia njema haishindwi, ninyi mtaibuka washindi na Mungu awasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi wa Mbeya, hatuna cha kuwafundisha, mnajua cha kufanya. Mshairi mmoja alisema, "usione, ukadhani." Nafikiri wakati fulani watu wa Mbeya walikuona wakadhani, lakini umethibitisha sio Tanzania, lakini na dunia kwa ujumla, kwamba Tanzania, nchi mojawapo katika Ukanda wa Afrika Mashariki inaweza ikamzaa binti, ikamlea, ikamsomesha, ikamfanya kuwa mtu wa msimamo wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, umelithibitisha hilo kwenye Mabunge ya Dunia. Umetupa heshima Watanzania. La muhimu zaidi umempa heshima mtoto wa kike wa nchi yetu. Tunawaomba watu wa Mbeya, kama kuna jambo mlilowahi kufanya jema ni kutuletea Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na kama kuna jambo Chama cha Mapinduzi kiliwahi kufanya ni kumteua na kumleta tumchague, Dkt. Tulia Ackson kuwa Spika wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajifunza mengi kwako pamoja na wasaidizi wako, Mheshimiwa Zungu na Wenyeviti wote wa Bunge hili, kwa namna mnavyotuendesha. Kwa kweli, mahali ambapo kanuni zinakiukwa unakuwa mkali, hata kama ni rafiki yako

huangalii uso wa mtu, lakini mahali ambapo mtu anahitaji haki, anaipata. Tunawatakia kila la heri viongozi wetu wa Bunge hili, mwendelee kutusimamia vizuri na sisi kama Wabunge tulio kwenye nyumba hii tutaendelea kuwaombea na kuwatakia kila la heri ili kazi yenu iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo nilitaka niliweke vizuri, kuna mkanganyiko mdogo umetokea wakati wa michango ya Waheshimiwa Wabunge. Kutenganisha kati ya gesi ya *LPG* na *natural gas*. Niliona *clip* moja ya mtu mmoja, nazungumza Watanzania ni kama hatuna akili. Gesi ipo hapa Mtwara, mnaenda kununua gesi ya kupikia India na mahali kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ni suala la uelewa tu. *Natural gas* na *LPG* ni gesi mbili tofauti zenye matumizi mawili tofauti, na zenye *chemistiry* mbili tofauti. Sasa kwa sababu, mimi pamoja na kwamba, ni Mwalimu, siyo kazi yangu kusimama hapa na kufundisha. Naomba unikubalie, unitengee siku moja wataalamu wangu wafanye semina kwa Wabunge wote, ili tujue tu tofauti ya *LPG* pamoja na *natural gas,* ili tuone tofauti hiyo ipoje, halafu tuweze kuichangia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa nafasi, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ili mpige makofi vizuri ni lazima muwe mmekaa sasa. Hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Basi kama ilivyo ada tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Mgt*.............. Sh. 5,600,498,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 1,417,700,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*..................Sh. 1,806,052,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit* ..........................Sh. 728,610,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit* .........................Sh. 709,258,000
Kifungu 1006 – *Government Comm Unit*...................Sh. 719,439,000
Kifungu 1007 – Procurement *Management Unit*.......Sh. 907,954,800
Kifungu 1008 – *Environment Management Unit*...... Sh. 597,224,000
Kifungu 1009 – *Management Info System Unit*..........Sh. 727,556,000
Kifungu 1010 – *Monitoring and Evaluation Unit*.........Sh. 876,632,000
Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*......................................Sh. 56,147,352,000
Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*..........................Sh. 8,149,206,200
Kifungu 3003 – *Cleaning and Cooking Unit*.................Sh. 844,744,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* ................. Sh. 3,000,000,000
Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*.........................................Sh. 1,995,181,219,000
Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*…....................Sh. 169,332,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa Hoja Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASALI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, wanaoafiki hoja ya

Mheshimiwa Waziri wa Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki, ahsante sana. Sasa kabla sijasema machache, nitangaze rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yamepitishwa rasmi na Bunge.

Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na ninyi Waheshimiwa Wabunge mmepata nafasi ya kuchangia, mambo mengi yamefanyika huko kwenye maeneo yenu, lakini pia katika hii bajeti wametoa ahadi nyingi za kuwafikia wananchi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, upande wa kushoto mnazungumza kwa sauti nikiwa nimesimama. Waheshimiwa Wabunge mlio upande wa kushoto mnazungumza kwa sauti nikiwa nimesimama.

Mheshimiwa Waziri tunakupongeza sana kwa ahadi zilizotoka kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi kwenye matumaini ambayo Watanzania wanapaswa kuwa nayo, hasa katika kuhakikisha umeme unamfikia kila Mtanzania.

Mawazo ambayo wameyatoa hapa Waheshimiwa Wabunge umeyajibu na umesema baadhi yake umeshaunda timu na mengine unakwenda kuunda timu kwa ajili ya kuyafanyia kazi ili wananchi wote waweze kupata umeme katika hali

ambayo haitakuwa mzigo sana kwao. Kwa hiyo, tunakushukuru sana.

Pia, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa namna ambavyo anakusaidia kwenye kazi nyingi maana kama wewe ulivyosema mwenyewe majukumu yako ni mengi, na Mheshimiwa Naibu Waziri anajitahidi kukuwakilisha vizuri katika maeneo mengi ambayo pengine wewe usingeweza kufika kwa sababu ya majukumu uliyo nayo. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakutakia kila la heri katika utekelezaji wa hii bajeti pamoja na kumsaidia vyema Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Tunawapongeza pia watendaji wote na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao hasa yale ambayo Wabunge wameahidiwa hapa kwa niaba ya wananchi wote wa Taifa hili, kuhusu maendeleo yao kwenye hili eneo la nishati.

Waheshimiwa Wabunge, pia namshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa hii Kamati wamefanya kazi nzuri sana ya kuisimamia Wizara hii, tunawashukuru. Wabunge wote, mmeweza kufanya kazi yenu vizuri kabisa na sitayarejea maneno ambayo wameyasema hapo Mheshimiwa Waziri wa Nishati, lakini pia na Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge leo kulikuwa kuna makofi mengi sana hapa kuashiria kwamba maombi ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu yafike huko majimboni. Kwa hiyo, nikagundua hata tulipoingia Kamati ya Matumizi sikuhitaji kusisitiza watu kuitikia kwa sauti, kila mtu alikuwa anaitikia kwa sauti kubwa sana. Kwa hiyo, kila mmoja, kila la kheri. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati amesema hapa kuhusu umuhimu wa mafunzo kutokana na hayo ambayo ameyasikia kwa baadhi ya Wabunge, na pia yamesikika huko kwa wananchi ambao sisi kama wawakilishi wao, tukiweza kupewa hii elimu, basi tutaweza kuwafikishia wananchi nao kupata uelewa ule ambao tutakuwa tumepewa.

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati sisi tuko tayari kabisa kwa ajili ya haya mafunzo ili yale ambayo pengine wananchi wanakuwa wamechanganya hapa na pale, na sisi wenyewe tumechanganya hapa na pale ili hayo yaondoke kabisa.

Kwa kuwa mjadala unaweza ukarejea tena wa kuhusu nishati tutakapokuwa tunajadili ile Bajeti Kuu, basi mafunzo hayo yafanyike kabla haijasomwa, ili iweze kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia kwenye hilo eneo la nishati. Itakapofika wakati wa Bajeti Kuu, wote tuwe tumeelewa kuhusu tofauti ya...

Nilikuwa ninatafuta Kiswahili, naona kimenipita kidogo, lakini *LPG* na *LNG*. Basi siku nyingine tutasema kwa Kiswahili, mniwie radhi.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine, Mheshimiwa Kingu alisimama hapa kueleza jambo ambalo limefanyika kwa nchi yetu, ni heshima kubwa sana. Sasa sikuwa nimetoa pongezi kwa ndugu yetu aliyeshinda nafasi hii, lakini sababu ilikuwa ni kwamba mkuu wa msafara ambao ulikuwa umeongoza hili ni Naibu Spika na alikuwa hajarejea bado. Sasa tunaye Naibu Spika hapa Bungeni, kwa hiyo nitumie fursa hii kuwashukuru sana sana Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, kwa kuongoza kikosi ambacho kilienda huko Angola kutuwakilisha sisi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda huko kuhakikisha tunashinda hiyo nafasi ya Katibu Mkuu wa Jukwaa la Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu. Kwa kweli Mheshimiwa Naibu Spika amefanya kazi nzuri, kikosi kimerudi na ushindi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zungu aliongozana, na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, tunakushukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya huko. Pia alikuwepo Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, naye tunamshukuru sana kwa ushirikiano mkubwa alioutoa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye Jukwaa hili Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwa linawakilishwa na

Wabunge ambao ni Mheshimiwa Shamsia Mtamba, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, na Mheshimiwa Ezra Chilewesa. Waheshimiwa Wabunge hawa wameweka huko mahusiano mazuri ambayo yametuwezesha sasa kufika sehemu nzuri ambayo tumeshinda hiyo nafasi sisi kama nchi. *(Makofi)*

Japokuwa mtakuwa mmeona kwenye vyombo vya habari ikiitwa kwamba ni uteuzi na mambo kama hayo, lakini ni kwamba huko kulikuwa na ushindani; na bila shaka mtakubaliana na maneno ambayo ameyasema Mheshimiwa Kingu na mengine ambayo wameyasema Watanzania mahali pengine, juu ya kazi nzuri inayofanywa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kubaki kwenye ramani ya dunia, na pia kuendelea kuwa na ushawishi katika dunia; na sasa mnaona nafasi nyingi ambazo Tanzania tunaweza kuzipata. Hata sasa ziko nyingi ambazo Watanzania wanagombea. *(Makofi)*

Ninyi mmeona Mheshimiwa Rais wetu namna ambavyo amekuwa akijitoa kwa hali na kwa mali. Kwingine anapiga simu mwenyewe, wakati mwingine inabidi azungumze yeye mwenyewe ili watu waelewe kwamba huyu mtu anatoka Tanzania, lakini pia Rais wake na Serikali yote na nchi yake yote wanampendekeza huyo mtu ama wanatamani mtu huyo aongoze; na kwamba Tanzania iko tayari kabisa kumpa ushirikiano. Ni jambo kubwa sana linalofanywa na Mheshimiwa Rais, kwingine hatuyaoni hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa namna ambavyo anaimarisha demokrasia, na pia diplomasia, maana yote mawili yanakwenda pamoja; demokrasia na diplomasia, na ndiyo inayotuwezesha kuendelea kuwa na ushawishi huko nje kama Watanzania. *(Makofi)*

Sasa hizi ni baadhi tu ya nafasi ambazo tunashinda. Baadhi yenu mnafuatilia na wengine pengine hamfuatilii sana, ndiyo maana Watanzania wanakuwa kama wanajiona ni wadogo sana

hivi ama mahali pengine watu wanasema kauli zinazoashiria kama vile tunajidharau wenyewe. *(Makofi)*

Sasa hivi, huduma za afya, nadhani zinaitwa hivyo kwa Kiswahili, *medical services* za *AU* zinaongozwa na Mtanzania ambaye ni Daktari kutoka Muhimbili, na ameanza kazi Februari. Kwa hiyo, haya mambo yako mengi na ni muhimu sana sisi kama viongozi, kwa kweli ninadhani Wizara itakapokuwa inakuja hapa, Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni muhimu itusomeesomee yale mambo huko nje Tanzania inashika nafasi zipi, ambazo haziji bure Watanzania wenzangu, lakini haziji bure Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Zinakuja kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Sasa kijana wetu ambaye ameshinda hiyo nafasi ya kuwa Katibu Mkuu wa Jukwaa la Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu anaitwa Dkt. Deo Mwapinga. Siku atakayokuja hapa Bungeni, basi tutamtambulisha kwenu rasmi. Ila kwa sababu ndiyo ametoka kushinda hiyo nafasi, kwa hiyo, kuna mambo huko mengi mengi yanaendelea. Atakuja hapa Dodoma kabla hili Bunge halijaisha na tutamtambulisha kwenu bila shaka ili mjue Bunge lenu limefanya kazi nzuri sana, na kwa kushirikiana na Wabunge wengine huko nje na hasa Maspika ndio wanaofanya uamuzi wa nani awe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, siku hiyo sasa tutazungumza pia kuwashukuru Maspika wengine kwa ushirikiano ambao wameutoa tulipompeleka huyu wa kwetu kwamba sote tumchague na wakakubaliana na ushawishi wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.56 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 30 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*